Hekima Dhidi Ya Imani

Asante, Ndugu Neville. Bwana akubariki. Habari za asubuhi, habari za asubuhi. Ndugu . . .

2 Habari za asubuhi, marafiki. Nina furaha kurudi katika nyumba ya Bwana!

3 Ndio kwanza nipige simu huko nyuma, dakika chache zilizopita, kumwombea mhudumu mzee. Naye alikuwa tu amezimia kwa muda kidogo, kitu kama hicho. Hakuna kasoro iliyopatikana kwake. Yeye ni mzee mtakatifu tu wa Bwana. Nikiwa barabarani kuja hapa, Shetani alijaribu kunifanya mgonjwa, kutapika, pia. Nikasema, "Itatubidi tu kuombeana." Hiyo ni kweli. Naam. Kwa hiyo, ilikuwa ni Ndugu Coggins. Tunamfahamu vizuri sana, hapa maskanini. Anatoka huko Carolina. Naye amekuwa mgonjwa, mgonjwa sana, anasimama tu na ku—kuzimia tu kwa muda kidogo. Lakini haonekani kuwa na kasoro yoyote, si ya kimwili. Kwa hiyo, ni ibilisi tu akijaribu kumjaribu. Kwa hiyo, yeye ni mjaribu mkuu, naye ni mzuri, pia.

4 Mliisikia hadithi ya maskini dada kizee aliyeenda kanisani, asingeweza kusema lolote baya juu ya mtu yeyote. Kasema, "Waonaje juu ya ibilisi?" Akasema, "Vema, yeye ni adui mzuri." Kwa hiyo hivyo ndivyo yeye—ndivyo alivyo.

5 Tuna furaha, asubuhi ya leo, kuwa katika nyumba ya Bwana tena, juma hili, tukikungojea Kuja kwa Bwana Yesu.

6 Na sasa, nilikuwa nikitaka kuzungumza juu ya somo, asubuhi ya leo, "Kukingwa na Damu," na ilionekana kana kwamba Roho Mtakatifu kidogo alibadilisha nia yangu juu ya hilo. Nami ninalo somo lingine, la mafundisho. Kwa sababu, basi, baada ya, nilisema, jana usiku, "Mbona abadilishe nia yangu juu ya somo la namna hiyo, 'Kukingwa na Damu'?" Mnafahamu ambapo hilo somo lingekuwa, "Israeli chini ya damu, wakienda taratibu kwenye ile ahadi," mnaona. Basi huenda nikalizungumzia, wakati mwingine.

7 Kwa hiyo nilikumbuka, katika ndoto niliyokuwa nayo hapa, sio muda mrefu uliopita. Nami, katika ndoto hii, nilipaswa kuwa nikiweka Chakula akiba maskanini, mnaona, hapa katika ndoto hii. Ni wangapi wanaoikumbuka, majuma machache yaliyopita, nikiwa na ndoto hiyo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Nisingewapa tafsiri yake. Na endapo haitanichukua muda mrefu sana, nitawasimulia tu, iwapo mngetaka kusikia. ["Amina."] Vema.

8 Ni kwa nadra ambapo mimi huota chochote kilicho na maana yoyote kwake. Ni, kwa kawaida, ninaenda kulala nimechelewa, kisha ninaamka. Nami nimeshikwa na wasiwasi

ama nimechoka, unaota, ndipo unaenda kulala na kuota, kisha unaamka. Mnajua jinsi ilivyo, mtu mwenye wasiwasi kama mimi.

9 Nami nilikuwa nimetoka na Ndugu Wood na Ndugu Sothmann, naye Bwana alikuwa tu akiwapa watu...wakija na...chini...Na hii ilikuwa ni huko Tucson, Arizona. Naye Bwana kikamilifu tu, katika kila kisa, akitoa fasiri za ndoto.

10 Sasa, mnaona, wakati mtu yeyote anaposimulia, anaponiambia juu ya ndoto, njia pekee niwezayo kutoa fasiri yake, mimi huiona hiyo ndoto tena. Na wengi wenu hapa mnajua, ya kwamba baadhi yenu mkiniambia mambo, kwamba hamkuniambia yote kuihusu, katika hiyo ndoto. Lakini nilipoipata, tena, nilipata yale ambayo hamkuniambia. Mnaona? Na kwa hiyo inakubidi kuiona tena, kisha Yeye anakwambia. Kwa hiyo, wakati mwingine inakata. Wakati mwingine ni ngumu, haikubaliki kwa mtu huyo. Lakini inakubidi kuwa mkweli, kwa kuwa ni Neno la Bwana. Mnaona? Maana, wao wanatarajia hilo. Na Hilo kamwe...Bwana amekuwa mwema kwangu, kuifanya iwe sahihi sikuzote.

11 Na kwa hiyo usiku huo ni—nilienda kulala, nami nikaota, mimi mwenyewe. Na nilidhani nilikuwa...Jamaa mmoja aliyekuwa akipigana ngumi pamoja nami, miaka kadhaa iliyopita. Wengi, ninyi watu wa zamani...

12 Nilikuwa tu nikiwazia juu ya Ndugu Roy Slaughter, amesimama pale mlangoni. Amekuwa nayo, nadhani mmoja wa washiriki wa zamani sana hapa, kanisani. Ndugu Slaughter, nadhani, ni karibu mmoja wa washiriki wa zamani sana. Nami ni—nilininii tu...

13 Wakati nikizungumza habari zake, kuna mambo mengi mazuri juu ya Roy Slaughter ambayo watu hawayajui. Hiyo ni kweli. Yeye ni ndugu yangu, na afadhali nimpe shada dogo sasa, ama chipukizi, kuliko shada zima la maua akiisha kutuacha. Hiyo ni kweli. Kuna mambo mengi mazuri. Ndugu Roy amekuwa ni ndugu halisi kwangu, yeye na familia yake, anaishi huko nje, na alifanya bidii kwa ajili ya familia hiyo ndogo, naye akawalea kundi zuri la watoto. Niliwajua wasichana wake wote na wavulana wake, nami nilihubiri kwenye mazishi ya mvulana wake mdogo alipokufa.

14 Nami nakumbuka, wakati mmoja hapa, tulikuwa na jamaa fulani akifanya kazi kanisani. Na...Naye alipaswa kuifanya, kama seremala tu. Hatukuwa na fedha nyingi. Naye alikuwa akienda kutengeneza upande huu wa ndani. Ndipo mtu fulani akaja aliyetaka kufanya kazi, wala hakuifanya. Naye akaketi huko, akadai alifanya kazi nusu saa, ama kitu fulani, na kuumiza mguu wake. Ndipo yeye, ya kutosha tu kulishtaki kanisa, naye akatushtakia dola elfu kumi. Vema, hatukuwa na kitu. Hatukujua chochote juu yake mpaka walipokuwa wametoa

hukumu. Mnaona, walishtaki. Hu—huyo mtu, hakuwa na bima, na kwa hiyo ikatuangukia. Hatukuwa nayo, kulipa.

15 Wala sitausahau usiku huo, tukiketi papo hapo, *pale* nyuma ndani, kwamba Roy aliingia mfukoni mwake. Ninii cha kale . . . Samahani, Ndugu Roy. Kitabu cha mfukoni kilichoparuza, na kutoa hundi alizokuwa nazo kutoka kwa kuvuta kwake mtunguo, vitu kama hivyo. Kasema, “Vema, Ndugu Bill, nitaweka hizi kwake.”

16 Maskini Evelyna mkongwe, dada yake, huenda ameketi papa hapa, mahali fulani sasa. Yeye, “Ndugu Branham, maskini nyumba yangu ndogo, ina thamani ya dola mia tatu pekee, bali itatubidi tu kuweka hiyo kwake.” Mnaona? Hizo ni nyenzo za kweli, halisi, ukizungumza nami. Hayo yako katika kitabu changu, hayo ni halisi.

17 Nakumbuka basi, baadaye kidogo kutoka hapo, niko kwenye mkutano wangu wa kwanza nje. Nilikuwa huko St. Louis, katika mmoja wa mikutano yangu mikubwa ya kwanza. Ndipo barua ya simu ikaingia, “Msichana wangu mdogo ni mahututi. Ndugu Slaughter. Njoo mara moja.” Nilienda tu kule, nikaanza kuweka nguo zangu kwenye sanduku. Hakukuwa na lingine. Kamwe nisingemkatalia. Nasi hapa tunakuja. Nikaja nyumbani, nikaingia chumbani. Wauguzi, kule chini, hospitalini kule, kwenye hospitali ya Katoliki huko New Albany, walikuwa wamemkatia tamaa maskini msichana wake. Wakati tu tukiingia chumbani, Bwana Yesu akamponya. Huyo hapo, mnaona. Mnaona?

18 Na kama vile mkate juu ya maji, itakurudia siku moja. Niko nje ya somo langu; lakini nitarudi mwanzoni.

19 Nami nilikuwa nikifanya ubondia. Basi palikuwapo na jamaa aliyeitwa hapa kwenye mji huu. Maskini jamaa huyo hunywa pombe sana sasa. Mmoja wa wavulana wake yuko kwenye kikosi cha polisi. Smith, George Smith, ndivyo wanavyomwita, “Smith wa sekunde sita.” Alianza kunifundisha kupiga ngumi, wakati tulipokuwa . . . kabla zile Glovu za Dhahabu hazijaanza. Tulikuwa huku nje kwenye makao ya serikali. Na katika hilo, mbona, yeye alikuwa ndiye mtu mwenye fujo kuliko wote niliopata kuona. Yeye angenipiga tu, nami ningeenda nikipindapinda hewani. Kisha narudi. Nikasema, “Si lazima uwe mkali hivi kulihusu. Unaona?” Nikasema, “Unanitoa pumzi kwa ngumi.”

20 Akasema, “Nakwambia, Billy,” kasema, “haidhuru umefunzwa vizuri jinsi gani, na una ujuzi wa riadha jinsi gani, na jinsi ulivyo na nguvu, kwa uzito wako, ama chochote namna hiyo,” kasema, “ngumi huikomesha damu inapopigwa namna *hiyo*.” [Ndugu Branham alipiga makofi—Mh.] Kisha kasema, “Huenda ukanichukia mimi sasa, bali utakapoingia mle kwenye ulingo, wewe mwenyewe,” kasema, “utalithamini.” Kasema,

"Mwili wako unajiimarisha hivyo, kurudi upesi. Kama ukipigwa konde, utaanguka tu, ukae hapo na kuhesabiwa. Lakini iwapo mwili wako umeimarishwa na unaweza kustahimili hivyo vipigo," kasema, "basi, unapoupiga, kipigo kikali kinakuangukia," kasema, "basi wakati wewe . . . unaweza kurudi upesi," kasema, "kusimama kwa miguu yako tena. Upigwe utupwe nje ya ulingo, uruke ndani tena." Alikuwa tu amemaliza kunipiga konde kanirusha moja kwa moja nje ya ulingo. Kwa hiyo kasema, "Inakubidi tu kufanya hivyo. Unaona?" Naye karibu aniue. Yeye alikuwa na uzito wa yapata pauni thelathini ama arobaini zaidi ya nilivyokuwa mimi. Naye angeweza . . . Alikuwa ni mpiganaji nami nilikuwa tu ni mwanafunzi, kwa hiyo alikuwa karibu aniue. Akasema, "Lakini utathamini hilo utakapoingia kwenye ulingo." Nilikuta kwamba hiyo ilikuwa ni kweli.

21 Kisha, nimewasikia hao masajini jeshini wakiwafunza hao wavulana, na wagumu. Wangemchukia sajini huyo. Lakini inapofikia kwenye mashambulizi, walimpenda, kwa sababu ya mafunzo magumu sana.

22 Hivyo ndivyo nilivyojaribu kuwafunza Wakristo. "Msikate nywele zenu. Msijipodoe. Msifanye *hivi*." Iweni wagumu. Mtanithamini nitakapokuja kwenye—kwenye mwisho wa safari yangu. Mnaona? Kufunzwa, mnaona, kufanya mafunzo hayo vizuri. Bali hebu—hebu tudumu moja kwa moja na Neno. Huenda likawa ni kali, linakatakata tofauti za kimadhehebu vipandevipande, lakini utalithamini utakapofika mwisho wa safari. Unaona? Ulisimama na kile Kitabu.

Kwa hiyo, mke, alinishika mkono, nasi tukatembea.

23 Naye George Smith sasa, yeye, nadhani, ni mtu mwenye mvi. Nadhani amenishinda umri kwa miaka saba au minane, kumi. Naye alikuwa amerudi kwenye ulingo, naye alikuwa akipigana vikali. Nao jamaa hawa vijana walioibuka, wavulana wenye mabega mapana, wasingeweza kumstahimili, hata kidogo. Walininii tu . . . Yeye angewapiga katika dakika moja. Basi kijana mmoja akasema, "Ninaweza kumshinda huyo mzee. Najua ninaweza." Kwa hiyo yeye, jamaa mkubwa wa kiriadha, akaruka kwenye ulingo pale. Hakudumu nusu dakika. Akarudi nje, kasema, "Sijui inatoka wapi, bali hakika yeye ni mwanamume."

24 Ndipo mara ghafla, nikamwangalia mke wangu, katika ndoto, nami nikasema, "Mke wangu, wajua, yeye alinipa mafunzo yangu ya kwanza."

25 Halafu basi, mnajua, ndoto zinachekesha. Nikashuka kwenye ba—bahari kubwa, nayo maji yalikuwa yenye mawimbi-mawimbi sana. Naye baharia . . . Sasa, Meda hakuwa pamoja nami wakati huo, mke wangu. Halafu basi, katika jambo hili, hu—huyo baharia akaja hapo, naye akanipa mtumbwi

mdogo wenye urefu wa kama futi mbili na nusu, futi tatu. Naye akasema . . . Ulikuwa ni mweupe kabisa, plastiki tu, na mweupe. Akasema, “Huu hapa mtumbwi wako.”

“Loo,” nikasema, “nisingeweza kuvuka, kwa huo, katika huo.”

26 Akasema, “Vema,” kasema, “huo utaenda mbio maili hamsini kwa saa, huku na huku *hivi*.”

27 Nikasema, “Huenda ukaenda, huku na huku ufukoni, bali hautaenda *huko* nje. Unaona?” Nikasema.

28 Akasema, “Vema, nenda nao.” Nikaangalia, na hapa aliketi Ndugu Wood, na Ndugu Fred Sothmann, hao ndugu wawili walikuwa pamoja nami usiku nilioota ile ndoto. Nao walikuwa wameketi katika mtumbwi wa kijani kibichi wenye kamba nyingi sana, kamba za kupiga kambi, mahema, na kadhalika. Nao walikuwa wameketi pale. Akasema, “Nenda pamoja nao.”

29 Nikasema, “Hao hata si mabaharia.” Nikasema, “Ninajua hivyo.” Nikasema, “Mimi ni baharia. Nami na—najua kuhusu mtumbwi, kuuendesha. Lakini,” nikasema, “hawa, hawataweza kamwe. Wasingeweza kufaulu. Nisingeenda namna hiyo, kwa vyovyote vile.”

30 “Vema,” yeye akasema, “wao wanakupenda.” Kisha kasema, “Kwa nini usirudi huku juu ukaweke akiba?”

31 Kwa hiyo, nikarudi. Na mahali hapo padogo tulipokuwa, mahali padogo paitwapo Klondike, yapata maili arobaini kutoka kwenye ustaarabu, duka moja dogo kwa ajili ya wafugaji na kadhalika. Ilionekana kana kwamba ilikuwa ni Klondike, napo pakageuka kuwa ni maskani hii. Nilikuwa nimesimama papa hapa. Nilikuwa nikiagiza, mapipa makubwa ya chakula cha kupendeza kuliko vyote nilichowahi kuona. Mafigili, ilivyoonekana, urefu wa futi tatu; na matanipu, na mboga za majani, na viazi, na kila kitu.

32 Akasema, “Weka akiba kubwa sana yake.” Mnaona? Nami nilikuwa nimesimama pale, nikikiweka tu akiba.

33 Ndipo nikaamka. Nisingeweza kuielewa. Nilidhani ilikuwa tu ni ndoto, na nikaendelea. Ilimsumbua Ndugu Wood na wengi wao. Kwa hiyo, hii hapa tafsiri yake. Ilinibidi kungoja, kama vile tu nimewaambia mara nyingi. Mambo yanapaswa kutukia kabla hujaweza; vitu fulani vinavyoliweka kwenye mstari. Hii hapa tafsiri yake. Wao . . .

34 Tulikuwa tukitumainia nchi za ng’ambo. Ndugu Miner Arganbright, rafiki msiri wangu, alikuwa akitaka kulipia matumizi yangu mimi na ya mke wangu, kuitalii Palestina. Nasi tulikuwa twende Uswisi, kisha tuteremke tuingie Afrika, na kwenye uamsho katika Juni. Naye mke wangu, na Rebekah, na hao wengine, hakika walisisimkwa kujua watapata kwenda kupitia Ujerumani, Uingereza, Ufaransa, na Palestina.

Walikuwa wangojee kule mpaka nimalize uamsho wa Afrika, kisha niwachukue njiani nitakapokuwa nikirudi. Nao wote walikuwa wana matarajio makubwa. Mlinisikia nikisema, "Bwana akipenda," sikuzote. "Bwana akipenda, ninakusudia kuupeleka uamsho huo kwenye nchi za ng'ambo. Sijui kabisa bado." Kwa hiyo nilikuwa nikingojea.

35 Lakini mambo yalikuwa hivi. Huyu Bw. Smith, George Smith, huyo alikuwa mkufunzi wangu wa kwanza mle, naye alikuwa amewashinda hata na zaidi hao vijana waliokuwa nchini siku hizi, katika mapigano yake. Ilikuwa ni mafunzo yangu ya kwanza, katika mstari wa maombi. Mnaona?

36 Mara nyingi, mimi huwaleta watu huku juu, kuna maono. Nangojea. Naam. *Huyu*, ono. *Yule*, ono. Kamwe halikutenda kazi vizuri tu. Sasa, nilipoanza kwa mara ya kwanza, kamwe sikumruhusu mtu. . . Isipokuwa nikute kitu fulani mstarini, ambacho hakikuwa ni sawa kabisa, na Yeye akanisimamisha, Mwenyewe, mnaona, na kuniambia habari zake, ningeendelea na kuwaombea watu. Na, jamani, ma—matokeo yalikuwa ni mara mia moja, maana nilipata kuninii. . . Ningewaombea mia nne ama mia tano usiku mmoja. Kwa njia hii, labda ishirini na watano ama thelathini, labda sio wengi hivyo. Labda maono kumi ama kumi na matano, nami ni. . . iliwabidi kunibeba mkanipeleka nje, karibu hivyo.

37 Kurudi kwenye jambo lilo hilo tena, mnaona, kurudi kwenye mafunzo yangu ya kwanza. Hata hivyo, hakuna kitu hudumani kilichopata kulistahimili, au kinachoweza, mnaona, maana ni Neno. Si dhehebu fulani. Ni Neno. Mnaona?

38 Halafu basi, pale, ndipo mnaona sehemu inayofuata baada ya hayo, Meda aliondoka kwenye hiyo ndoto. Nilipofika baharini, hiyo ilikuwa: kwenda katika nchi za ng'ambo.

39 Sasa, Ndugu Arganbright aliniita, hivi majuzi usiku, amesisimkwa sana, na kusema, "Ndugu Branham, itakuwa ni likizo moja kubwa. Ndugu Shakarian amekuwa na mshtuko wa moyo, kwa hiyo ile mikutano ya nchi za ng'ambo imefutiliwa mbali." Na wao. . . Ule mkutano wa Uswisi, yeye alitaka niende huko kwa ajili ya usiku mmoja tu, nami nilikuwa niwe na mkutano huo mmoja wa usiku. Ndipo hizo zingine zote zilikuwa ziwe ni likizo, matembezi tu kote nchini. Loo, hilo, sasa, ambalo ni zuri sana; Ndugu Arganbright ni kipeo, cha Mkristo, rafiki msiri wangu na wa familia yangu.

40 Na, lakini, mnaona, ule mtumbwi mdogo mweupe wa plastiki, aliotaka niabiri, ulikuwa ni Neno la Mungu. Na hakuna mahubiri ya kutosha ndani yake, kuniita kwenda nchi za ng'ambo. Nikasema, "A-ha, sio huo. Kwa ajili ya huo tu? Aa-ha."

Akasema, "Basi nenda, nenda pamoja nao, kama waendavyo."

41 Nikasema, “Hao si mabaharia, wahubiri. Mimi ni mhudumu. Kama wangalienda, ingekuwa ni likizo, kwa jumla, pamoja na kamba za kupiga kambi ndani yake.” Bali nisingefanya hivyo. Nikalikataa. Kwa hiyo hiyo hapo tafsiri ya—ya hiyo ndoto. Mnaona?

42 Na halafu Bw. Arganbright akaniita, siku chache zilizopita usiku, na kuniambia kwamba—kwamba ile—ile . . . Hakika, tulisikia ya kwamba mikutano ya nchi za ng’ambo ilikuwa imefutiliwa mbali, kwa sababu ya Ndugu Shakarian. Halafu basi hakuna . . . Ule, ule wa Uswisi, nilikuwa tu na usiku mmoja. Nami . . .

43 Ilibidi Meda aniambie, kwanza, kwamba hakutaka kwenda. Kwa hiyo nikampigia simu, kutoka Florida, hivi majuzi usiku, ama Georgia, nami nikamwambia. Nikasema, “Ndugu Arganbright amepiga simu na kusema inatupasa kuondoka tarehe ishirini Mei.”

44 Akasema, “Hiyo haiwezekani. Hiyo haiwezekani.” Mnaona? “Watoto watakuwa ndio wanafanya mtihani wakati huo. Siwezi kwenda.” Mnaona, ilibidi aukatae, yeye mwenyewe, maana yeye ndiye aliyehusishwa. Ilikuwa ni likizo yake. Basi hiyo hapo.

45 Hata ndoto, kila kitu, zina maana yake. Kila kitu kina kitu fulani mahali fulani. Kwa hiyo, ndoto zina tafsiri zake.

46 Sasa, nikirudi . . . Huenda nikasema hivyo mpate kuelewa, na haya yanarekodiwa. Nikiwa njiani, kuja nyumbani . . .

47 Kabla tu sijaenda huko nje, ni wangapi wanaonikumbuka nikilirudia hapa, ya kwamba Sauti ilinijia, chumbani asubuhi moja baada ya ono, na kusema kuhusu, ikanena juu ya yule nyoka, naye akifungwa, na nisiogope chochote? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Yeye alisema, “Usiogope.” Kasema, “Hivi sijathibitisha kuwa pamoja nawe popote uendapo?” Kasema, “Hivi sijathibitisha kuwa pamoja nawe kwenye ziara zako za mawindoni?” Mnakumbuka wakati nilipowaambia kile nilikuwa nitapata, kabla ya kuondoka, na yote hayo? [“Amina.”] Mnaona? Kasema, “Hivi sijathibitisha kuwa pamoja nawe?” Ndipo Sauti tamu kwelikweli ikaja, kasema, “Uwepo usioshindwa wa Yesu Kristo upo pamoja nawe popote uendapo.” Nami najua, kwa jambo hilo, tunasongea kwenye kitu fulani. Sijui ni kitu gani. Siwezi kusema.

48 Nikija nyumbani, hivi majuzi usiku, ama hivi majuzi mchana, ama kabla tu sijaja nyumbani, niliingia kwenye ono. Nami nikawaona jamaa wadogo, wembamba, walionekana kama wavulana wadogo, ama kitu fulani, walikuwa wamevaa chepeo. Nasi tulikuwa tumesimama, tukiwinda. Nami nilikuwa nimempiga risasi dubu mkubwa mno wa hudhurungi. Nao wakageuka na kuniambia, kasema, “Lakini kuna utata fulani kuhusu ule mkutano.”

49 Nikasema, "Haidhuru ni utata gani, kama ninapaswa kwenda, popote pale, nitaenda kwa vyovyote vile, mnaona. Haijalishi." Ndipo hilo ono likakoma. Sijui huko ni wapi. Lakini, hili liko kwenye kanda. Litatukia. Mnaona? Kumbukeni tu, litatukia. Ni ono.

50 Kwa hiyo, sasa, Jumapili ijayo, nitakuwa Tennessee, Bwana akipenda, Jumamosi ijayo usiku na Jumapili, pamoja na Ndugu M. E. Littlefield, kwenye, loo, yale makao makuu ya church of God huko Cleveland, Tennessee. Ndugu M. E. Littlefield, kwenye kanisa lake, lile nililoliweka wakfu kwa ajili yake hapa, miaka miwili ama mitatu iliyopita, huko Cleveland, Tennessee, Jumamosi ijayo usiku na Jumapili asubuhi. Itakuwa tu ni ibada ya Jumapili asubuhi pekee, Jumapili. Nayo inipe wakati, familia yangu iende pamoja nami, kisha tutarudi. Nilimwahidi, kuja na kuhubiri tena katika kanisa lake. Hiyo ni Jumapili ijayo.

51 Halafu, Jumapili ifuatayo, Ndugu Arganbright atakuwa hapa pamoja na Ndugu Rowe, yule mwanadiplomasia wa Washington, ambaye amekuwa, ametumika chini ya marais watatu au wanne. Wanapaswa kuwa hapa kwenye Jumapili hiyo, na wakiwa na sinema mpya. Ninataka kila mtu ajaribu kuwa hapa, ikiwezekana, kwa ajili ya wakati huo. Ninataka kuwa hapa, mimi mwenyewe.

52 Jumapili ifuatayo ni Pasaka. Tunatarajia mkutano mkubwa hapa, Pasaka. Bwana akipenda, nataka kuwa hapa Jumapili ya Pasaka. Kwa kuwa . . . Nasi tuna ibada ya kuchomoza kwa jua, kama kawaida. Ubatizo, nyinyi nyote mtakaobatizwa, Jina la Bwana wetu Yesu, mwe hapa kwa ajili ya Jumapili. Nao umetarajiwa, ama kunenwa, muda mfupi uliopita, kwa kuwa hatuna nafasi ya kuketi, huenda tukachukua ule wa Klabu ya Vijana, kunaketi watu mia saba ama nane, juu ya hapa tu, karibu sana na hapa, klabu mpya huku pembeni, turudi hapa kwa ajili ya ibada ya ubatizo basi. Kisha turudi kule juu, kusudi kila mtu aweze kuwa na kiti cha starehe kwa ajili ya asubuhi ya Pasaka. Tutajaribu kuangalia hilo, juma hili, tupate kujua.

53 Halafu ibada itakayofuata, kuanzia wakati huo na kuendelea . . . Ninaondoka hapa tarehe ishirini na . . . ishirini na tano ama ishirini na sita ya mwezi huu. Na tarehe saba . . . sita, saba, nane, na tisa, na kumi, niko huko mbali nyuma kwenye . . . kutoka Van- . . . ama Kisiwa cha Victoria, huko nyuma kabisa miongoni mwa Wahindi fulani, ambako inakubidi kwenda kwa mtumbwi, kuwafikia.

54 Maskini rafiki yangu mmishenari, ndugu, nilikuwa pamoja naye kwenye msimu wa kupukutika uliopita kwenye ziara ya kuwinda. Na kutoka kwenye nyumba nzuri, yeye pamoja na mke wake. Na mikono yake, kila kitu, ni kibichi, mahali mbalimbali. Vema, hivyo ndivyo hiyo ilivyokuwa. Ilitokana na viroboto, kunguni na kadhalika, mnaona, waliokuwa nao

wakiishi huko nje, ambako iliwabidi tu kuishi katika chochote kile, miongoni mwa hao Wahindi. Alikuwa ameleta baadhi yao kwenye mkutano, yule chifu. Wote ni Wakatoliki, karibu wote. Naye Roho Mtakatifu akashuka kupitia kule na kumchukua chifu huyo, na hao wote waliokuwa pamoja naye, na kumponya kila mmoja wao papo hapo mkutanoni. Wao kwa urahisi waliunguza kabisa pwani hiyo, huku na huku, na mitumbwi yao ikitoka. Wao ni wavuvi weledi, huku na huku katika pwani. Naye Ndugu Eddie anaita, nami nina hisi ndogo ya kwenda, mnaona, kwenda kule.

55 Halafu tunaondoka hapo, na tuna safari ya siku moja kutoka huko, na kuwa na siku mbili usiku ama siku tatu usiku katika Fort St. John. Hiyo ni huko juu kabisa kwenye barabara kuu ya Alaska. Na siku mbili usiku kule.

56 Kisha, nikija nyumbani, na ninii. . .Nafikiri ni tarehe saba, nane, tisa na kumi Juni. Sasa, hapa ni mahali ambapo nyote mngeweza kwenda, kwenye mikutano hii hapa, itakuwa Pines ya Kusini. Mnamjua yule ndugu aliyeandika makala mazuri sana hapa, sio muda mrefu uliopita. Jambo lingine, yeye alinitumia magazeti mengine. Nilipaswa kuyaleta. Nitakuwa nayo hapa Jumapili ijayo, Bwana akipenda. Na hiyo ni huko Pines ya Kusini, karibu tu, loo, mwendo wa saa sita au nane kuendesha gari kutoka hapa, Pines ya Kusini, Carolina ya Kaskazini. Ama, hiyo ni Carolina ya Kusini? Carolina ya Kaskazini. Naam. Hiyo ni kweli. Halafu, naam, ndipo tutaondoka kule tarehe kumi.

57 Halafu kwenye tarehe kumi na moja na kumi na mbili, pamoja na Ndugu Bigby huko Columbia, Carolina ya Kusini. Naye huyo ndiye yule mtu, Mpresbiteri aliyeandika yale makala. Kwangu mimi, yalinipendeza vizuri kuliko lolote walilopata kuandika kunihusu mimi. Yeye alikuwa ni Mpresbiteri, daktari wa uungu. Naye akaja Chicago na kuandika hayo makala. Juu ya. . .Ninasahau yalikuwa ni nini sasa. Yalikuwa mazuri sana. Ninayo mahali fulani, na gazetini. Jambo fulani kuhusu "Mpresbiteri, akikutana kwenye Pentekoste," ama kitu kama hicho, "nabii mpentekoste kwa Mpresbiteri," kitu fulani. Basi tutakuwa pamoja naye.

58 Halafu, jana usiku, tulimpigia simu Ndugu Roy Borders, ambaye tayari yuko kwenye Pwani ya Magharibi. Na kuna baadhi ya watu huko nje walio na kadiri ya makanisa thelathini na tano na arobaini kushirikiana mikutanoni; Sedalia, California; na huko Grass City, na kutoka hapo. . .ama Grass Valley, hasa. Na kutoka hapo, twende Oregon; hata huko—huko Washington.

59 Na kisha Ndugu Arganbright, akija, tunaenda, tunapanga sasa, katika juma la mwisho la Julai, kuwa huko Anchorage, Alaska, kuandaa tawi pale kwa ajili ya Wafanyabiashara Wakristo, kufuatia siku sita ama nane za uamsho ambazo

ninatumaini kuwa nao, huko Alaska kugumu, kunakoparuza. Mwajua jinsi ilivyo, watafutaji tu na wachimba madini. Na sahani moja ya hemu na mayai inagharimu yapata dola tatu na senti hamsini. Ni—ni mahali pagumu kweli, bali wanahitaji Injili.

60 Sasa, ninalokusudia kufanya, ni, mambo haya ninayofundisha juu yake hapa, kuweka akiba Chakula hiki na kukisambaza, ninataka kwenda sasa. Sina uongozi dhahiri wa mahali popote, bali ninaenda, nikipanda mbegu, kutumwa mahali fulani, nilianza.

61 Mke wangu, yuko hapa mahali fulani. Alipata barua kutoka kwa mama fulani hapa Illinois hivi majuzi. Iliichoma tu penye nafsi ya moyo wangu. Mama huyu alisema, "Dada Branham," kasema, "hapana shaka ila ambavyo mara nyingi, na kotekote, tangu ulipoolewa, kwamba imekubidi kuteseka sana, Ndugu Branham akiwa ameondoka, ukiwa na watoto hao." Kisha kasema, "Hao watoto, hakika, wanamlilia baba yao na kadhalika." Kisha kasema, "Najua unayomaanisha, kwa sababu nina mume mzuri sana, mimi mwenyewe." Akasema, "Lakini, nitakwambia hali yangu."

62 Akasema, "Ni—nimekuwa na upasuaji mkubwa mara nne, hii miaka minne iliyopita." Akasema, "Ninakunywa karibu, dawa kumi na tano ama kumi na sita za kutuliza maumivu kwa siku." Kisha kasema, "Ninadungwa sindano tatu za Leksironi, na kadhalika, kwa juma." Kisha kasema, "Ninameza lundo la tembe za kulala, na kitu cha hivi karibuni sana, na kutuliza mishipa. Na hizo sindano, nami nameza kadiri ya tembe mbili, tembe maradufu za kulala usiku, wala siwezi kulala." Kisha akasema, "Daktari wangu ameniambia niende kwenye hospitali ya wendawazimu kabla sijafikia nisipoweza kurudi. Huenda kukawa na tumaini kwamba ninaweza kuiokoa akili yangu." Naye akasema, "Wala hakuna kitu katika taaluma ya tiba popote kingaliweza kunisaidia."

63 Kisha akasema, "Nilikuwa nikidhamiria kujiua, nikipanga, kumwacha mume wangu mpendwa na msichana wangu mdogo." Akasema, "Tunaishi Kansas. Ninapapenda, kwa sababu ninaona nafaka ikikomaa, na kuwazia mavuno."

64 Nafikiri alikuwa Mmethodisti. Kisha akasema ambapo... Halafu basi, huko kwenye chuo cha Methodisti katika Bloomington, Illinois, walichukua gazeti, kwamba ningekuwa kule, miezi kumi na mmoja iliyopita. Wengi wenu mnaukumbuka mkutano wa Bloomington. Mlikuwa kule.

65 Naye akasema, "Mume wangu alinichukua, pamoja na marafiki kadhaa, na kuondoka." Kisha kasema, "Bwana alijua nisingeweza kuvumilia hayo siku moja zaidi." Alikuwa amedhoofika sana. Ndipo akasema, "Nilikuwa ndiye mtu wa kwanza. Mwanao, Billy Paul, akanipa kadi. Basi usiku

huo, hapo mume wa—wako alipoziita zile namba, nilikuwa wa kwanza mstarini, kuombewa." Kisha kasema, "Mara nilipokuja jukwaani," kasema, "yeye aliniambia maisha yangu na akaniambia yale niliyofanya, na yote kuhusu hilo, na kusema, 'BWANA ASEMA HIVI, imekwisha.'" Kasema, "Dakika iyo hiyo, sijawahi kuwa na uchungu mwingine." Kasema, "Nilikuwa na uzito wa pauni sabini na kitu. Nina uzito wa pauni mia moja na sitini na kitu sasa." Kisha kasema, "Dada Branham, unapokuwa mpweke," kasema, "ninajua jinsi unavyojisikia, ukigawana mume wako na ulimwengu, na vitu kama hivyo. Lakini," kasema, "kumbuka tu, maskini mke wa nyumbani wa Kansas yuko huru leo hii, kwa kuwa alikuwa radhi kumsikiliza Bwana."

66 Nilimwonyesha Billy. Nikasema, "Billy, ninataka uitume hii kwenye chuo kile cha Methodisti."

Akanyosha mkono na kuchukua lundo, kasema, "Soma baadhi ya hizi."

67 Nikasema, "Najua. Najua ni nzuri sana, lakini hii moja imetosha. Hii imeandaa tu mahali."

68 Mliusikia huo? "'Mchafu! Mchafu!' Pepo wabaya walimsukuma," mnaona, moja kwa moja akaingia wazimu, "huko makaburini. Wakati Yesu alipokuja, Yeye aliwaweka huru mateka." Naye Yesu ni Neno. Kwa hiyo, lichukue Neno, nalo litamweka mateka huru.

69 Mimi hapa ninazungumza, nikichukua muda wangu, nikichukua muda wenu, na mengi sana ya kusema.

Na tuviinamishe vichwa vyetu.

70 Bwana, kama wapatikanao na mauti, tunajua hatuna wakati mwingi sana uliosalia wa kuzungumza. Ninapoangalia juu ya maskini wasafiri hawa wenye njaa ya moyo waliotoka makondeni, kutoka kulima, baadhi yao wamekuja kutoka kwenye kazi za umma, kutoka kazini, na baadhi yao waliendesha motokaa kupitia milimani, jangwani, na makondeni na vinamasi, na kukutanika hapa, kisha inawabidi kusimama. Lakini wao ni wasafiri. Si wa ulimwengu huu. Wao wapo hapa tu kama shuhuda, kama taa zilizowekwa juu ya kilima, zinazotoa Nuru kwenye jamii mahali wanakoishi. Ndipo wanapokuja pamoja, kuwekwa wakfu tena, na kuchajiwa kwa Neno, wao wanasimama, wanashikwa na mkakamao wa viungo vyao, na wa—wazee kwa vijana, sawia.

71 Wanakupenda Wewe, Bwana. Hiyo ndiyo sababu wapo hapa. Mtu yeyote anajua ya kwamba mtu asingeweza kuja, na kuendesha gari kwa maili kadhaa, na kusimama ukutani, na kuegemea, na miguu ina mkakamao, apate tu kuonekana. Na pamoja na kundi hili, Bwana, sisi—sisi ni watu maskini. Hatuji kwa mavazi maridadi. Tunakuja hapa kukuabudu Wewe.

Kusudi moja moyoni mwetu, lengo moja na kusudi moja, hilo ni Wewe, Bwana.

72 Ninaomba, Mungu, kwamba Wewe utawapa thawabu. Jalia pasiwepo na mtu mmoja atakayepitia kwenye milango hii, leo hii, bali yule atakayepata Uzima wa Milele. "Ndipo taabu za barabarani zitaonekana kama si kitu, tutakapofikia mwisho wa safari." Endapo wao ni wagonjwa, waponye, Bwana.

73 Na sasa ndio kwanza tuzungumze juu ya mikutano mingine, ama pasipo kujua kwa dhahiri, basi nitaenda, yakiwa ni mapenzi Yako, nikizisambaza tu Mbegu. Zitachipuka, kama zikianguka kwenye udongo mzuri. Ninaomba, Bwana, kwamba utaziongoza kwenye udongo huo mzuri.

74 Huku zimewekwa jukwaani, ama mimbarani, nilipaswa kusema, hapa asubuhi ya leo, pana leso, vifurushi vidogo. Inamaanisha kwamba watu ni wagonjwa, wahitaji. Ee Mungu wa Mbinguni, aliyemfufua Kristo kutoka kwa wafu na amemtoa kwetu katika siku hii ya mwisho, katika umbo la Roho Mtakatifu, jalia Yeye Yule aliyeko kila mahali aangalie chini; ajuaye yote, anayejua mambo yote; mwenye uweza wote, mwenye nguvu zote. Angalia maskini vifurushi hivi. Pia vijalie, vitakapowagusa wagonjwa na wanaoteseka, jalia Roho Mtakatifu ayahuishe maombi hayo kwenye masikio ya Mungu, na jalia waponywe mara moja.

75 Bwana, nawazia juu ya maskini mwanamke yule. Ndio kwanza niunukuu ushuhuda wake, "Huko nje Kansas leo hii, mwenye furaha, hamna uchungu. Hakuna daktari anayeweza kupata kasoro yoyote kwake. Hakuna uchungu tena, hakuna dawa za kutuliza tena, hakuna tembe za kulala tena; anapata usingizi mzuri na mzito. Kila kitu ni shwari." Ee Bwana, hakika, wakati Wewe unapokuja, kila kitu ni shwari basi. Tunakushukuru Wewe kwa ajili ya jambo hilo.

76 Sasa, Baba, tunapoligeukia Neno, libariki Neno Lako. Na lisikurudie bure, bali jalia litimize yale limekusudiwa na kuwekewa wakfu. katika Jina la Yesu tunaomba hayo. Amina.

77 Sasa, mnaweza kusikia vizuri, kila mtu? Huko nyuma kabisa, yote ni sawa? Ni upi mzuri zaidi, kama nikizungumza *hivi*, ama nizungumze *hivi*? *Huku*, upande huu hapa ni bora zaidi? Hilo ni afadhali kwenu nyote huko nyuma? Vema, nitakivuta hiki hapa, karibu kidogo tu basi.

78 Jumapili iliyopita, ni juma moja, ni—nilichelewa kidogo, nilikuwa na ibada ndefu sana. Sipendi kuwa hivyo. Na sasa, mara moja moja, halitanisumbua hata kidogo, kama mtu amekaa chini, atawaona wale wanaosimama, angetaka kubadilishana mahali nao, kidogo, kuwapumzisha. Lingekuwa ni tendo zuri sana la Kikristo. Na sasa, sasa, labda, ifikapo—ifikapo Pasaka hii, huenda tukawa na mahali pengine pa kufanyia i—i—ibada kubwa.

79 Sasa tunataka kufungua, asubuhi ya leo. Ninyi askari wote uchukueni Upanga we—wenu sasa, nasi tutatangaza vita juu ya adui. Tulizoea kuimba wimbo mdogo muujuao:

Vita vimepamba moto, Ewe askari Mkristo,
Ana kwa ana katika safu thabiti.

Mmeusikia huo wimbo.

Silaha zinang'aa, bendera zinapepea,
Ukweli na uongo vinashambuliana leo hii.

Mnaona? Hiyo ni kweli.

Vita vimepamba moto, ila msichoke,
Iweni na nguvu na katika nguvu Zake shikilieni kwa uthabiti;
Mungu akiwa upande wetu, bendera Yake juu yetu,
Tutaimba wimbo wa mshindi hatimaye.

80 Hiyo ni kweli. Sasa tunataka kufungua, kwanza, kusoma somo la Maandiko linalopatikana katika Yohana Mtakatifu 10, vifungu vitano vya kwanza.

Amin, amin, nawaambieni, Yeye asiyeingia mlangoni katika zizi la kondoo, lakini akwea penginepo, huyo ni mwivi naye ni mnyang'anyi.

Lakini yeye aingiaye...mlangoni ni mchungaji wa kondoo.

Bawabu humfungulia huyo; na—na kondoo huisikia sauti yake: naye anawaita *kondoo wake kwa majina yao, na kuwapeleka nje.*

Naye awatoapo nje kondoo wake mwenyewe, huwatangulia, na wale kondoo humfuata: kwa maana waijua sauti yake.

...mgeni hawatamfuata kabisa, bali watamkimbia: kwa—kwa maana hawazijui sauti za wageni.

81 Sasa, somo asubuhi ya leo, ambalo nimelichagua kufundisha kidogo, ni: *Hekima Dhidi Ya Imani. Hekima Dhidi Ya Imani.*

82 Sasa, kunavyo vyanzo viwili pekee, ama kwa vyanzo viwili, ambavyo hatuna budi kuishi. Mlijua hivyo? Sasa sisi...

83 Ninayo Maandiko mengi yaliyoandikwa hapa chini. Nami ninawataka...Labda tutayarejea, tunapoendelea. Na—nami nitajaribu kutoka upesi niwezavyo. Wala sitajaribu kuninii... Kulielezea tu, kusudi mpate kulichukua kutoka hapo na kuendelea. Mnaona?

84 Lakini kunazo asili mbili tu tunazoweza kutoa maisha yetu kwake. Na moja ya hizo ni hekima, na hiyo nyingine ni imani. Na laiti tungewazia yale hekima inayotoa, kisha yale imani inayotoa! Lakini, asili hizo mbili, tunarudi nyuma asubuhi ya leo na kuzichukua kwa ajili ya somo la shule ya Jumapili, na

kuzitoa kwenye Biblia; na kuonyesha kwamba ni nini, na yale zitakayofanya, na yale zimefanya, kwa msaada wa Bwana.

85 Sasa, imani na hekima. Sasa, kwanza kabisa, tutaona, kwamba, katika Mwanzo, mlango wa kwanza, tunaona ya kwamba—ya kwamba imani iliwasilishwa, nayo hekima ikawasilishwa. Na, leo hii, asili hizo mbili zingali zinawasilishwa kwa jamii ya binadamu. Tunaona, kwamba, Mungu alikuwa ndiye Mwanzilishi wa imani, kuamini, watu wapate kuliamini na kulitumainia Neno Lake. Naye Shetani ndiye mwanzilishi wa hekima, akijaribu kuwafanya watu waikubali hekima yake, na kuwaondosha kwenye imani iliyo katika Neno la Mungu. Asili hizo mbili.

86 Tunaona ni ajabu sana kwamba Mwanzo, mlango huu wa mbegu, unaanza namna hiyo. Nasi tunaona ya kwamba mambo yote tuliyo nayo, leo hii, asili yake ni katika Mwanzo, maana neno *Mwanzo* linamaanisha "chanzo." Na kama tukiona mambo haya tuliyo, siku hizi, jinsi yalivyo, ilibidi yawe na mwanzo mahali fulani. Itakubidi kufuatilia kila kitu huko nyuma mwanzoni.

87 Basi hili hapa wazo dogo kwa ajili yenu. Kila kitu kilichokuwa na mwanzo, kina mwisho. Lakini ni mambo ambayo hayakuwa na mwanzo, ndiyo hayana mwisho, vitu pekee vilivyo vya Milele.

88 Kwa hiyo, ningetaka kuuliza swali. Kamwe tungewezaje kuleta maana ya neno "uwana wa Milele wa Mungu"? Iwapo Yeye alikuwa ni Mwana, alikuwa na mwanzo. Kama alikuwa ni Mwana wa Milele, angewezaje kuwa Mwana na awe ni wa Milele? Kwa kuwa, *mwana* ni—ni zao la kitu fulani. Lakini, kama Yeye alikuwa—Yeye alikuwa, asingeweza kuwa ni Mwana wa Milele. Hakuna kitu kama hicho, "Mwana wa Milele wa Mungu." Maana, iwapo Yeye—iwapo Yeye kamwe hakuwa na mwanzo, basi hawezi kuwa chochote ila wa Milele. Lakini, iwapo Yeye alikuwa ni Mwana, alikuwa na mwanzo, kwa hiyo Yeye hawezi kuwa ni Mwana wa Milele.

89 Ilikuwa ni Mungu wa Milele aliyedhihirishwa katika Mwana. A-ha. Mnaona? Mungu wa Milele, maana Mungu ndiye kitu pekee kilicho cha Milele.

90 Na njia pekee tunayoweza kuishi kamwe ni kwa sababu tunao Uzima wa Milele. Mwili huu hufa, sehemu zetu zote hufa. Lakini sehemu iliyo ya Milele ni Mungu, wala haiwezi kufa. Sasa, sasa, Neno, Biblia, ni ya Milele, kwa sababu ni Mungu katika umbo la Neno. Na yale yaliyokuwa ndani ya Mungu, katika mawazo Yake, kabla hapajakuwapo na Neno lolote lililonenwa, ilikuwa ni Mungu. Mnaliona? Ilikuwa ni Mungu. Kwa hiyo, tukiwa tumekusudiwa tangu zamani, sisi tulio; tukisema "sisi," nikitumaini niko pamoja nanyi mliokusudiwa

tangu zamani; yalikuwa ni—ni mambo yaliyokuwapo pamoja na Mungu katika Umilele.

91 Halafu basi, kama wewe ni mtoto wa Mungu aliyezaliwa mara ya pili, wewe ni, nawe unaye Roho Mtakatifu ndani yako, wewe ni dhihirisho la Neno la Mungu lililonenwa kabla halijakuwa Neno. Halina budi kuwa wazo kabla halijakuwa Neno. Neno ni wazo lililotamkwa. Nayo mawazo yalikuwa katika Mungu, halafu basi tulikuwa katika Mungu katika Umilele, nasi tulinenwa kwa Neno tukawa. Loo, ni ninii . . . Kwa Neno lipi? Neno *Hili*, Neno la Mungu.

92 Sasa, Mungu ndiye mwanzilishi wa imani. Shetani ndiye mwanzilishi wa hekima. Kwa kuwa, Mungu aliwapa watoto Wake wa kwanza Neno Lake, na kuwaambia hawana budi kuliamini Hili; kisha akaweka mauti, utengano, adhabu, wakikosa kuliamini.

93 Ndipo Shetani anajongea karibu na kujaribu kumpa Hawa, hekima, "Utakuwa na hekima, ukijua mema na mabaya, kama Mungu." Sasa, mnaona, kwanza kabisa, unaona upesi sana ya kwamba hekima hutokana na ibilisi. Hilo ni ajabu, sivyo? Bali ni kweli. Hekima hutoka kwa ibilisi. Yeye ndiye mwanzilishi wa hekima.

94 Sasa, hakika, chochote alicho nacho ibilisi, ni upotovu wa cha asili. Dhambi ni upotovu, upotovu wa haki. Uzinzi ni upotovu wa—wa tendo halali. Uongo ni upotovu wa kweli.

95 Na kwa hiyo he—hekima ninayowataka mwipate vizuri, kabla hatujaanza. Kunayo hekima ya Mungu, hekima ya Mungu, ni, dumu pamoja na Neno Lake. Lakini Shetani, katika hekima yake, alijaribu kuligeuza Neno, kwa hiyo hiyo ndiyo hekima ninayozungumzia.

96 Kuna kiasi fulani cha imani kinachoambatana na Shetani. Kusudi u—umkubali Shetani, huna budi kumwamini Shetani, kwa hiyo kuna imani iliyopotoshwa kwa kitu kilichopotoshwa. Na chochote ambacho kingejaribu kuligeuza Neno la Mungu, kulifanya liseme jambo fulani ambalo halisemi, ni roho mbaya, mnaona, akitoa hekima dhidi ya hekima ya Mungu. Kwa hiyo, tutarejea kwake kama hekima, wala si imani ya Shetani.

97 Wengi wa hao watu wanaoamini hilo, ni waaminifu, na kuamini, kwa imani yote tu uliyo nayo, kwamba wako sahihi. Mnaona? Inakubidi kuangalia. Blanketi huenea pande zote mbili sasa. Lakini, yeye, wao ni . . . Njia pekee ya kuwa na hakika, ni kurudi kwenye Neno la asili. Hapo ndipo kila kitu kimewekewa msingi, juu ya Neno.

98 Sasa, tunaona ya kwamba vikundi hivi viwili vidogo, ama asili, ni: kimoja, hekima; na hicho kingine, imani. Navyo vimepingana tangu uumbaji, katika bustani ya Edeni.

Sasa, kunao watoto pande zote mbili.

99 Sasa, he—hekima tunayonena habari zake ni ipi? Kitu fulani ambacho hakitakubali kwamba Neno hili lote ni Kweli. Ni kitu ambacho kitaondoa kutoka kwenye ile Kweli, kikijielezea kuwa ni maarifa bora zaidi, hekima bora zaidi. Basi ikiwa hekima ya namna hiyo hutokana na Shetani, watoto wake huishi kwa hekima hiyo.

100 Na kama imani ya Mungu ilikuja kupitia kwa Mungu, naye Mungu ni Neno, watoto wa Mungu huishi kwa imani. Biblia ilisema, "Wenye haki wataishi kwa hekima"? [Kusanyiko linasema, "La."—Mh.] Imani! "Wenye haki wataishi kwa imani." Sio yale anayoweza kujifunza, bali yale anayoweza kuamini. Vema.

101 Sasa, sasa tunaona. Hebu tuchukue hekima, kwanza. Hekima ina kutoa hoja. Imani haina kutoa hoja. Bali hekima ina kutoa hoja. Hebu tuanze tu kufungua katika Biblia, na hebu tufungue sasa kwenye Mwanzo, mlango wa 3 katika Mwanzo, na tulifundishe tu hili.

102 Sasa tunafanya nini, tunajaribu kufanya nini asubuhi ya leo? Kuyafuata yale Bwana aliyosema, "Weka Chakula akiba." Mtakihitaji, moja ya siku hizi. "Weka Chakula akiba."

103 Sasa, Mwanzo 3:1, hebu tusome sasa, tuone jinsi hekima ilivyo na kutoa hoja.

> *Basi nyoka alikuwa mwerevu kuliko* wanyama wote *wa mwitu aliowafanya* Bwana *Mungu. Akamwambia mwanamke, Ati hivi ndivyo* amesema *Mungu,* (kuamini, kusema Neno), *Msile matunda ya miti yote ya bustani?*
>
> *Mwanamke akamwambia nyoka, Matunda ya miti ya bustanini twaweza kula:*
>
> *Lakini . . . tunda la mti ulio katikati ya bustani, Mungu amesema, Msile,* (akilinukuu Neno), *wala msiliguse, msije mkafa.*

104 Sasa, imani inashikilia Hilo. Mnaona? Sasa angalieni.

> *. . . nyoka akamwambia mwanamke, Hakika hamtakufa:*

105 Hoja, kutoa hoja, "Mungu ni mzuri sana. Mungu ana rehema nyingi sana. Yeye anawapenda sana." Unamsikia ibilisi yuyo huyo wa kale siku hizi. "Mungu ni mzuri kupita kiasi kufanya *hili*. Mungu hatafanya *hili*. Mungu hataadhibu." Yeye atafanya yale hasa Neno Lake liliyosema atafanya. Mnaona?

106 "Hakika hamtakufa." Mnaona? Yeye anajaribu kufanya nini? Kumfanya ahojiane naye. Katika dakika moja hiyo unapolihoji Neno la Mungu, basi unapoteza imani. Unaona? Usiwe na "ndiyo, la, huenda ikawa." Dumu moja kwa moja na Hilo. Unaona? Hawa alikuwa na mtazamo mzuri, bali alisikiliza hoja zake.

107 Kunao tu watu wengi sana siku hizi ambao wanayo maarifa mazuri, wanaojua ya kwamba Neno hili linapaswa kuwa ni Neno la Mungu, Nalo ni Neno la Mungu, bali wanasimama na kuacha mwanafunzi fulani wa seminari atoe hoja awaondoe Kwake, kutoka kwa Roho Mtakatifu, kutoka kwa mambo ya Mungu. "Kutoa hoja, inatupasa kuzitupa chini."

108 Sasa, kifungu cha 4.

> *Kwa maana . . .*

Nitawaambia ni kwa nini Shetani alisema. Nitasoma kifungu cha 4, kwanza, kisha cha 5.

> *Nyoka akamwambia mwanamke, Hakika hamtakufa—hamtakufa:*
>
> *Kwa maana Mungu* yuajua *ya kwamba* zile siku *mtakapokula tunda la mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama miungu, mkijua mema* kutoka kwa *mabaya.*

109 Mnaona, yeye anampa hoja, "Hivi mngetaka kuwa sawa na Mungu? Kuleni . . . " Kwa maneno mengine, "Mnataka kweli kuwa sawa na Mungu? Shikeni shauri langu. Nisikilizeni. Mungu hamaanishi Hilo. Kamwe hakulimaanisha."

110 Unaposikia hilo, liondokee. Hiyo ni kweli. Huo ni mlio wa nyoka. Linasikika la maana. Bali usitoe hoja, hata kidogo. Liamini tu, lile Mungu alilosema. Sasa, wakati ninii . . .

> *Mwanamke alipoona ya kuwa ule mti wafaa kwa chakula, . . .*

111 Mnaona ilivyokuwa? Hoja zake zilimfanya kujua ilikuwa ni sawa, ilikuwa ni kweli.

> *. . . na kwamba ulikuwa unapendeza* jicho, *nao ni mti wa kutamanika . . .*

112 "Kumfanya mtu awe na imani"? [Kusanyiko linasema, "La."—Mh.]

> . . . kumfanya mtu awe na maarifa, *kumfanya awe na hekima, . . .*

113 Mnaona ilikuwa ni kitu gani? Shetani akitoa maarifa, maarifa yaliyokuwa kinyume na Neno, "wa kumfanya mtu awe na hekima."

> *. . . alitwaa katika tunda . . . akala, akampa* na *mumewe; naye akala.*
>
> *Wakafumbuliwa macho* yao *wote wawili wakajua wa uchi; wakashona majani ya mtini, wakajifanyia nguo.*

114 Sasa, ni kitu gani kilicholianzisha? Kutoa hoja. Mnaona? Imani haina hoja. Hutoi hoja, hata kidogo. Unaamini. Unapoombewa, na kulikubali Neno la Mungu kwa ajili ya uponyaji, usitoe hoja na hisia zako. Usitoe hoja na chochote

kingine. Hakuna kutoa hoja kwake. Mungu alisema hivyo, na hilo latosha.

115 Loo, jinsi ningetaka kusimama hapa kwa dakika chache, na kutulia kwenye hilo, nitoe somo kutoka kwake. Siwezi kufanya hilo, na kuyahubiri haya, yapata mafungu arobaini ama hamsini niliyoandika hapa. Lakini kutoa hoja . . .

116 Bwana anapotoa ono . . . Nitawaambia tu, njia yangu mwenyewe ya kitoto. Bwana anapotoa ono la jambo fulani litakalotukia, mbona, sijali ni kitu gani kilicho kinyume chake.

117 Pia kumbukeni, kila kitu kinachoweza kuelezewa, kinyume, Shetani atakielezea. Atajaribu kutoa hoja, "Huwezi kufanya hivyo."

118 Kwa mfano, hilo ambalo ndio kwanza nilinukuu dakika chache zilizopita, kuhusu kwenda . . . Sasa, hili kidogo lilikuwa nje ya njia tuliyozoea. Kabla tu mama yangu hajatuacha. Naye Bwana alijua nisingeweza kutimiza miadi hiyo na ndugu hao, kuhusu kwenda kuwinda. Basi alinipa ono, na kunituma huko mbali katika British Columbia.

119 Ndipo tulipofika kule, yule kiongozi akasema, "Kamwe sijapata kumwona dubu mwenye ncha za fedha. Nimeishi hapa maisha yangu yote. Mbali na hayo, tunaelekea moja kwa moja katika maeneo ya kondoo, juu ya farasi. Hakuna wenye ncha za fedha. Hakuna . . . Hutampata kule juu." Mnaona? Mnaona? Kujaribu, mnaona, kujaribu kuondoka; hoja.

120 Shetani akaniambia, "Itakuwa, wewe ulininii tu—ulielewa tu hilo ono vibaya."

121 "Ila sikulielewa vibaya. Itakuwa hivyo. BWANA ASEMA HIVI." Ndipo yule kuro alipojitokeza, nasi tukampata huyo, ambaye alikuwa kwenye lile ono, kama mjuavyo nyote.

122 Ndipo akasema, yule kiongozi akaniambia; ndugu mzuri sana, nitakuwa pamoja naye sasa katika majuma machache, Mkristo mchanga. Akasema, "Ndugu Branham, ndugu yangu alikuwa na kifafa. Nawe ukampanda farasi huyo siku hiyo, kisha ukaniambia jambo la kufanya, nacho 'kifafa cha ndugu yangu kitakwisha.'" Akasema, "Nilipofanya kile hasa Roho Mtakatifu alichokwambia uniambie," kasema, "kamwe hajashikwa na kifafa, tangu siku hiyo."

123 Akasema, "Sasa sisi hapa, juu ya mlima huu. Na kwa maili tatu kutelemka hadi chini, hapana hata kichaka chenye urefu wa inchi nne. Hakuna kitu ila kuvumwani ya kuro, miforosadi michache ya samawati, nayo hufikia urefu wa inchi mbili ama tatu tu." Akasema, "Kuvumwani ya kuro na forosadi za samawati, moja kwa moja hata kwenye mwisho wa msitu, nao farasi wetu walikuwa wamefungiwa kwenye mpaka wa msitu. Na sasa, kulingana na yale uliyoniambia kabla hatujakuja hapa, kwamba, mahali fulani kati ya hapa na mahali mvulana yule

anaposimama, aliyevaa lile shati la mirabamiraba, utamwua dubu mkali mwenye ncha za fedha aliye na urefu wa futi tisa."

Nikasema, "Hayo ni BWANA ASEMA HIVI." Mnaona?

Ilikuwa ni kitu gani? Shetani akijaribu kunifanya nisiamini hilo.

124 Tukaanza kushuka mlimani. Kadiri tulivyokaribia, yeye aliendelea kusema, "Ndugu Branham, tuko tu yapata maili moja kutoka kwake sasa."

Nikasema, "Kwani unatilia shaka, Bud?"

"Hata kidogo."

125 Tukafika yapata nusu maili. Kasema, "Tuko nusu maili tu sasa."

126 Nikasema, "Hiyo ni kweli." Kasema, "Wazia tu, katika nusu maili!" Kutupa chini hoja.

127 Yeye akasema, "Angalia. Tunaweza kuona kila kitu moja kwa moja mbele zetu. Hakuna kitu kote huko."

128 "Lakini," nikasema, "Mungu yule aliyenipa hilo Neno anaweza kumwumba mmoja pale. Usitoe hoja. Amini tu. Usivutiwe na hoja zozote. Hilo halina uhusiano wowote nalo. Amini tu alilosema Yeye. Hivyo tu."

129 Nilikuwa nimesimama pale, nikaangalia juu vilimani, kila mahali, kuvumwani manjano za kuro tu; jua likishuka; vilima, vinavyopendeza. Ungeweza kuona doa lolote dogo mahali popote, kwa maili tatu mlimani, moja kwa moja juu yangu. Ndipo nilipogeuka kuangalia, yapata maili mbili mbele yangu, ama maili moja na nusu, ama maili mbili, alisimama dubu mkali mwenye ncha za fedha aliye na urefu wa futi tisa. Jinsi alivyofika pale, sijui mimi. Lakini alikuwa yupo pale. Mnaona?

130 Usitoe hoja. Amini. Haidhuru hali ya mambo ikoje, usijali hali ya mambo. Amini.

Sasa Mungu alisema, "Si—siku utakapokula tunda lake, siku hiyo utakufa."

131 Shetani akasema, "Hebu nikwambie jambo fulani, unaona. Sasa, Hilo, hilo ni . . . Loo, naam, tunasema ya kwamba Mungu ni wa kweli. Hakika. Hiyo ni kweli. Tunaliamini Neno hilo. Loo," Shetani alisema, "Ninaamini Hilo, hakika kabisa. Lakini, sikiliza, hebu nikwambie, Yeye hakumaanisha Hilo hasa."

Kweli alimaanisha Hilo. Alimaanisha yale tu Yeye aliyosema.

132 Shetani akasema, "Sasa, angalia, nitakwambia ni kwa nini alifanya hivyo. Yeye kweli . . . Unaona, wewe—wewe—wewe huna hekima, bado. Huna hekima yoyote. Unaona? Wewe ni kama kondoo tu, wa kuongozwa. Wewe si mali yako." Hivyo ndivyo Mungu anavyokutaka. "Kamwe hujawahi . . . Huna Ph.D., bado. Hu—hu—huna elimu ya kutosha. Unaona? Lakini mimi nina

hekima. Nitakuthibitishia. Sasa, angalia, wewe hujui mema na mabaya. Unajua kuna kitu kama hicho, bali hujui ni kitu gani. Hebu nikuonyeshe jinsi linavyofanywa." Hivyo tu ndivyo alivyotaka kumwambia mwanamke huyo. Hivyo tu ndivyo alivyotaka kufanya. "Hebu nikuonyeshe jinsi linavyofanywa."

Akasema, "Lakini tutakufa."

133 Akasema, "Hakika Mungu hatafanya hivyo. Lakini Yeye anajua ya kwamba mtakuwa na hekima pia." Unaona?

134 Akiweka hekima yake dhidi ya Neno la Mungu. Hiyo hapo hekima ninayonena habari zake. Mnaona? Hekima dhidi ya imani, dhidi ya imani. Hivyo hapo vita vya kwanza. Nalo Neno la Mungu likashikilia imara na kweli. Wakati walipokula lile lililokatazwa, walikufa; nao wamekufa, tangu wakati huo. Mnaona? Hapo ndipo, ilithibitika papo hapo, pasipo na shaka hata kidogo.

135 Sasa tutaliendeleza kwa kitambo kidogo. Sasa, nilikuwa na Mwanzo 3:1, 17, na sasa. . .ama 1 hadi 7, hasa, na sasa, sasa, ambapo hekima ina hoja. Wangapi wanaamini hilo sasa? Semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mnaona? Mnasema sasa . . .

136 Madaktari wanasema, "Vema, nitakwambia." Sasa angalia, hebu mchukue maskini mwanamke huyu ambaye ndio kwanza nitoe ushuhuda wake. Daktari anasema, "Hakuna unachoweza kufanya. Umekwisha tayari. Hakuna matumaini kwako. Nenda kwenye hospitali ya wendawazimu. Mpelekeni huko."

137 Yeye akasema, "Kabla sijaenda huko kwenye moja ya vizimba hivyo, nitajiua."

138 Halafu nini? Mungu akajitokeza jukwaani. Na kupitia kwa tangazo lake, mahali fulani kwenye gazeti huko mbali Kansas, kutoka Bloomington, Illinois, yeye alisikia. "Imani chanzo chake ni kusikia." Mnaona? Vema, mumewe akamwandaa. Walikuwa wanapendana kwelikweli, mmoja kwa mwingine.

139 Wazieni. Miaka minne, na kupasuliwa kukubwa mara nne; vitulizaji kumi na vitano, kumi na sita. Hivyo vinatosha kumwua mwanadamu. Unaona? Na sindano hizo zote, mara mbili ama tatu kwa juma. Nami ninajua moja ya hizo ilikuwa ni Leksironi, nami ninasahau hiyo nyingine ilikuwa ni gani. Ilikuwa ni kitu fulani kwa ajili ya ugonjwa wa akili. Alikuwa akidungwa sindano hizi, na, isitoshe, tembe mbili za kulala. Wala hata asingeweza kulala, kwa hizo. Taabu, mgonjwa siku nzima, usiku kucha, mwaka baada ya mwaka. Hakuna kitu kingaliweza kufanywa.

Lakini, "Imani chanzo chake ni kusikia." Mnaona?

140 Sasa, alipofika kule, Mungu alimweka jukwaani, wa kwanza. Mnaona? Na katika kile. . .Mbona, kitu gani? Nilipomwendea, nami nikasema, "U hali gani, dada?" "U hali

gani?" Kamwe hakusikia lolote kuhusu hili. Hajui lolote juu yake. Lakini kasema, "Wewe ni Bibi *Fulani-wa-fulani*. Unatoka Kansas."

141 Sasa, upesi, hilo linamfanya ku—kuwazia. "Ngoja kidogo. Ndio kwanza nimsikie akisema, kwamba, 'Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Na hapa tulithibitisha, katika Biblia, usiku wa leo, kwamba Kristo aliahidi kuonekana katika siku za mwisho, Kanisani Mwake, nayo mambo waliyofanya huko Sodoma, na kadhalika,' aliyohubiri juu yake." Ambayo ndiyo mahubiri yangu ya ufunguzi. "Kwa kuwa, sasa, hapa ninaliona likiendelea, papa hapa." Unaona? "Sasa, naam."

142 "Sasa, umekuwa kwa madaktari wengi. Umefanyiwa upasuaji mara nne."

143 "Yeye anapata wapi habari hizo? Hizo zinatoka wapi? Maskini mtu huyo mdogo mwenye upara, hajui hayo. Yanatoka wapi?"

"Na ulipokuwa njiani kuja huku, jambo *fulani na fulani*."

144 "Aisee!" Mnaona? "Sasa, hayo ndiyo yale hasa ndio kwanza amalizie kuhubiri. Hilo ni Neno."

145 Lakini, mwajua, Shetani alisema, "Unajua, ukikubali hilo, mchungaji wako. . . " Hilo halina uhusiano wowote nalo. Unaona? Tupilia mbali kutoa hoja. Unaona? "Lakini daktari wako alisema huna budi kwenda kwenye hospitali ya wendawazimu." Tupilia mbali kuhojiana.

146 "Ninangojea nione yale Mungu atakayosema kulihusu." Unaona? Ndipo Mungu. . .Sikujua la kusema. Ndipo Roho akalichukua na kulilipua.

147 Akaliamini. Kamwe hakutoa hoja, "Mwaka baada ya mwaka, baada ya mwaka, kushikwa na fadhaa, kuharibikiwa na akili, upasuaji na kadhalika, mambo haya yote; mbona, hayana busara, nafikiri ningeweza kuponywa hapa, katika sekunde moja." Bali hakuwazia juu ya kutoa hoja. Aliamini tu. Imani ilifanya hilo, naye akaponywa, dakika hiyo.

148 Mkitaka kumwandikia, mbona, Billy anaweza kuwapa anwani yake. Vema, sasa. Sasa, i-. . .

149 Hekima itatoa hoja. Sasa. . .Lakini imani haina hoja. Haifanyi chochote ila kulishikilia Neno. Inaishikilia ahadi.

150 Sasa hebu tusome kidogo. Hebu tufungue Warumi, mlango wa 4, na kusoma kidogo tu. Na ni mpaka tutakapofinywa kweli na wakati, tutayasoma tu Maandiko haya, Warumi, mlango wa 4. Maana, kweli ninapenda kulisoma Neno. Linakusaidia ku—kulisoma Hilo. Warumi, mlango wa 4, na hebu tuanzie kwenye kifungu cha 17. Sikilizeni.

151 Paulo, akiandika wasifu juu ya maisha ya Ibrahimu, mwajua, hakuna kilichosemwa juu ya Ibrahimu akishuka kwenda Gerari,

wala hakuna kitu katika huo wasifu, mwajua. Ni kwamba tu, "Ibrahimu alimwamini Mungu," Paulo, yule mtume mashuhuri, akiandika wasifu juu ya Ibrahimu.

152 Kifungu cha 17, "Kama ilivyoandikwa . . . " Ninapenda hilo: Paulo, akidumu na Neno.

> *(Kama ilivyoandikwa, Nimekuweka kuwa baba wa mataifa mengi,) . . .*

153 "Nimefanya." Ibrahimu alikuwa na umri wa miaka sabini na mitano. Aliishi na mkewe tangu alipokuwa na . . . wote wawili walipokuwa vijana. Alikuwa dada yake wa kambo. Hamna watoto; yeye alikuwa tasa naye mke alikuwa mgumba. Lakini Mungu alikutana naye na kusema, "Nimefanya," wakati uliopita, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, hakika "nimekufanya baba wa mataifa mengi." Sio wa watoto wengi, bali mataifa mengi. Wazia tu hilo.

> *. . . mbele zake yeye aliyemwamini,* Mungu, *yaani Mungu, mwenye kuwahuisha wafu, ayatajaye yale yasiyokuwako kana kwamba yamekuwako.*

154 Usitoe hoja, hata kidogo. Sikilizeni.

> *. . . ayatajaye yale* yasiyokuwako *kana kwamba yamekuwako.*
>
> *Ambaye kinyume na matarajio . . .*

155 Jamani! "Pasipo hata na tumaini." Vipi kama angalitoa hoja? "Pasipo hata na tumaini."

> *Naye aliamini kwa kutarajia yasiyoweza kutarajiwa, ili apate kuwa baba wa mataifa mengi; kama ilivyonenwa, Ndivyo utakavyokuwa uzao wako.*

156 Haijalishi ni lingine lipi linalosemwa. "Mungu alisema hivyo, na hilo latosha." Loo, laiti Hawa angalikaa tu pamoja na hilo! Mnaona? Lakini yeye alisimama, kutoa hoja, kupata hekima. Ibrahimu hakutaka hekima yoyote. Yeye alitaka tu Neno. "Mungu alisema hivyo, na hilo linalimaliza."

157 Mnajua, nimehubiri juu ya hilo, mara nyingi. Akaenda akanunua nepi zote na vipini, na kila kitu, akajiandaa kwa ajili ya huyo mtoto mchanga, naye Sara akashona vibuti. Basi mwaka baada ya mwaka ukapita. "Mungu abarikiwe, tutampata, kwa vyovyote vile. Hiyo ni kweli."

158 "Kwa nini, yeye," daktari angesema, "vema, hawezi kumpata. Huwezi kumpata."

"Wala usiniambie mimi. Tutampata, kwa vyovyote vile. Jambo ndilo hilo."

159 "Pasipo na tumaini, hata hivyo aliamini katika tumaini." Matumaini yote yamekwisha, hata hivyo aliliamini wakati tumaini lilipokuwa tayari limekufa, kwake. Tumaini lilikuwa limekufa kwa kila utafiti wa sayansi, kila chimbuko la hekima.

Tumaini lilikuwa limekwisha, bali hata hivyo angali aliiamini. Ilikuwa ni kitu gani? Imani ndani yake; imani katika tumaini wakati tumaini halikuwapo. Hum! Ningependa kutulia kwenye hilo kidogo. Imani katika tumaini wakati hapakuwa na tumaini pale, hata hivyo angali aliamini katika tumaini. Mnaona? Maana, yeye alisema, "Yeye aliniambia, 'Ndivyo hao uzao watakavyokuwa.'"

160 Sasa, kifungu cha 19. "Basi asiyekuwa dhaifu wa 'hekima, maarifa, alikuwa na digrii yake'"? [Kusanyiko linasema, "La."—Mh.] La.

> . . .*asiyekuwa dhaifu wa imani,* (Ah! Haya basi.) *hakuzingatia hali ya mwili wake uliokuwa umekwisha kufa, . . .*

161 Matumaini yalikuwa yamekwisha. Mwili wake ulikuwa umekufa. Sikilizeni, yafuatayo:

> . . .*akiwa amekwisha kupata umri wa kama miaka mia moja, na hali . . .kufa kwa tumbo lake Sara:*

162 Tumaini lilikuwa limekufa. Mwili wake ulikuwa umekufa. Tumbo lake Sara lilikuwa limekufa. Yeye alifanya nini? Kifungu kifuatacho, "Hakusita." Loo, jamani!

> *Lakini akiiona ahadi ya Mungu hakusita kwa kutokuamini* (hekima); *bali alitiwa nguvu kwa imani, akimtukuza Mungu;*

163 Loo, jamani! Ati nini?

> *Huku akijua hakika ya kuwa, kile alichoahidi, alikuwa* pia anaweza *kufanya.*

164 Hum! Haidhuru nini, hakuna kuhojiana kwake, hata kidogo. Yeye analichukua tu Ne—Neno na kulishikilia. Sasa, kama *Hili* ni Neno la Mungu, mnaliamini? Basi kwa nini kushuku Neno lolote Lake, ahadi yoyote Yake? Mnawezaje kusema ya kwamba *Hili* ni sehemu, na *Hili* si zuri; na *Hili* ni *lile*, na kuchagua yale mnayotaka? Hamwezi kufanya hivyo. Ama lote ni zuri au hakuna lililo zuri. Kweli. Kwa hiyo, mara mnapoona kwamba ni Kweli, lishike. Msiliachilie, haidhuru hali ya mambo yakoje, jinsi wanavyojaribu kutoa hoja, "Mbona, huwezi." Msifanye, msifanye hivyo, hata kidogo. Dumuni nalo kabisa. Mungu aliliahidi.

165 Kama naenda sasa kuchukua msimamo wangu kwa ajili ya Kristo, na Yeye amenipa Roho Mtakatifu, Roho Yake inashuhudia juu ya Maisha Yake ndani yangu. Ndipo nikifikia kufa, Shetani anajaribu, aseme, "Sasa, unaona, wewe hukuwa mfuasi wa dhehebu." Dumu moja kwa moja na Neno. "Hukufanya *hivi*. Hukufanya *vile*." Haidhuru nini *hilo,* Shetani hana hoja kulihusu Hilo. Ni Neno la Mungu. Dumu na Neno. Unaona? Inaangusha mahojiano yote. Unaona? Huna hoja yoyote; hushikilia tu kwenye Neno. Unaona?

166 Sasa, imani kwa urahisi hulitumaini Neno Lake. Mnaona? Hivyo ndivyo Yeye alivyowataka wafanye. Hilo—hilo, sasa, mnapata msingi sasa. Hivyo ndivyo vile hasa Mungu aliitaka jamii ya binadamu kufanya: kutumaini kila Neno alilosema.

167 Naye Hawa alitumaini kiasi kikubwa Chake. Lakini kitu kimoja kidogo alikikubali, "Vema, nikijawa na hekima, labda—labda ilikuwa hivyo. Labda inapaswa kuwa *hivi*." Mnaona? Basi papo hapo ndipo alipopoteza mshikilio wake. Hapo ndipo alipoanza kuzamia, papo hapo. Hapo ndipo jamii yote ya binadamu ilizama moja kwa moja kaburini, kutoka papo hapo, kwa kuwa alitilia shaka Neno moja.

168 Baadhi yao husema, "Vema, ninaamini *Hili* ni kweli. Ninaamini *Lile* ni kweli. Ninaamini Mungu anaweza kuokoa, bali siamini Yeye huponya. Ninaamini Roho Mtakatifu, hakika, alishuka kwenye siku ya Pentekoste, bali hapana mahali ambapo kuna kitu chochote kinachosema Roho Mtakatifu alishuka, baada ya Pentekoste."

169 Loo, ndugu! Hivyo ndivyo wanavyolisema; wanajiita wenyewe makanisa ya Kristo. Mnaona? "Wenye mfano wa utauwa, bali wakilikana Neno." Aha! Aa-ha! Jambo ndilo hilo. Mnaona?

170 Huna budi kuamini. Usitoe hoja. Amini. Usijaribu kuwa na hekima. Liamini tu Neno.

171 Hekima hujaribu kutoa hoja na kuwasilisha njia bora zaidi. Sasa, hivyo ndivyo Shetani alivyomwambia Hawa hasa. "Sasa, hutakufa. Hakika hutakufa, maana Mungu ni Mungu mwema."

172 Yeye ni Mungu mwema. Na jinsi tu ninavyoweza kumtumaini, kwamba ni Mungu mwema, ni kwamba atadumu na Neno Lake.

173 Unawezaje kunitarajia kuwa mkweli wakati mimi si mkweli? Kama nikikwambia jambo moja, nifanye jambo lingine, neno langu haliaminiki kabisa. Mnaona?

174 Ingawaje, kinachomfanya Mungu mwema, ni kwa sababu Yeye alinena Neno, nasi inatupasa kuishi kwa Neno hilo. "Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno la Mungu, litokalo kinywani mwa Mungu." Basi, Mungu hana budi kudumu na Neno hilo. Hilo ndilo linalomfanya Mungu mwema.

175 Sasa, kama akisema, "Vema, nitawaacha wapite na *hili*. Mimi, nitawaacha wafanye *hili*. Vema, *hilo* ni sawa. Loo, mimi, ni—nitasonga *huku,*" mbona, Yeye hana msimamo, mnaona; Yeye si Mungu; Yeye ni—Yeye ni mtu wa kawaida tu. Mnaona? Lakini, ili kuwa Mungu mwema, Yeye hana budi kudumu na Neno Lake. Hilo linamweka kila mtoto...Iwapo atamwacha *huyu* kufanya uzinzi, *huyu* mwingine kunywa kidogo, na—na *huyu* mwingine angeweza kudanganya kidogo, *huyu* mwingine

anaweza kuiba kidogo, na huyu mwingine anaweza kufanya—kufanya *hivi*; kisha anifanye mimi nifuate tu nyayo, kuingia?

176 Yeye anayo njia moja, nao wote waingiao wataingilia kwenye lango hilo. "Mlango ni mwembamba, na njia imesonga. Hakuna unajisi utakaoingia mle." Katika Ufunuo, lilisema, "Wote walio nje ni wachawi, wazinzi, na mbwa, na kadhalika." "Heri nyinyi mfanyao amri Zake zote, apate kuwa na haki kwenye Mti wa Uzima." Hiyo ni kweli. Kunayo njia moja, hiyo ni ya Mungu.

177 Hatuitolei hoja, hakuna njia nyingine. Vema, kanisa la Kirumi linasema, "Sisi ndio Kanisa. Hiyo—hiyo Biblia hata haistahili ninii . . . Mbona, mbona, Hiyo, usingeweza . . . " Askofu Sheen alisema, "Kujaribu kuishi Kwayo, kulikuwa ni kama kutembea kwenye maji yenye matope." Mnaona? Unaona? Utafanyaje jambo hilo? Unaona? Basi, kama yeye ni sahihi, basi Biblia imekosea. Biblia ni sahihi; yeye amekosea. Sasa utasema nini? Iwapo Neno la Mungu ni la kweli, ama ni Askofu Sheen ama—ama Biblia. Sio tu Askofu Sheen, bali Kasisi *Fulani-wa-fulani*, na Dk. *Fulani-wa-fulani,* na *Fulani-wa-fulani*. Nisingelilitaja jina la mtu huyo, isipokuwa kama alilisema kwenye redio. Kwa hiyo, yeye alilisema kwenye redio, kwa hiyo nadhani ninaweza kulitaja jina lake. Dk. *Fulani-wa-fulani* na *Fulani-wa-fulani,* walisema *hivi-na-hivi* na *hivi-na hivi*. Sasa utamwamini nani, Mungu ama hao?

178 "Vema," wasema, "Kweli halilimaanishi tu *Hivi*." Linalimaanisha tu jinsi Hilo lilivyoandikwa.

179 Vema, huo ndio uongo wa kwanza wa ibilisi. Alimwambia Hawa, "Kweli halimaanishi *hivyo*. Hakika Mungu ni mzuri kupindukia kufanya hivyo. Hamtakufa." Bali walikufa. Nao watakufa, kila wakati. Hawana budi kukabiliana na Neno!

180 Hekima hujaribu kuchukua nji—njia bora zaidi, njia ya kisasa, njia ya kupendwa na watu wengi, ninii . . . njia rahisi zaidi, kujikuta huku.

181 Sasa hivi, hebu mchukue jamaa mmoja hapa, labda Mungu anaanza kumshughulikia. Sasa, anafikiri inambidi kuja huku. Inambidi kumfanya mke wake kuingia moja kwa moja mstarini. Inambidi kuachana na karamu zake za karata. Inambidi kuacha kwenda kwenye dansi. Mke wake hana budi kuacha nywele zake zikue. Inambidi kuacha kujipodoa. Inambidi kuacha kuvuta sigara, kunywa pombe. Inambidi kuachana na shirika hilo kubwa alilomo. Hana budi kujinyenyekeza madhabahuni. Hana budi kusimama na kuitwa mlokole, mtakatifu anayejibingirisha, Beelizebuli, chochote awezacho kuitwa. "Nitakuwa wa kidini, bali nitashuka niende *hapa,* nijiunge na kanisa hili *hapa* chini. Ninyi ni watu wenye mawazo finyu sana." Haya basi. Mnaona? Kunayo sababu, sababu.

182 Sasa tutafikia kwenye jambo kuu, katika dakika chache, juu ya hilo. Mnaona? Utajuaje ni lipi sahihi na lisilo sahihi, basi? Unaona?

183 Sasa, yanajaribu kulifanya Neno liseme jambo fulani, maarifa hufanya. Maarifa, hekima, hujaribu ku—kutoa hoja. Hekima hupata njia bora zaidi. Hakuna njia nyingine ila njia ya Mungu. Hekima hujaribu kuelekeza, kusema, "Loo, vema, sasa, mwajua, tusingeweza kufanya hilo kwenye wakati *huu*." Hatuna budi kulifanya, kwa vyovyote vile. Mnaona? Hujaribu kupata njia rahisi. Hujaribu kuifanya Biblia iseme mambo ambayo haisemi.

Sasa unasema, "Loo, Ndugu Branham, sasa wewe una . . . "

184 Ngoja tu kidogo. Tutarudi kwenye mbegu tena. Ni kitu gani ibilisi alichojaribu kufanya kwa hekima? Kulifanya Neno la Mungu kusema jambo fulani ambalo halikusema. Hiyo ni kweli. Alijaribu kulifanya Neno la Mungu liseme jambo fulani ambalo halikusema. Kwa hivyo hivyo ndivyo linavyokuja leo hii, wakati wanapojaribu kulifanya Neno la Mungu kusema jambo fulani ambalo halisemi.

185 Vema, wao wanasema, "Vema, nitakwambia, Ndugu Branham, wewe huna tafsiri ya kweli."

186 Biblia ilisema, ya kwamba, "Unabii si wa kufasiriwa apendavyo mtu binafsi." Kwa nini? Kwa nini si la kufasiriwa apendavyo mtu? Kwa nini? "Neno la Bwana liliwajia manabii." Hufasiriwa na nabii. Haliwezi kuwa la kutafsiriwa, apendavyo mtu mwenyewe. Manabii tayari wamelifasiri Hilo kwako. Hilo hapo, limeandikwa moja kwa moja Pale. Hivyo ndivyo linavyopaswa kuwa.

187 Mungu hana budi kuwa na kitu fulani cha kimsingi ambacho watu wote hawana budi kuhukumiwa kwacho.

188 Ikiwa ni kwa kanisa, ni lipi sahihi? Yapata mia tisa ya hayo, madhehebu mia tisa mbalimbali. [Ndugu Branham anakohoa—Mh.] (Samahani.) Ni lipi lililo sahihi? Utajuaje unaingia? Vipi kama wewe ni Mmethodisti, nao Baptisti wako sahihi? Vipi kama wewe ni Mpentekoste, Wapresbiteri wako sahihi? Vipi kama wewe ni Mkatoliki, na Walutheri wako sahihi? Vipi kama wewe ni Mlutheri, nao Wakatoliki wako sahihi? Mnaona?

189 Hapana budi pawe na msingi mahali fulani. Kwa hiyo kama Neno . . .

190 "Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu." Mnaona? Huyo Neno alikuwa ndani ya Mungu. Alikuwa ni Mungu. Ilikuwa ni mawazo Yake yaliyokuwa pamoja na Yeye, sikuzote Pale. Mawazo ya Mungu ni ya Milele kadiri alivyo Mungu. Amina. Hayo si maziwa yaliyoenguliwa, ndugu. Unaona? Hili hapa linakuja. "Mawazo ya Mungu yalikuwa ni Neno Lake, hapo mwanzo," hiyo ni

kusema, “katika Umilele,” sasa, wakati “mwanzo” ulipoanza kwanza, wakati. “Hapo mwanzo alikuwako Neno, mawazo ya Mungu, huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu.” Mnaona? Mawazo Yake ndiyo Yeye aliyokuwa.

191 Hayo ni wewe, pia. Kile mawazo yako yalicho ndicho ulicho wewe. Haijalishi kile unachojaribu kuishi, kwa kitu kingine, mawazo yako ndiyo uliyo. Huenda ukaendelea, ukatenda kama jamaa mzuri, lakini moyoni mwako wewe ni mwanamke mzinzi na chochote kile. Hivyo ndivyo ulivyo wewe, mawazo yako.

192 Nayo mawazo ya Mungu yalikuwa ni Neno Lake yaliyokuwa pamoja na Yeye na ndani Yake, na Hilo lilikuwa ni Mungu. “Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye huyo Neno akafanyika mwili.” Mawazo ya Mungu yalidhihirishwa katika mwili wa binadamu, “Alifanyika mwili, akakaa miongoni mwetu.” Haya basi.

193 Sasa, iwapo unao Uzima wa Milele leo hii, uko ndani ya Mungu. Kwa Utu wa Mungu ndani yako, wewe ni wazo la Mungu lililotamkwa. Whiu! Basi, usisikilize hoja zozote, taji yako isije ikachukuliwa, ikapewa mwingine. Usichukue hoja zozote, hata kidogo. Amini tu yale Mungu aliyosema ni Kweli, na udumu pamoja na Hiyo.

194 Kutoa hoja, kupitia kwa hekima, hujaribu kulifanya Neno liseme jambo fulani lisilosema.

Sasa unasema, “Hiyo ni kweli, Ndugu Branham?”

195 Vema, hebu turudi tu kwenye Mwanzo na tupate kujua. Hebu twende kwenye Mwanzo, mlango wa 3 wa Mwanzo, nasi tutasoma ki—ki—kifungu cha 4, tuone kama—kama hekima hujaribu kulifanya Neno liseme jambo ambalo silo. Mlango wa 3 wa Mwanzo, kifungu cha 4.

Nyoka akamwambia mwanamke, Hakika hamtakufa:

196 Unaona kile inawasilisha? Ni kitu gani? Kujaribu kulifanya Neno liseme jambo fulani ambalo halisemi. Mnaona?

Mungu alisema, “Mtakufa.”

197 Hekima, kama vile Shetani alivyokuwa akiliwasilisha kwake, kasema, “Hakika hamtakufa.” Mnaona? Ni kujaribu kulifanya Neno liseme jambo fulani, ambalo, “Sivyo lilivyo.”

198 Hivyo ndivyo hekima ilivyo siku hizi. Loo, ndugu, jinsi tungeweza kudumu kwenye hilo! Maseminari, shule za theolojia, hicho ndicho kiota chao chenyewe. Huo ndio umma wao, ni kujaribu kulifanya Neno la Mungu liseme jambo fulani ambalo halisemi.

199 Ninampa changamoto mtu yeyote anionyeshe Kanuni ya Imani ya Mitume katika Biblia. Ninampa changamoto mtu yeyote anionyeshe “ushirika wa watakatifu” katika Biblia.

Wote wawili Protestanti, Katoliki huamini hilo. Ninakupa changamoto unionyeshe moja ya mambo hayo, katika Biblia. Unaona? Ni umma wa hekima ukijaribu kutoa hoja.

200 "Vita vyetu si vya kimwili, bali vina nguvu, kutupa chini hoja zote, mnaona, kuziangusha chini ngome za Shetani." Kiumbe hicho kikuu, chenye madoido, kinachovutia! Sio mtia grisi mjanja; la, la, hiyo ni upande wa ndani. Lakini, upande wa nje, dhambi inavutia maradufu. Mwajua, dhambi inavutia.

201 Ni wanaume wangapi hapa ndani, na wanawake, wamepita umri wa miaka hamsini? Inueni mikono yenu. Sikuninii . . . Sikupaswa kuwauliza wanawake. Lakini mimi . . . Sisi sote tunakubali ukweli. Ninataka kuwaulizeni swali. Mnaona siku hizi kwamba wanawake ni warembo mara mbili, karibu hivyo, kadiri ya walivyokuwa, wakiwa mbioni, wastani kote ulimwenguni? Endapo hiyo ni kweli, inua mkono wako. Hakika. Wao ni warembo mara mbili kadiri ya walivyokuwa.

202 Chukueni picha za kale. Mwangalieni nyanya; sketi zake ndefu; msokoto wa nywele zake umening'inia mgongoni mwake. Hakuwa ni mrembo sana ukimwangalia.

203 Waangalieni wa kisasa siku hizi. Maskini nguo ndogo zinazobana mno, ambazo, kila umbo, hawezi kusogea pasipo kutenda dhambi. Akitembea, akijiinamisha mtaani, akiwa na hivyo vipodozi na vipodozi vya Max Factor anavyoweza kuweka juu yake, karibu zote. Akitengeneza nywele zake kama msichana mdogo. Amevaa sketi ndogo juu kidogo tu, karibu, juu ya magoti yake, kama anayo, hasa. Lakini, ukimwangalia, yeye ni mrembo. Shetani anajua jinsi ya kufanya hilo. Yeye ndiye mwanzilishi wa urembo, urembo wa aina hiyo ambao husababisha dhambi.

204 Dunia, yenyewe, ni tumbo la uzazi. Mungu aliweka mbegu Zake wapi? Mbegu huwekwa wapi? Katika tumbo la uzazi. Mungu huziweka mbegu. Naye mwanadamu hufanya nini? Kama vile ibilisi, katika tumbo la uzazi, atamfanya mtoto mchanga kuumbuka akiweza. Hivyo ndivyo pepo wamefanya duniani, kuchanganya mbegu, kuvifanya viumbe, sivyo. Afadhali niachane na hilo; kamwe sitayafikia haya mengine hapa, niliyoyaandika hapa chini. Mnajua ninalomaanisha. Hiyo ndiyo sababu kuna kiumbe kilichoumbuka kilicho tayari kutupwa. Mungu amemalizana nacho. Ulimwengu wote uko nje ya utaratibu. Kila kitu ni makosa. Vijito vimechafuliwa. Hewa imechafuliwa. Uchafu! Uvundo!

205 Maskini mzee Mhindi, sio muda mrefu uliopita, alisema, "Mzungu, sitaki kuishi muda mrefu zaidi. Nimemalizana na vita." Kasema, "Watoto wangu wachanga wako wapi? Wemekufa kwa njaa? Mke wangu yuko wapi?" Kasema, "Kabla hujaja huku na wanawake wako na wiski, na dhambi, tuliishi kwa amani. Ni ardhi yetu. Mungu alitupa sisi, bali unatunyang'anya. Utalipia hilo, siku moja."

206 Iangalieni, leo hii. Hayo majangwa makubwa, ya kupendeza na milima iliyotapanywa uvundo, dhambi, chupa za wiski, makopo ya pombe. Kila mahali pamejaa vilabu vya pombe na upuuzi mtupu. Reno, Nevada, jangwa lile kubwa huko ng'ambo, si kitu ila ukahaba. Ndivyo ilivyo ile miji mikuu, hata hewa na mazingira yamechafuka. Mahali wakati mmoja ile milima mikuu ilipokulia, sasa imekatakatwa kwa kila namna ya kila kitu kingine. Ambako miti ilikulia, imekatiliwa mbali. Ambapo yale majangwa, maji yalikotiririka bila kizuizi, kumechafuliwa. Ulimwengu wote uta—utageuzwa. Dunia itazaa mtoto wake kutoka kwenye mbegu. Umepotoshwa, pepo wakiurarua, wakiufanyia kazi, hakika, ni—ni uumbaji uliopotoshwa. Mungu atautupilia mbali na kuanza upya tena. Hiyo ni kweli.

207 Lilitoka wapi? Mtu mmoja kuamini ninii moja dogo... kutokuamini fungu moja dogo la Neno la Mungu.

208 Ulimwengu wote unaugua. Biblia inasema, ya kwamba, "Hata maumbile yenyewe yanaugua kwa ajili ya siku hiyo ya kufunguliwa, yakikungojea kule kudhihirishwa kwa wana wa Mungu." Miti inajitahidi, bure. Maua yanajaribu kuiangaza njia kwa ajili ya...Lakini, yanaugua na kulia, nayo yanajua kuna kasoro fulani. Kupotoshwa! Tumbo haliwezi kuzaa kilicho kikamilifu, kwa kuwa limepotoshwa. Ardhi inanuka. Imeloweshwa damu isiyo na hatia. Ina ninii...Iko kama...

209 Ningeweza kusema kitu fulani, huenda kisipendeze kabisa. Ni—ni—ni uvundo. Mungu alisema, "Kinanuka," mbele Zake, kichafu sana. Unaingia msalani, mahali pa kutabawali, na unavunda tu, umechafuka. Hivyo ndivyo ulimwengu unavyonuka hasa, pia, kama Mungu akiunukia. Uchafu, kitu hicho chote ni kichafu.

210 Mungu ataupasua vipande-vipande. "Nitaumba mbingu mpya na nchi," Yeye alisema. Naam, bwana.

211 Ni kitu gani? Tumbo lake la uzazi halijazaa Utawala wa Miaka Elfu. Limeleta kitu kilichopotoshwa. Kwa nini? Ukijaribu kuwa na hekima.

212 Sina neno dhidi ya Florida. Simaanishi hili kwenu watu wa kutoka Florida. Lakini wakati nilipovuka nikaenda Florida kwa mara ya kwanza, kisha nikarudi kwenye ngome ya Georgia pale, nilisimama pale pale na kusema, "Kama raia wa Marekani, ninaitoa sehemu yangu kwake kwa Waseminole ambayo ni mali yao." Mbona, wanashughulikia vitalu vyao vizuri kuliko ninavyozishughulikia nywele zangu, kila kitu ni chororo kama unyoya. Mitende ina taa kote juu yake. Vyombo vikubwa maridadi vya safari za anasa baharini na kadhalika, wakijaribu kuleta Utawala wa Miaka Elfu pasipo na toba. Kwangu mimi, ni lundo la utupu.

213 Mara milioni moja zaidi, ni heri nipande kule British Columbia, kwenye kilele cha kilima, na kuangalia kwenye

milima ambayo Mungu aliumba, wala mikono ya mwanadamu kamwe haikuigusa. Hakika.

214 Kwenda kwenye miji hii, makazi makubwa, hayo, hayo siyo, yanayonivutia. Ninachukia upuuzi wa namna hiyo. Mnaona?

215 Lakini ninajua ya kwamba siku moja, siku moja, itabadilishwa. Itamtupa mtoto wake aliyeteseka. Dunia, itabadilishwa, siku moja. Sawa.

216 Imani inaamini ya kwamba imeandikwa, na kusema, "Neno halina dosari."

217 Hivi mliwasikia wahudumu wakisema, "Vema, nawaambia, Toleo la King James, ama Toleo hili la Masahihisho, ama *hili* hapa, ni tofauti—ni tofauti tu kidogo. Kweli, halikumaanisha Hivyo"? Mmesikia hayo? [Kusanyiko linasema, "Naam."—Mh.] Loo, jamani! Ulimwengu umechafuliwa nayo. Mnaona? Ila imani haiamini hilo.

218 Imani huamini, Mungu anayeweza kunifanya mimi, anaweza kukiweka Kitabu hicho katika utaratibu nipate kuishi kwacho. Ikiwa Mungu Yule aliyeniumba anaenda kunihukumu, hawezi kukiweka Kitabu Chake katika utaratibu, basi Yeye ni Mungu duni sana. Haya basi. Ninaamini kila Neno Lake ni Kweli. Naam, bwana. Hii inafanya nini, kuamini hilo? Inaipa imani mahali pakamilifu ndani Yake pa kutulia. Mnaona? Huwezi kutokuamini, kwamba Neno hilo limeharibiwa, kwa njia yoyote. Inakupasa kuliamini Hilo jinsi tu lilivyo.

219 Kama ukijaribu kutumia hekima, kusema, "Sasa angalia hapa. Si jambo la maana kwamba Mungu alisema lingetenda jambo kama *hili*." Lakini Mungu kweli alisema hivyo. Mnaona? Hiyo ni kweli. Sasa, kama ukisema, "Vema, sasa, kama Mungu alifanya *hivi,* kama aliuchukua uhai wa mtu kwa sababu hakuwa Mlawi, naye akaweka mkono wake kwenye lile Sanduku wakati Hilo lilipokuwa karibu kuanguka." Haijalishi jinsi alivyokuwa ni mkubwa, Yeye aliuchukua uhai wake kwa ajili yake.

220 Mungu alisema, "Ni Walawi, peke yao, wangeweza kuligusa Hilo." Akauchukua. Hilo ndilo lililomchochea Daudi, mwajua. Mnaona? Mlawi, hakuna mtu ila Mlawi aliyepaswa kuligusa Sanduku hilo. Nalo hili hapa lile Sanduku, likirudi moja kwa moja kwa uamsho, naye mmoja nje ya hao akajaribu kulishika hilo Neno.

221 Hiyo inaonyesha ya kwamba waliopakwa mafuta wa Mungu ndio pekee wanaopaswa kuligusa Neno hilo. Kanuni hizi za imani na madhehebu hayana shughuli kulivuruga Hilo. Roho Mtakatifu tu ndiye aliye na haki kwenye hilo Neno, na ni mauti kwa mtu mwingine yeyote kuligusa. Ama, kutokuliamini lolote la Hilo, ama kulifundisha, "Huyo ataondolewa, sehemu yake, kutoka kwenye Kitabu cha Uzima." Usiweke mikono yako juu Yake. Kaa mbali Nalo. Sikilizeni. Amini tu yale Hilo linayosema. Usichukue neno la mtu mwingine yeyote. Chukua yale Hilo

liliyosema. Dumu moja kwa moja na Neno. Ni mauti kufanya lingine lolote Kwake. Sasa, maana ni . . .

222 Imani inafanya nini? Huliamini Hilo jinsi tu lilivyo. Hivyo ndivyo Mungu amelilinda kote katika wakati, nalo Hili hapa. Ni Neno la Mungu, kwangu mimi. Mungu analiheshimu hilo. Linatoa imani kamilifu katika ukweli Wake.

223 Ungewezaje kamwe kumwoa mwanamke endapo msichana huyo mdogo alikuwa—alikuwa—alikuwa amezurura-zurura na kufanya kila kitu, na kuishi katika ukahaba na kila kitu kingine? Na—na, hata hivyo, ulienda ukamtoa katika nyumba ya ukahaba. Akaja, naye alikuwa . . . Anasema, "Vema, nita—nitajaribu kuwa msichana m—mzuri zaidi." Huwezi kuwa na imani na mwanamke huyo. Unaona? Huwezi. Mwanamke anawezaje kuwa na imani na mwanamume aliyefanya jambo lile lile? Kamwe huwezi kuijenga imani yako pale. Hakuna kitu cha kujengea. Unaona? Huwezi kufanya hivyo.

224 Ungewezaje kwenda hapa nje na kusema, "Huu hapa mtumbwi ulio na mashimo mengi sana ndani yake, nami nitaushindilia magunia ya nyasi. Labda, huenda ikawa utaninii—utayastahimili mawimbi, kuvuka mto"? Nami nisingetaka kubahatisha kwake, wakati kunao mmoja umewekwa pale uliojengwa vizuri. Hakika.

225 Kwa nini tuchukue theolojia ya kujibunia yenye mashimo kote ndani yake? Imethibitika kwamba ni mbaya. Mnaona? Wakati, hili *hapa* moja limewekwa hapa, ambalo kweli ni Neno la Mungu, Yule aliyestahimili mawimbi, kupitia kwenye kila dhoruba kali na tufani. Limeshikilia vizuri kadiri lilivyoweza. Sikuzote litastahimili. Vema.

226 "Mbingu na nchi zitapita," kasema Yesu, "bali Neno Langu halitapita." Kwa nini? Ni ya Milele. Yalikuwako hapo mwanzo. Yeye amekuja tu huku kulidhihirisha Neno la Mungu. Yeye alikuwa dhihirisho la Mungu. Mungu alikuwa akijidhihirisha Mwenyewe kupitia Mwana Wake.

227 Yote haya yalianza katika Mwanzo, ule mlango wa mbegu, nayo yamekuwako tangu wakati huo. Tangu, yamekuwa jukwaani, limekuwa ni jambo lile lile, vita kati ya hekima na imani, sikuzote ni vita. Kwa hiyo, hekima ni ya ibilisi na kwa ajili ya watoto wake.

228 Hivi mliwahi kutambua? Ninyi nyote mmewaona kondoo. Nyote mmewaona mbuzi. Lakini, mwajua, kilio chao hao wawili kinafanana sana, inahitaji mchungaji halisi kujua tofauti yake. Ukimweka maskini mbuzi mmoja huko nje, umwache alie, alie. Kisha uende hapa na kumweka kondoo pale, na umwache alie. Uwasikilize. Sauti zao zinafanana kabisa. Lakini mchungaji halisi anaweza kuishika sauti hiyo.

229 Yesu alisema, "Kondoo Wangu wanaijua Sauti Yangu." Mnaona? Wanaweza kujua kama ni mbuzi. Vema, Yeye ni

Kondoo, Mwenyewe. Aa-ha. Yeye si ninii... "Kondoo Wangu wanaijua Sauti Yangu. Wageni hawatawafuata." Sauti Yake ni nini? Hii hapa, Neno. Mnaona? "Kondoo Wangu waijua Sauti Yangu." Mnaona?

230 Hawatamwacha mtu yeyote aseme, "Loo, sasa, hapa. Ninazungumza, Sauti ya Mungu, pia. Hii inasema *hivi* hapa." Lakini ni, mnaona, Shetani. Tutalifikia hilo katika muda kidogo, kuwapoozeshea hilo kwanza. Mnaona?

231 Sasa, sasa mnaona ya kwamba Neno mbegu haliwezi kukulia kwenye hayo mazingira, basi, ya maarifa. Hiyo ni kweli? Mnaona? Mara maarifa yanapochanganyikana na imani, inakufa papo hapo.

232 Hawa alikuja na kusema, "Bwana Mungu alisema: 'Siku tutakayokula hilo, siku hiyo tutakufa.'" Kisha akasimama kuona yale angesema.

233 Akasema, "Lakini, sikiliza, mpenzi, ewe maskini mrembo. Unaona? Hakika Mungu alikuumba kwa kusudi fulani. Unajua hiyo ni kweli. Unaona, wewe ni mwanamke, uliumbwa kwa kusudi hili. Hivyo ndivyo ilivyo. Hujui hilo sasa, bali uliumbwa kwa kusudi hili. Loo, wewe ni maskini mrembo, kipenzi. Aa-ha. Angalia maskini mikono hiyo inayovutia sana. Unaona? Mbona, hakika utakula. Hakika."

"Lakini Yeye alisema, kama—kama tukila, 'tutakufa.'"

234 Akasema, "Lakini, loo, unafikiri kwamba Baba mzuri, mwenye upendo, Mungu, angefanya kitu kama hicho?" Yeye alifanya nini? Alisikiliza hoja, akachukua hekima yake. Kasema, "Ni mti, unapendeza. Unaweza kutamanika." Naye akauangukia. Hiyo ni kweli kabisa. Basi alipouangukia, ilikuwaje? Kama vile ingekuwa kwa mwanamke yeyote. Mara unapouangukia, inamaliza papo hapo. Hiyo ni kweli.

235 Sasa, mnaona, ile mbegu aliyokuwa ameshikilia, naye hatimaye angalikuwa mama, kwa mapenzi ya Mungu, kupitia Neno lililonenwa. Hatimaye angalikuwa mama. Lakini, asingeweza kungojea, akaingilia hilo.

236 Sasa, mnaona, basi, mara alipofanya hivyo, alipoikubali hekima pamoja na Neno, nayo hiyo hekima ilikuwa ni kinyume na Neno...Mkielewa, semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mnaona? Endapo hekima iko pamoja na Neno, na inathibitisha kuwa pamoja na Neno, nalo Neno linajizaa Lenyewe kwa jambo lile lile, basi ni Neno. Bali ikiwa hekima inapingana na Neno, wala haiko pamoja na Neno, bali inajaribu kupata kitu fulani cha kuongezea Kwake ama kuondoa Kwake, ni ya ibilisi. ["Amina."]

237 Nazo mbegu za Roho Mtakatifu za Biblia haziwezi kukua kwenye mazingira ya hekima. Hilo linaiua kila seminari nchini. Hilo linatoboa mashimo moja kwa moja kuzipitia, linazitia

pancha, na—nayo hukumu inamiminika ndani. Hiyo ni kweli. Hakika inamiminika, mnaona, kwa maana Neno haliwezi kukua pamoja na hekima, hekima ya kilimwengu. Halitakua.

238 Hawa alipaswa kuliamini Neno jinsi lilivyotolewa kwake. Hiyo ni kweli? Hakupaswa kumsikiliza mtu mwingine yeyote akisema lolote kulihusu; jinsi tu lilivyotolewa kwake, hivyo ndivyo alivyopaswa kuliamini. Pasingekuwapo na mauti kamwe, kama angaliamini Hilo. Hiyo ni kweli.

239 Naye mwanamume au mwanamke atakayelichukua Neno la Mungu jinsi tu tulivyopewa Hilo, alishikilie jinsi Mungu alivyolisema, Hilo ni Uzima. Lakini kulichanganya na baadhi ya hekima ya dhehebu fulani, unakufa papo hapo, kama tu ilivyofanya hapo mwanzo. Hilo ni Mbegu. Hivyo ndivyo, hivyo ndivyo lilivyotenda kazi mara ya kwanza, hivyo ndivyo litakavyotenda kazi kila wakati. Daima limefanya hivyo. Mungu akitujalia, tutathibitisha hilo kote katika Biblia, asubuhi ya leo. Hivyo ndivyo tu Hilo linavyoweza kukua, ni kujitenga Lenyewe na hoja zote, ama chochote kingine, na kuliamini tu Neno.

Hawa alipaswa kulichukua jinsi tu Mungu alivyotupatia Hilo.

240 Nami nimewaelezea na kuwaambia ya kwamba Mungu amehifadhi na kuiweka Biblia hii, na hivyo ndivyo Mungu alivyonipa mimi hapa. Sitaki hekima nyingine yoyote. Ninataka jinsi tu Mungu alivyolisema Hapa.

241 Sasa, natumaini siwaudhi. Lakini kama Biblia ilisema ya kwamba sina budi "kutubu," inamaanisha kutubu; sio kufanya vitubio, bali kutubu.

242 Biblia ilisema nibatizwe, Jina la "Yesu Kristo," haikumaanisha kitu kingine. Haikumaanisha "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu." Ilisema Hilo.

243 "Vema," mnasema, "Mathayo 28:19 ilisema, 'Mkawabatize katika Jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu.'" Hivyo ndivyo ilivyokuwa hasa.

244 Sasa, kama hiyo si kweli, endapo hawana jambo sahihi, basi imani aliyokuwa nayo Petro, kubatiza katika Jina la Yesu Kristo, na Biblia nyingine yote, basi walikuwa na u—ufunuo wa uongo ambao Mungu alibariki. Hilo linamrudisha moja kwa moja: Ingalimbidi kumbariki Hawa hapo mwanzo, basi.

245 Jina la "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu," hizo ni sifa tatu. Kunalo Jina moja tu. Huwezi kubatizwa katika Jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu mpaka umebatizwa katika Jina la "Yesu Kristo," maana hilo ndilo Jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu. Nayo Biblia nzima imeandikwa namna hiyo. Kila mtu katika Biblia, aliyepata kubatizwa, alibatizwa katika Jina la "Yesu Kristo." Hakuna mtu katika Maandiko, aliyewahi kubatizwa katika sifa za "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu." Na

kila mtu aliyebatizwa katika Jina la—la "Bwana Yesu Kristo" alibatizwa katika Jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu.

246 Kila mtu aliyebatizwa, zile sifa za "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu," hajabatizwa katika jina lolote hata kidogo; sifa, kama vile mhudumu, kasisi, daktari, chochote zaidi; baba, mwana, na mwanadamu, mke. Sifa!

Kasema, "Haileti tofauti yoyote."

247 Basi andika sifa zako kwenye hundi yako, na si jina lako, uone kule itaenda. Aa-ha. Useme, "Ninaitia sahihi hundi hii katika jina la mke nyumbani." Vema, hilo linaleta maana nyingi kadiri lingalifanya kutokuliamini Neno la Mungu wakati ufunuo umewekwa hapo hapo mbele zako. Hakika ingeleta. Unaona? Hakika. Vema.

248 Linapaswa kuaminiwa jinsi Mungu alivyolisema Hilo. Halijipingi. Kama likijipinga, njoo unionyeshe. Aa-ha. Halijipingi, hata kidogo. Huenda Shetani akalipinga kwako, bali hawezi kulipinga Neno. La. Kwa hiyo, Neno halitavumilia hilo. La, bwana. Hilo ni jambo la kale, nalo limewaziwa, ila kamwe halijathibitishwa bado.

249 Hebu tuzifuatilie asili hizi mbili, ama yale huenda mkayaita mazingira, tuone kile yanachoumba. Hebu tuzifuatilie kwa dakika chache. Mazingira; asili hizi zote mbili zitaumba mazingira.

250 Ninataka kuwaulizeni jambo fulani. Hivi uliwahi kwenda kanisani . . . Na—nasema hili kwa uchaji sasa, na kwa . . . kutoa tu jambo muhimu; Mungu aepushe. Ulipata kwenda kwenye kanisa ambapo mchungaji ni mgumu kweli? Kusanyiko ni vile vile. Hiyo ni kweli. Mnaona? Ni kitu gani? Ni mazingira yaliyosababisha hilo. Nenda mahali ambapo mchungaji anasema, "Sasa, ngoja kidogo, hakuna kitu kama upuuzi huo. Siamini kitu kama uponyaji wa Kiungu, kuhusu ubatizo wa Roho Mtakatifu." Mwajua, utaona kila mmoja wao, hao, kusanyiko. Endapo wao si ninii . . .

251 Ikiwa kunaye tai mle ndani mahali fulani, yeye atatoka, miongoni mwa kundi hilo la kuku. Aa-ha. Hakika atatoka. Kweli kabisa. Ataliacha. Naam. Naam. Hakika ataliacha. Hawezi kuvumilia hilo. Yeye ni tai. Yeye ni ndege aliyejengwa apate kuruka angani, si kwenye kitalu. Naam, bwana. Sasa, huyu hapa.

252 Na sasa tunaona, kwamba, mazingira hayo. Nawe unaingia popote ninii . . . mambo hayo, ambamo imani inafundishwa kanisani, utakuta kanisa lililo katika mazingira hayo.

253 Ee Mungu! Hebu—hebu niwaelezee hili, kusudi, ninyi, kama mnaweza kuliona. Mnaona? Nendeni . . . Hiyo ndiyo sababu watu huja miongoni mwa watakatifu ambapo wanaomba, waaminio. Paulo alisema hakupata yeyote mjini, ila Timotheo,

hiyo ilikuwa Imani ya thamani kama ile aliyokuwa nayo, mwajua. Hao wengine wote ni wa kimadhehebu. Mnaona? Lakini alipoingia kwenye mazingira hayo, mnaona, yeye, unakuta mambo yakiendelea, ambayo hayo mazingira yameumba. Unawakuta watu wakiishi kwa imani unapofikia mahali ambapo linasema, "Jamani, mbona, Biblia ni ya kweli. Mungu huponya." Ukitembea miongoni mwa kusanyiko lao, utakuta, "Mbona, nilikuwa nikifa kwa kansa. Nikaponywa." "Wakati mmoja nilikuwa kipofu. Ninaona."

254 Huyo mgeni aseme, "Whiu! Jamani! Nini, mnataka kusema . . .? Ulikuwa na shida gani?"

255 "Nitakuonyesha kwenye kumbukumbu yangu. Njoo nyumbani pamoja nami. Njoo, ukale chakula cha kutwa pamoja nami ndipo nitakuonyesha jambo fulani. Ninayo kumbukumbu huko juu. Jirani zangu wanajua nilikuwa katika hali kama hii. Nilikuwa nimepooza, kwa miaka kadhaa. Nikaombewa." Unaona? Ni kitu gani? Neno hilo—hilo katika kanisa hilo, kundi hilo la waaminio, limeumba mazingira hayo.

256 Sasa, Neno, katika urahisi Wake bali hata hivyo katika ukamilifu wake, litakuaje katika mahali ambapo maarifa yanatia uvuli Hilo na kusema, "Haiwezekani"? Mnaona? Haiwezekani. Kwa hiyo, ambapo maarifa yanahubiriwa kutoka kwenye seminari, watoto hufa.

257 Mahali ambapo imani inahubiriwa kutoka kwenye Neno, watoto wanaishi. Amina. Hiyo ndiyo tofauti yake, ni Uzima tu na mauti.

258 Jambo lile lile lilitukia katika bustani ya Edeni. Hilo ndilo lililowapata hasa; mazingira mawili kule. Hapo Hawa alipoondoka kwenye Yale ya kweli, akaingia kwenye ya uongo, alikufa. Mnaona? Yatafanya hivyo, kila wakati.

259 Kwa hiyo, hawawezi kudumu. Ikiwa kanisa lako lina mazingira ya namna hiyo, loo, ewe mtoto, ukitaka kuishi, wewe liamini Neno.

260 Sasa, hapa patakuwa na mwiba mdogo sasa. Nami silimaanishi kwa njia yoyote ya ukali. Ninaninii tu . . . Haya ni mafundisho. Huna budi, unapozifikia sehemu hizi, huna budi kuchoma na kuunguza, kidogo, unaona.

261 Sasa ngoja. Ni kama tu kumtia ndama alama. Nilikuwa ninachukia kufanya hivyo, kumtia ndama alama; maskini jamaa huyo mdogo. Tungekimbia huko. Na sijui kama mliwahi kuwarushia kamba ndama, au la, na—na—na—na kuwafunga. Unawarushia kamba, unaona, unakingamisha ninii . . . Naye maskini jamaa huyo mdogo! Unakimbia huko chini, unakichukua chuma hiki chenye joto cha kupiga chapa, unakichomelea kwake. Loo, ndugu, lilionekana la kuchukiza sana. Uliposimama, kweli alishikwa na wazimu wa kutimua mbio. Alikimbia tu na kurusha mateke, na kupiga makelele na

kulia, na kuendelea. Lakini, nawaambia, walijua, tangu hapo na kuendelea, alikuwa ni mali ya nani. Hiyo ni kweli. Walijua alikuwa wa malisho ya—yapi. Hakuna mchezo kuhusu hilo basi.

Kwa hiyo, hebu tupige chapa. Hebu tupige chapa. Naam, bwana.

262 Wakati waliposema, mwajua, ninii . . . Nyinyi, wengi wenu, mmesoma ama—ama kuimba ule wimbo wa *Tafakari la Kaoboi*, mnaona. Na yule ndama wa mwaka mmoja aliyepotea, wanapomwingiza ndani, yule wa mwisho pale, kwenye ule msako; yule ndama wa mwaka mmoja aliyepotea, wanamfanya tu supu, maana hana chapa yoyote juu yake, hata kidogo. Na hivyo basi hao wengine wanaenda malishoni mwao. Lakini bosi wa huo msako anajua ng'ombe wake, kwa hiyo kama wewe . . . Chapa huumiza.

263 Sasa angalieni. Shetani angeweza kuthibitisha kisayansi, kwa hekima yake . . . Sasa nitachukua mahali pa daktari hapa, kwa dakika chache. Shetani angeweza kuthibitisha kisayansi, kwa hekima yake, ya kwamba udongo aliokuwa akitaka kutoa, jamii ya wanadamu ipate kukulia, ulikuwa na vitamini. Hakika ulikuwa nayo. Angeweza kuthibitisha hilo kisayansi. Wanaweza kuthibitisha kisayansi chochote wanachotaka, karibu chochote. Mnaona? Hakika.

264 Ulikuwa na vitamini P, "anasa, umaarufu." [Kiingereza: "pleasure, popularity."—Mf.] Hiyo iko ndani yake. Hiyo iko kwenye udongo wake wa hekima. Hakika. Hakika. Anasa zote za ulimwengu, sinema zote, madansi yote, yote, chochote, "Endelea. Hilo ni sawa. Halitadhuru kitu. Hakika." Mnaona? Umaarufu, "Loo, ninyi ndilo kanisa kubwa kuliko yote lililoko mjini." Vema.

265 Ulikuwa na vitamini C ndani yake, ambayo aliitaja kama "maarifa ya kawaida." [Kiingereza: "common sense."—Mf.] "Inatoa hoja, unaona." Naam.

266 Ulikuwa na vitamini R ndani yake, iliyomaanisha "hoja." [Kiingereza: "reasonings."—Mf.] Naam, angeweza kutoa hoja. Lakini, unaona, hiyo haitafanya kazi.

267 Ulikuwa na vitamini bee, B, ndani yake, inayomaanisha "urembo." [Kiingereza: "beauty."—Mf.] Shetani ni mrembo. Dhambi inapendeza. Nayo dhambi inapoanza kuongezeka zaidi na zaidi, ndivyo inavyozidi kuwa ya kupendeza.

268 Ni nyumba bora sana jinsi gani tuliyo nayo siku hizi kuliko ile nyumba ya magogo? Ni nzuri zaidi jinsi gani? Wanawake wetu ni warembo zaidi jinsi gani siku hizi kuliko walivyokuwa? Mnaona? Florida ni nzuri zaidi jinsi gani, ilikuwa sasa, na jinsi Mungu alivyoiumba? Mnaona?

269 Inao urembo. Ni wangapi wanaojua ya kwamba Shetani ni urembo? Naye alitamani urembo, kisha akajaribu kuumba

urembo, ufalme wa kupendeza zaidi, na kadhalika. Hakika. Tunajua jambo hilo. Shetani yuko katika urembo.

Sasa angalia. Yeye alikuwa na vitamini R, ambayo ni "hoja."

Vitamini B, ambayo ni "urembo."

270 Vitamini M, ambayo ni "mamboleo." [Kiingereza: "modern."—Mf.] "Loo, unataka kuwa wa kisasa." Chukua tu maarifa yake uone kama huamini upuuzi huo. Yatakua moja kwa moja ndani yako. Vitamini hiyo itakuja moja kwa moja mahali unapoketi.

271 Jamaa fulani anasimama, anakupa maarifa yake kidogo, "Sasa, angalieni, enyi marafiki. Ingekuwaje kama tungalichukua kanisa hili kubwa linalopendeza la dayosisi hapa na liwe na makelele mengi sana, na kulia, na kunena kwa lugha, na kukimbia huku na huku sakafuni, na kutoa povu kinywani kama mbwa wenye kichaa? Basi—basi unafikiri meya wa mji angesema nini, halmashauri ya mashemasi, kama tulikubalia upuuzi kama huo kuingia humu?" Loo, hakika, ni ya kisasa.

272 "Mnafikiri watu wetu wangesimama kule chini mtaani, wakiwa na tari mkononi mwao? Nalo lingefanya nini kama dada zetu wangekuja na nywele kubwa, ndefu zimening'inia chini? Nao hao wanawake wengine wa kanisa wakipitia mjini, 'Angalieni pale. Angalieni pale.' Mbona, rais wa kanisa hili, ama chochote kilicho, mwajua, 'Vema, angalieni, angalieni pale. Yeye anaonekana kama ni mtindo wa kale, sivyo? Tairi yake ya akiba imeisha pumzi mgongoni mwake.'" Mnaona? Mwajua, kitu kama hicho.

273 "Tunataka kuwa wa kisasa." Mnaona? Hiyo ni hekima ya ibilisi. Hayo ndiyo inayokuza. Hiyo ndiyo vitamini iliyo kwenye udongo, inayotokeza katika bidhaa inayozaa. Endelea, ewe Yezebeli mamboleo. Vema. Mamboleo, kama vile wanawake wa siku hizi. Hakika. Loo, mamboleo. "Vema, watu wa kisasa kuliko wote wa mjini watakuja kwenye hilo kanisa." Hakika. Halina budi . . . Mbona? Wao hukulia katika vitamini hiyo ya kisasa.

274 Vitamini ya kutoa hoja, vema, zinakulia humo. Mnaona? Hivyo ndivyo ilivyo, kutoa hoja. Lakini mara unapoanza kukulia humo, umekufa kwa Neno. Inakubidi kulikana Neno kabla ya kuweza kuwa hilo. Unaona?

275 Jinsi tu unavyoweza kuwa mwenye dhambi ni kulikana Neno la Mungu. Dhambi ni kitu gani? Kutokuamini. Kutokuamini nini? Neno la Mungu. Unaona? Inakubidi kulikana Neno, kwanza.

Sasa, loo, nina yapata vitamini zingine kumi zilizoandikwa hapa chini.

276 Lakini hii hapa vitamini moja ambayo alikosa kuwaambia. Alikuwa na vitamini D mle ndani. Hiyo ndiyo vitamini iliyo

kubwa kuliko zote mle ndani, matokeo, “kifo.” [Kiingereza: “death.”—Mf.] Mnaona?

277 Ndilo kundi la watu waliovalia nadhifu kuliko wote, la kisasa kuliko yote yaliyopo, kanisa la kupendeza kuliko yote, dhehebu lililo kubwa kuliko yote, mnaona, la kisasa kuliko yote lililokuwepo, la kupendeza kuliko yote lililokuwako, mambo ya maana sana yanayoweza kusemwa. “Mbona tusininii . . . ”

278 “Kama Mungu alitufanya kiumbe Chake, kwa nini awahukumu wanawake hawa wasionekane warembo wawezavyo, wawe na nywele fupi? Kwa nini Yeye ahukumu kipodozi kidogo?”

279 Vema, Yeye alikuwa na mmoja katika Biblia aliyejipodoa, Naye akamlisha kwa mbwa. Kwa hiyo ninyi wazieni tu hilo, mnaona. Hiyo ni kweli kabisa.

280 “Mbona—mbona Mungu afanye hivyo? Mbona, jamani, Yeye hatutarajii kuishi kulingana na Biblia hiyo.” Hakika alifanya hivyo. Alimwambia Hawa hana budi kuishi . . . Ama, Yeye alimwambia . . .

281 Yesu alisema, kwamba, “Mtu huishi kwa kila Neno, kila Neno litokalo kinywani mwa Mungu.” Ni nani aliyesema hilo? Yesu. Hiyo ni kweli? Alisema, “Kama mtu mwingine yeyote akisema lolote tofauti, na awe mwongo; Neno Lake liwe kweli.” “Mbingu na nchi zitapita, lakini Neno Langu halitapita.” Haya basi.

Kwa hiyo vitamini D iko kwenye fomula yake, mamboleo. Hiyo ni kweli.

282 Sasa, lakini, Neno mbegu ya Biblia haiwezi kukua kwenye udongo kama huo. Mtu angewezaje kwenda katika moja ya hayo makanisa mamboleo sasa? Roho wa Mungu analishukia, nao wa—wanataka kulia kwa shangwe, “Utukufu kwa Mungu! Haleluya!”

283 Mnajua nini? Mbona, mngemfanya huyo mhubiri ameze mahubiri yake. Mbona, ninawaambia. Ni—ninaweza tu kumwona yeye akisema, “Umhu.”

284 Ndipo hao korongo wote mle, watanyosha shingo hiyo, mwajua, waangalie kote, wapate kuona. “Vema, ni kitu gani kilichosema hayo?”

285 Halafu, dakika chache, mhubiri angesema, “Yesu Kristo, Mwana wa Mungu.”

“Utukufu kwa Mungu! Hiyo ni kweli.”

286 “Umhu,” mashemasi. Haa! Wewe, wewe uko mlangoni, katika dakika chache. Watakutupa moja kwa moja nje. Unaona?

287 Neno haliwezi kukulia hapo, haliwezi kamwe. La, kamwe haliwezi. Mnaona? Haliwezi tu kabisa. Mnaona?

288 Kisha anakuja, akinyunyizia sumu yake juu Yake, kujaribu kuua chembe ya Uzima ndani yako. "Sasa kunalo kundi la watu nchini siku hizi, linaloamini kwamba Mungu huponya. Mbona, hakika, tunajua, hisi ya akili inaonyesha kwamba Mungu alitupa madaktari, kuponya."

289 Sasa, hebu muulize daktari mzuri, mwenye akili kama yeye ni mponyaji. Atakwambia, "La, bwana. Ninaweza kung'oa jino, bali siwezi kuliponya tundu linamotoka." Hiyo ni kweli. "Ninaweza kuuweka mkono, bali siwezi kuuponya." Kweli kabisa. "Mungu ndiye Mponya." Mnaona?

290 Sasa, kitu chochote kitapataje kukua katika upuuzi kama huo? Neno mbegu linawezaje kamwe kukua katika kitu kama hicho? Kamwe haitakua. Haiwezi kukua katika mazingira ya namna hiyo. Bila shaka haiwezi.

291 Lakini imani hukua tu katika vitamini moja. Ina vitamini moja tu. Haiibidi kuwa na mchanganyiko wowote, hata kidogo. Imani hukua katika vitamini moja, hiyo ni Neno. Hicho ndicho kitu pekee ambacho imani inaweza kukulia, ni Neno. Na jinsi pekee inavyoweza kukua ni kwa sababu inaliamini Neno, nayo haina budi kuchukua Neno lote na kuamini ni kweli. Nayo vitamini ya imani huendelezwa katika neno dogo la herufi nne, U-h-a-i, "Uhai." Ina vitamini L, imani inayo. Imani ina vitamini L.

292 Hekima ina vitamini P; vitamini R; anasa; na vitamini hoja; vitamini, vitamini hizi zingine zote. Hizo, ima-. . . ho-. . . Maarifa yana hizo zote. Mnaona? Hekima ina hayo yote, hutoa hoja.

293 Lakini imani inacho kitu kimoja tu: Uhai. Huo ndio tu utakaodumu. "Neno Lako ni Uzima. Neno Lako ni Kweli. Yeye ni Neno, Njia, Kweli, Nuru." Imani huning'inia tu papo hapo. Hivyo tu. Wala haitaichukua. Uzima wa Roho Mtakatifu, Uzima wa Milele, humo ndimo imani inamokulia: Neno, *Zoe*, Uhai wa Mungu Mwenyewe. Hapo ndipo mahali pekee imani inapoweza kutenda kazi, ni wakati imani inapolisikia Neno na kuamini ya kwamba Hilo ni Neno la Mungu. Ndipo, katika hiyo Zoe, linakua na kuzaa yale Neno liliyosema.

294 Mungu, Yeye aliufanyaje ulimwengu? Mnaamini ulimwengu ulikuwa katika mawazo ya Mungu? Hakika, ulikuwa, ilibidi uwe. Yeye aliufanyaje? Alinena tu.

295 "Yeye atapata wapi vitu hivyo?" Ungewezaje kuhojiana na Mungu, useme, "Mungu, ulipata wapi hizo nyenzo, ku—kufanya mawe kwake? Ulizipata wapi?" Zilitoka kwenye gesi. "Ulitoa wapi hiyo gesi, Bwana?" Mnaona? "Uliumbaje maji? Fomula yake ni ipi? H_2O. Ulipata wapi haidrojeni, oksijeni?" Mnaona? Jambo ndilo hilo. Mnaona? Kamwe halileti maana.

296 Mungu alisema nini? Yalikuwa katika mawazo Yake. Nayo mawazo Yake ni Neno Lake, kabla halijadhihirishwa. Ndipo basi

hapo mawazo Yake yaliposema, "Na iwe," ikawa. Jambo ndilo hilo. Hapo ndipo imani inapokaa.

297 "Kwa...ninii..." Waebrania 11 ilisema, "Kwa imani ulimwengu uliumbwa." Ulimwengu uliumbwa kwa imani. "Mungu aliufanya ulimwengu kwa vitu visivyoonekana." Kwa imani Mungu alinena ulimwengu ukawepo, kwa sababu li—lilikuwa ni Neno lililokusudiwa kimbele. Lakini mara alipolisema, likawa uhai.

298 Sasa unaweza kusema, "Ninaamini Hilo, Ndugu Branham." Moyoni mwako unaweza kuliamini. Basi litamke, "Ninaliamini." Kamwe usilibadilishe, hata kidogo. Dumu moja kwa moja Nalo. Angalia kile kitakachokulia kwake. Itazaa Neno, maana ni imani. Mnaona? Hekima inakuondosha. Imani inakuleta Kwake. Unaona hilo?

299 Hiyo inakatilia mbali kila kanuni ya imani ya kujibunia, inakatilia mbali kila shule ya kusomea, ya thiolojia ya kujibunia, inaziponda ikaziangamiza. Hizo hapo, profesa wao, D.D., Ph.D., L.L., Q.U.D., na jamaa hawa wote inawabidi kwenda shuleni na kujifunza saikolojia na mambo haya mengine yote. Kuna Kitu kimoja tu anachokiacha nje. Jinsi ya kujiwasilisha mwenyewe pamoja na saikolojia, na kwamba atavaa nguo za aina gani, na jinsi inavyompasa kusema "amina" vivyo hivyo tu, na, loo, upuuzi! Acha ninii...

300 Ongozweni na Roho Mtakatifu. Wana wa Mungu wanaongozwa na Roho wa Mungu, sio hekima ya seminari. Lakini Roho wa Mungu huwaongoza wana na binti za Mungu. Hakika. Ni kweli. Amina.

301 Sasa, hutoa kila kanuni ya imani, kila shule ya kusomea, kila theolojia ya kujibunia. Si ajabu wao hawawezi kuamini; hakuna kitu humo ndani kwa ajili Yake kukulia. Mnaona? Wana vitamini R, kutoa hoja, ambayo tunapaswa kuondolea mbali. Vitamini ya umaarufu, vitamini ya anasa, "Sina budi tu kujifurahisha kidogo." Ni raha ya aina gani? "Loo, kutoka nje na kulewa kidogo, mara moja moja, wajua. Kujifurahisha tu kidogo; haitaleta tofauti yoyote."

302 Mwajua, mambo madogo kama hayo hapo, hayo ni hizo zote, vitamini hizo zote. Mnaona? Basi vitamini ya aina hiyo italikuzaje Neno, ambalo huikataa vitamini hiyo? Utafanyaje hilo? Mnaona? Neno huikataa hiyo. "Mkiupenda ulimwengu, au mambo yaliyo katika ulimwengu, kumpenda Mungu hata hakumo ndani yenu," ilisema Biblia. Mnaona? Kwa hiyo ni vipi—ni vipi ninii la Mungu...Neno la Mungu litakuaje chini ya vitamini kama hizo?

303 Inahitaji vitamini fulani udongoni kuzaa nafaka. Haina budi kuwa katika udongo wa aina nzuri. Tunalifikia, katika muda kidogo tu. Mnaona? Haina budi kuwa na aina nzuri ya udongo, la sivyo haitakuza nafaka. Hebu chukua ardhi fulani, haitakuza

huu, na itakuza kitu kingine. Ardhi ya mchanga, vitamini mbalimbali, kadhalika, inakuza vitu fulani. Isipozikuza, mbona, hunayo, kamwe haitakua. Hivyo tu.

304 Sasa, magugu yatakua karibu popote, udongo wa namna yoyote. Hiyo si ni kweli? Magugu ya kale ya kimadhehebu yatakua tu kila mahali.

305 Lakini, ninakwambia, ndugu, ukitaka kuzaa matunda ya Uzima, hayana budi kutoka kwenye Neno. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Hakika. Vema.

306 Ninatumaini siwaweki muda mrefu kupita kiasi, asubuhi ya leo. [Kusanyiko linasema, "La."—Mh.] Mnaona? Sasa, msininii . . . Mnaona? Vema.

307 Si ajabu hawawezi kuamini; hawana kitu cha kuishia. Yesu alinena habari zao katika Mathayo mlango wa 13 na kifungu cha kwanza. Hebu tufungue hapa tuone jinsi Yesu alivyosema kulihusu, mambo haya tunayozungumzia. Mathayo mlango wa 13, na katika kifungu cha kwanza.

> *Siku ile* Yesu akatoka *nje ya nyumba, akaketi kando ya bahari.*
>
> *Wakamkusanyikia . . . makutano wengi, hata akapanda chomboni, akaketi* chini; *na ule mkutano wote wakasimama pwani.*
>
> *Akawaambia* hao mambo mengi, na *akawaambia mambo mengi kwa mifano, akisema*, *Tazama, mpanzi alitoka kwenda kupanda* mbegu;
>
> *Hata alipokuwa amepanda,* mbegu *nyingine zilianguka karibu na njia, ndege wakaja wakazila:*
>
> *Nyingine zikaanguka* juu ya *miamba,* nazo hazikuwa *na udongo mwingi: nazo* mara zikaota, *kwa udongo kukosa kina:*
>
> *Na jua lilipozuka, ziliungua; na* zikaja . . . *na kwa kuwa hazina mizizi, zikanyauka.*
>
> *. . . nyingine zikaanguka penye miiba; ile miiba ikamea, ikazisonga* kabisa:
>
> . . . nyingine *zikaanguka* penye *udongo mzuri, zikazaa* nyingine, zikazaa *tunda*, *moja mia,* . . . sitini . . . na *thelathini.*
>
> *Mwenye masikio ya kusikia, na asikie.*

308 Sio hekima. "Masikio," mnaona, vema, "kusikia." Vema.

309 Angalieni. Alisema nyingine zilianguka, wakati ile Mbegu ilipotoka, ikalihubiri Neno.

310 Nyingine zikaanguka karibu na njia; kama tu maji juu ya mgongo wa bata, yanavyomwagika.

311 Zingine zikaanguka penye miamba, mawemawe, yalikuwa tu na mavumbi kidogo yaliyopeperushwa pale. Zikaota, bali hazikuwa na mizizi, hakuna mahali pa kutia mizizi yake. Sasa nitatoa mifano hapa, nami natumaini sitaudhi hisia zozote. Mnaona?

312 Hilo lilikuwa ni kanisa Katoliki. Wao walisema walijengwa juu ya mwamba. Nitakubaliana nao. Hakika nitakubaliana nao. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Hamna ardhi chini yake, hata kidogo, hamna ardhi juu yake ya kukulia. Kwa nini? Isingeweza kuzaa . . . Wasingeweza kuzaa vitamini ya Biblia, maana hata hawaiamini. Fundisho lao ni mafundisho ya sharti, hiyo ni kweli, mafundisho ya sharti ya Kirumi, hakuna Neno ndani yake, hata kidogo. Mnaona? Zikaanguka juu ya miamba; hiyo ilikuwa ni hekima kuu. Loo, ndugu, ninawaambia, walikuwa nayo katika njia kuu sana. Wanalielezea katika njia ya saikolojia, na mijengo mikubwa mno, na nguo nzuri, wanaonekana kama miungu mitakatifu, ya makasisi na kila kitu kingine.

313 Ni wangapi waliosikia ushuhuda ule wa maskini yule mtawa ambaye ndio kwanza atoroke? Mnao hapa? Ninataka huo uchezwe Jumatano fulani usiku hapa kanisani, na kila mtu hapa anapaswa kuwa na ushuhuda huo. Mmoja wao alinifuatilia kwa muda mrefu. Jinsi ambavyo wao . . .

314 Nilishuka kule Meksiko, mimi mwenyewe, na nimeyaona hayo mashimo ya chokaa, mashimo ambamo watoto wa hao watawa; wakati makasisi wangewapata kwa hao, watoto wachanga; ambamo walichomewa ndani ya hayo mashimo ya chokaa, na vitu kama hivyo. Hilo ndilo lililoufanya ukomunisti uinuke huko Meksiko. Walivunjilia mbali huo upuuzi mtupu. Hilo ndilo lililoufanya ukomunisti uinuke huko ng'ambo.

315 Kamwe msiogope ukomunisti. Mungu anautumia ukomunisti. Siuamini. Ni wa ibilisi. Bali Mungu humchukua ibilisi na kurejea tena papo hapo, kama vile Yeye alivyofanya na Mfalme Nebkadreza, kisha akaja kule na kuwachukua Israeli. Mnaona? Naam. Ninyi angalieni mwone kama Biblia hailithibitishi. Moja ya siku hizi tutaliendea. Mungu aliuinua moja kwa moja, apate kuwalipizia kisasi watoto wa Mungu, juu ya maskini kahaba huyo. Hivyo ndivyo Biblia ilivyosema hasa. Naam. Kasema, "Watamteketeza kwa moto, naye ataufikia mwisho wa maangamizi yake." Hayo ndiyo yatakayompata hasa, pia. Huyo hapo.

316 Hizo ni zile zilizoanguka penye miamba, udongo mdogo tu hata kitu hicho kisingeweza kukua. Kikafa. Halafu, hiyo ilikuwa ni hekima kuu.

317 Halafu zingine zikaanguka penye udongo wa Kiprotestanti, lakini, baada ya kitambo kidogo, hekima kuu ya madhehebu makuu ikazisonga, ikamsonga Roho akatoka. "Siku za miujiza zimepita. Dk. *Fulani-wa-fulani* alisema *hivi-na-hivi*. Mnaona?

Hakuna kitu kama hicho." Kamilifu tu, zote zikasongwa. Yakasonga kitu gani chote kikatoka? Yakamsonga Roho, kwa ajili ya hekima. Mnaona?

318 Roho Mtakatifu alishuka katika siku za Martin Luther. Roho Mtakatifu alishuka katika siku za John Wesley. Roho Mtakatifu alishuka katika siku za kanisa la mwanzoni la Kipentekoste. Lakini madhehebu yamefanya nini? Kwa hekima yao, walimsonga akatoka. Wakasonga kitu gani? Ile Mbegu. Mbegu ni nini? Neno. "Halimaanishi Hivyo. Linamaanisha *hivi*, pale." Mnaona? Wanalipata . . .

319 Sasa, watu wengi wenye mioyo miaminifu wa hao wahudumu, nimekutana nao, tukaketi na kuwazungumzia, hata kwenye hoja ya ubatizo na mambo mengi. Nimeomba yeyote aje, kulijadili. Wakasema, "Ndugu Branham, kama tungefanya hivyo, kanisa letu lingetutoa nje."

320 Nikasema, "Nani? Ni lipi lililo muhimu sana kwenu, Neno la Mungu ama kanisa lenu?" Kamwe hutaenda mbali zaidi, katika mavumbi hayo ya madhehebu. Mnaona? Mnaona? Vema. Iwapo linalikana Neno, ni baya. Mnaona? Inaonyesha ni hekima iliyobuniwa na mwanadamu.

321 Sasa, Waprotestanti walikabwa wakatoka. Iliikaba Roho moja kwa moja ikawatoka, walipoanza kuchukua hekima badala ya imani katika Neno; hekima katika dhehebu, hekima ya kimadhehebu badala ya imani katika Neno. Wote wanaoelewa hilo, semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mnaona? Imani katika yale—yale kundi la watu, la Methodisti, Baptisti, Presbiteri, Pentekoste, Wakiinjilisti, na wote wakakusanyika pamoja. Na karibuni wataunda muungano wa kanisa, ambao utakuwa ndio "ile alama ya mnyama." Naye atakuwa na mamlaka yale yale katika taifa hili, Ufunuo 13:11, waliyokuwa nayo kule; nao watasababisha mateso juu ya watakatifu, kama tu vile walivyofanya hapo mwanzo, ka—kanisa la Kirumi. Mnaona? Huko ndiko linakoelekea moja kwa moja sasa.

322 Basi hiyo ndiyo sababu Neno linapandwa sasa, kila mahali, "Kaeni mbali nalo. Tokeni kwake." Mnaona?

323 Sasa, hekima ililisonga kabisa. Hekima yao wenyewe inamsonga Roho Mtakatifu kutoka kwao. Hebu niwathibitishie, katika Biblia, Ufunuo, mlango wa 3; ambapo ndio kwanza tupitie zile nyakati za kanisa. Yesu alikuwa amekabwa akatolewa Kanisani Mwake, naye alikuwa nje; akijaribu kubisha mlangoni, arudi ndani. [Ndugu Branham anagongagonga mimbarani—Mh.] Aa-ha. Hivyo ndivyo lilivyosema hasa. "Nasimama mlangoni nabisha. Mtu yeyote akiona kiu, kama ataniruhusu tu niiingie, nitakuja." Lakini hakuna aliyefungua mlango. Mnaona? Walimweka nje. Ilikuwa ni kitu gani? Walikuwa na ninii . . . Mbegu iliwaangukia. Mnaona? Mnaona?

324 Lakini nyingine zilianguka katika bonde la mateso. Baadhi ya mbegu zilienda katika bonde la mateso. Sasa, katika bonde ndipo unapata maji, udongo ulio bora zaidi. Unapomchukua mtu ambaye amepigwa sana hata theolojia yote imetwangwa ikamtoka, ikachekwa ikamtoka, ikadhihakiwa ikamtoka, ambapo amepitia kwenye vinu vya kusagia na yote ikasagwa ikamtoka, mpaka chuma kimekuwa tayari kwa ajili ya kazi, utakuta kwamba kuna unyevu karibu na hapo. Hiyo ni kweli. Katika bonde, jamaa huyo ametupwa bondeni, akafukuzwa kwenye dhehebu lake. Yeye yuko "huko chini jalalani," wanavyokuita. Mnaona? Sio jalalani, bali "bondeni," tunafundishwa. Huko chini bondeni, mwajua, huko ndiko Yungiyungi hukulia, pia, mwajua. A-ha. A-ha. Hiyo ni kweli, mnaona, "Bondeni." Vema. Nyingine zikaanguka kwenye bonde la mateso, mateso makali. Baadhi ya hizo Mbegu zikaanguka mle ndani, bonde la mateso, mateso makali, wakaitwa kila kitu kama Yungiyungi alivyoitwa, "Beelizebuli," akadhihakiwa.

325 Lakini kwenye bonde hili kuna mito ya maji. Zaburi 1, ilisema, "Heri mtu yule." Hebu nilisome tu. Hebu nionyeshe yaliyo kwenye bonde hili. Nini, Zaburi . . . Nilidhani nisingekuwa na wakati, bali tutachukua tu wakati, mnaona, kusoma hili, mnaona, kupata hili hapa. Tutasoma hili tuone mtu huyu ni nani hapa chini, ambaye yuko tu mahali alipopandwa. Kama amepandwa juu ya . . . huko juu penye mwamba wa jangwani uliojaa mavumbi, ambako hakuna udongo hata kidogo, ama amepandwa bondeni? Vema.

Heri mtu yule asiyekwenda katika shauri, hekima . . .

Amina! Amina! Amina! Amina!

. . . *asiyekwenda katika shauri la wasio haki,* . . . *kusimama katika njia ya wakosaji,* . . . *kuketi barazani* pamoja *na wenye mizaha.*

Bali sheria ya B*WANA* *ndiyo impendezayo,* Neno; *na katika sheria,* Neno, yeye *huitafakari mchana na usiku.*

Naye atakuwa kama mti uliopandwa kandokando ya vijito vya maji, . . .

326 "Vijito." Ni kitu gani hicho? Zile karama tisa za kiroho. Vijito vingi vya "Maji" mamoja, Roho mmoja. Maji mamoja, bali yakitoka katika asili tisa mbalimbali, vijito vya Maji. Mnaona?

. . . *vijito vya maji, uzaao tunda lake,* tunda la Roho, *kwa majira yake. Wala* majani *yake hayanyauki; na kila* alitendalo, hilo *litafanikiwa.*

327 Mnaona, nyingine zilianguka chini katika bonde hilo pale, ilipo mito hii. Na kutoa . . . Mliona? Ninataka kupata kitu kingine. Zilifanyaje? Zilianguka chini, mtoni . . .

328 Hazikuwa zimewekwa. Atakuwa kama mti "uliowekwa, ukatolewa kwenye *hili* hadi kwenye *lile*"? Yeye "alipandwa."

Nini? Kukusudiwa tangu zamani. Wazo lile la Mungu, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, lilimweka pale. Mnaona? Sio kuchomelewa, si kwa bahati; bali "alipandwa," kukusudiwa (nini?) katika mito ya Maji. Loo!

329 "Shina lake halitanyauka." Loo, haleluya! "Ajapokufa, nitamfufua tena katika siku za mwisho." Hiyo ni kweli.

330 Yeye amekusudiwa tangu zamani kuwa Pale, sio tu kwa bahati. Yeye alikusudiwa tangu zamani kulishika Neno hilo wakati lilipopandwa. Naye atakuwa pale pale. Inaponata, yeye yuko pale. Amepandwa, sio tu kuchomelewa chini. Kwa kweli amepandwa. Hiyo ni kweli. Tofauti kubwa: kuchomelea kijiti chini, na kupanda kitu fulani. Ni tofauti. Mbegu ilipandwa; ikapata mashimo Yake yenyewe ya mizizi. Wakati maji yanapoanza kuingia na kuuvunjilia mbali Uhai wake, Roho, unaanza kusema . . .

Unasema, "Kuna karama tisa za kiroho."

Yeye akasema, "Amina."

"Yesu, yeye yule jana na hata milele."

"Amina."

"Angali anaponya jinsi tu Yeye alivyofanya daima."

"Amina. Amina. Amina." Mnaona?

331 Yeye amepandwa kandokando ya mito, mito inayotoka kila upande, mito ya Maji. Si ajabu yeye hawezi kunyauka. Si ajabu, yeye amepandwa. Nyingine za hizo Mbegu zilianguka huko. Hawezi kufa. Yuko moja kwa moja kwenye kijito cha Uzima. Anaendelea kuzaa. Hiyo ni kweli. Anatoa Uhai wake kwenye mito hiyo, "mito," Agano Jipya, Agano la Kale. Amina. Analishwa tu, kote kote! Loo, ndugu!

Mtampenda? Amina!
Mtamsifu? Amina!
Mtamwabudu? Amina!
Amina! Amina!

332 Naam, bwana. Naam, bwana. Loo, ninaupenda huo, nanyi je? Naam.

. . . huzaa yake, huzaa matunda *yake kwa majira yake;* . . .

333 Mwanzo 1:11. "Kuzaa matunda yake." Matunda gani? Matunda ya nini? Matunda Yake. Matunda gani? Matunda Yake Mwenyewe. Ni tunda lipi? Biblia. Mnaona? Yote yapo hapa. Tunda, upendo, upo hapa katika Biblia. Furaha, hapa katika Biblia. Nguvu, Roho Mtakatifu, mambo haya yote hapa, uponyaji wa Kiungu, ahadi za Mungu, hayo ndiyo matunda. Haya *hapa*. Basi endapo amepandwa katika Hili, hii imepandwa katika u— udongo mzuri, katika imani. Imani inafanya nini? Imani inaanza kumfanya Huyo akue.

Amina!

Inaanza kumpandisha juu. Mnaona? Jambo ndilo hilo; humpandisha juu. Hakika. "Atakuwa kama mti uliopandwa kandokando ya maji; unaozaa matunda yake kwa majira yake."

334 Sasa, itazaa tunda la aina gani? Yohana 14:11, Yohana 14:11, Yeye alisema, Yesu alisema, "Yeye," ninaamini ni 14:12, "Yeye," Yesu alisema, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya." Kwa nini? Neno lile lile liko ndani yake. Yeye alikuwa Neno. Hiyo ni kweli? "Basi mkikaa ndani Yangu, na Maneno Yangu ndani yenu, ombeni mtakalo."

335 Nilikuwa nikizungumza na Ndugu Evans kule nyuma, sio muda mrefu uliopita. Yeye alikuja hapa juu. Yeye huendesha gari mbali sana! Alilipoteza gari lake. Aliketi kule kwa Miller's, akaacha ufunguo ndani, mtu fulani akaja na kuliiba. Alikuwa na kila kitu alichokuwa nacho, ndani yake. Akaja. Yeye, yeye na Ndugu Fred, na Ndugu Tom, baadhi yao, wakaja nyumbani. Wakasema . . . Vema, alionekana kama mtoto mdogo aliyenyang'anywa peremende yake; yeye, amevurugika kabisa, mwajua. Akasema, "Kamwe sijui la kufanya." Nikasema, "Vema, . . ."

336 Sasa ni kitu gani? Sasa, wao wanakuja, jambo la kwanza ni gani? Kwenye Neno; kumwomba Baba. "Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu likae ndani yenu, ombeni mtakalo." Ati nini? Dumu na Neno, dumu tu moja kwa moja na Neno.

337 Nikasema, "Hebu tuombe." Tukainama sakafuni, nasi tukaanza, kuomba.

338 Basi wakati tukiwa pale, tulikuwa tukiomba, nikasema, "Baba, naja Kwako, katika Jina la Bwana Yesu. Huyu hapa ndugu ambaye hutumia, anafanya kazi siku chache tu kwa juma. Mikono yake, yote imeparuza, kutokana na kutengeneza magari yaliyoharibika na vitu kama hivyo, apate pesa za kutosha kuendesha maili elfu moja mia nne hadi mia tano kila Jumapili, apate kuja mikutanoni. Yuna lundo la watoto wa kulisha. Inamgharimu yapata, yapata dola hamsini ama sabini kwa juma, kufanya safari hiyo, apate tu kuja kanisani. Unaona? Kweli. Yeye amekuja hapa, akijaribu kulisikia Neno, tunapojaribu kujitahidi kulishindania." Kisha nikasema, "Sasa, mtu fulani mwovu amemwibia gari lake." Ilikuwa ni kitu gani? Nikasema, "Sasa, Bwana, ninakuomba Wewe, umrudishie gari lake, katika Jina la Yesu Kristo."

339 Nilifanya nini? Nililiweka Neno hilo, ahadi hiyo, mbele za Mungu, nikaitia muhuri kwa Jina la Yesu, na kulituma hilo Neno. Moja kwa moja likashuka barabarani, huko mbali sana, likapata mahali ilipoanzia; kama vile mbwa mwindaji anavyoufuatilia mburuzo wa sungura. Mnaona? Huyu hapa Yeye akaja, akishuka kwenda barabarani, akitoa mlio mkali. Akafika

kule chini, yapata tu nusu ya safari kufika Bowling Green, Kentucky. Ni kitu gani kilivunjika? Neno likampata.

340 Papo hapo ono likarudi upesi. Nikamwona mtu, mwenye shati lililoonekana la manjano, akiendesha motokaa, jamaa mdogo, wakati mmoja alikuwa ni Mkristo. Neno likamgusa. "Unafanya makosa." Neno likamshika. Yeye akalituma Neno Lake, mnaona, mnaona, na kumshika. "Utashikwa kwenye hiki, siku moja, nayo sheria itakushika kwa kufanya jambo hili. Geuka ukalirudishe." Neno likamshika. Wakati mmoja alikuwa ni Mkristo. Nikamwona akilileta hapa juu, akaliegesha kando ya barabara.

341 Nikasema, "Sasa, ndugu, shikeni njia tu mwende, njia fulani *hapa*, mtalipata gari lenu. Ngojeni hapa kidogo, hata hivyo, mpaka atakapolirudisha. Sasa, si ulikuwa na tangi lililojaa petroli?"

"Naam," akasema.

342 Nikasema, "Hapatakuwa na chochote kilichoguswa. Ila litakuwa na nusu ya hiyo petroli, maana limekunywa nusu yake, kuendesha. Alikuwa yapata katikati ya Bowling Green, yapata—ilitumiwa kwa yapata maili mia moja."

343 Wakati alipolipata, hivyo ndivyo lilivyokuwa, vivyo hivyo hasa. Ilikuwa ni kitu gani? Neno lilienda likamshika.

344 Akarudi akasema, sio muda mrefu baada ya hapo, mtu fulani akanunua gari kutoka kwake. Akaponyoka wala hakulilipia. Mnaona? Kasema, "Ndugu Branham . . . "

345 Nikawaza, "Maskini mtu huyu!" Alikuwa na deni yake dola mia nne. Nikasema, "Ninaomba." Nikalituma Neno. Neno likaenda, likafika njiani mwake, likampata.

346 Wakati, tukashuka kwenda kumtafuta mtu huyo. Yeye, kamwe hajapata kuwa Mkristo, mnaona, alikuwa—alikuwa . . . Yeye alicheka. Walimwomba, aende kanisani, wakati mmoja. Akasema, "Vema, wakati mhubiri akihubiri, nitawaangalia warembo wenye nywele za shaba." Kwa hiyo, mnaona, huwezi kupata . . . Naam. Huyo ni—huyo ni—huyo ni ibilisi, huyo ni, mnaona. Kwa hiyo Neno lisingeweza kumshikilia.

347 Neno lilifanya nini? Lilimfuatilia kwa jicho. Mnaona? Usininii tu . . . Ndugu Welch aliendelea tu kushikilia, kasema, "Itakuwa sawa. Itakuwa sawa." Neno likamfuatilia. Mnaona? "Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu likae ndani yenu, ombeni mtakalo." Mnaona? Neno likamfuatilia.

348 Muda si muda mwajua, mmoja wa wavulana wake alikuwa akiendesha gari, hapa chini barabarani, nalo hilo hapo. Akamwona mtu huyo kwenye hilo gari, akachukua namba yake, akageuka, akageuka na kuingia, kwa Ndugu Wood. Wakaipiga, waone ilikuwa wapi. Yeye alikuwa Bowling Green.

349 Mungu Mbinguni anajua, sikusikia neno moja kulihusu, sikujua lolote kulihusu.

350 Jumapili iliyopita, ilikuwa ni juma moja lililopita, alasiri, tulipomaliza kuhubiri hapa, nikaenda kule na kubadilisha nguo zangu, nakajiandaa kwenda Florida, kwa ajili ya . . . ama chini . . . Ndugu Welch, kwa ajili ya mkutano usiku huo unaofuata. Nilipoingia kwenye gari, nikamwona mtu huyo. Nikasema, "Ndugu Welch . . . " Nisingeweza kumwambia, sasa. Hana budi kuchukua hatua, yeye mwenyewe, mnaona, kama tu vile ilivyombidi Meda kufanya uamuzi wake pale. Mnaona? Nikasema, "Tutapitia Bowling Green."

Akasema, "Hiyo ni yapata maili thelathini nje ya njia."

351 Tukashuka kwenda barabarani. Nikawazia, "Loo, yeye—yeye, ata—atalipata. Mnaona? Atalipata. Mnaona? Hana budi tu kulipata."

352 Tukashuka. Mimi na Dada Evans . . . Basi baada ya kitambo kidogo, akasema, "Wajua, Ndugu Branham," akasema, "Hivi nimekuwa mpumbavu hivi?" Kasema, "Ulisema Bowling Green, muda mfupi uliopita."

"Naam."

353 Akasema, "Unamjua yule mtu aliyechukua pesa zangu, aliyetoroka nazo?"

"Ndiyo."

354 Kasema, "Yuko Bowling Green. Nimekuwa nikiwazia hilo. Ninii tu . . . Nina kitu hapa. Nitakifungua, nitafute mahali alipo. Ndipo nitafungua . . . " Nikasema . . .

355 Kasema, "Ungefanya nini? Utaenda kule chini, ukazichukue pesa zako?"

356 Sasa, mnaona, kama nikimwambia, basi . . . Mnaona, yeye ana jambo la kufanya, yeye mwenyewe. Mnaona? Analo jambo la kufanya. Nisingeweza kumwambia. Kama ningalimwambia, lingelivunja lile ono papo hapo. Mnaona? Kwa hiyo ilinibidi kuacha . . . Mnaona? Kama tu vile . . .

357 Kwa nini Yesu alisimama pale, kamwambia Mariamu na Martha, "Liondoeni lile jiwe"? Mbona, Yeye alikuwa ni Mungu. Angaliweza kusema, "Ewe jiwe, usiwepo tena," nalo lisingalikuwapo pale. Lakini alikuwa na jambo la kufanya.

358 Kwa nini Yeye alisimama pale, akaangalia mavuno? Mnaamini Yeye alikuwa ndiye Bwana wa mavuno? Aliwaambia wanafunzi Wake, "Ombeni Bwana wa mavuno, kwamba atawatuma wafanyakazi kwenye mavuno Yake." Kwa maneno mengine, "Ninyi niombeni Mimi nifanye yale ninayoenda kufanya." Mnaona?

359 Sisi ni marafiki. Sisi ni—sisi ni . . . Ni Kanisa. Tuna jambo la kufanya, sisi wenyewe. Unalo jambo la kufanya. Hii hapa Injili,

ninaijua Hiyo, bali kama mkiketi tu hapa wala hamwihubiri, itafaa nini? Mnaona? Mnalo jambo la kufanya. Inawapasa kutia juhudi. Hamna . . . Unasema, “Vema, ninaamini kwamba Mungu anaweza kuponya, ila tu sijui.” Simama na hebu Neno hilo liwe neno lako. Liamini. Usilitolee hoja; liamini tu.

360 Nikasema, “Vema . . . ” Nilijua, kama hakuenda, alikuwa anaenda kuzipoteza. Nikasema, “Kama ingalikuwa ni mimi, kama ingalikuwa ni mimi, ningeenda nikachukue fedha zangu sasa hivi.” Naye akafanya hivyo. Wakati alipomwamsha mtu huyo kitandani, alikuwa na pesa kiasi. Akampigia tu simu jirani yake, akapata hizo zingine, akalipa.

361 Ni kitu gani? Ni Neno. Mnaona, kama Hilo linaweza kupata mahali pake, linaweza kugeuka. Sasa, jambo lile lile juu ya uponyaji wa Kiungu.

362 Sasa, vipi kama Ndugu Welch angalisema, “Vema, sidhani nitashuka niende; nafikiri nitapitia tu njia ile nyingine.” Vipi kama jamaa huyo alisema, “Vema, siendi kule ambako lile gari haliko”? Mnaona? Halitatukia.

363 Lakini inakubidi kuamini. Huna budi kuliamini. Na hilo ni . . . Basi hilo linaangukia katika mazingira ya imani, nalo halina budi kuleta hiyo. Halina budi kuileta. Loo, hilo ni . . .

364 Hivi uliwahi kuwazia kuhusu, wakati mtu fulani alipofufuliwa kutoka kwa wafu, kile kinachotukia? Hivi ulipata kuwazia, huko Finland kule, ule wakati yule mvulana mdogo alipofufuliwa katika wafu? Roho yake ilikuwa imemtoka. Sasa, Neno halina budi kwenda, kupitia anga lisilo na mwisho huko ng’ambo, na kuichukua maskini nafsi hiyo na kuirudisha moja kwa moja. Linawezaje kufanya hivyo? Hilo ni Neno, “Waponyeni wagonjwa. Wafufueni wafu.” Mnaona? Yeye atafanyaje hilo? Halina budi kuja kwa Neno lililotiwa maji. Yeye alikuwa ameonyesha ono, nalo halina budi kutukia. Huyo hapo yule mvulana amelala. Hapo kila kitu kimewekwa jinsi Yeye alivyokuwa amesema, miaka miwili hapo kabla. Nayo hiyo hapo. Hiyo ndiyo sababu ninasema kumhusu yule dubu akishuka kilimani, hata iwe ni nini: halina budi kutukia, halina budi kuwa tu hivyo. Mnaona? Lingefanya nini? Neno!

365 Nikasema, “Baba wa Mbinguni, huko kwenye nchi za uenyeji wetu, Wewe uliniambia, yapata miaka miwili iliyopita, kwamba mvulana huyu mdogo angefufuka kutoka kwa wafu. Kwa hiyo, juu ya msingi wa Neno Lako, ahadi Yako. Kwanza, Neno lilisema, ‘Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.’ Uliwatuma wanafunzi Wako mbele, Wewe, ukawaambia ‘mkawaponye wagonjwa, mkawafufue wafu, mkawatoe pepo.’ Halafu, kwa ono, Wewe ulinionyesha mimi kwenye nchi ya uenyeji wangu kwamba mvulana huyu mdogo . . . atafufuka kuwa hai tena.”

366 “Kwa hiyo, ewe mauti, huwezi kumshikilia tena. Ninalo Neno la Bwana.”

367 Sio mimi; mimi siye Neno. Yeye ndiye Neno. Mnaona? Kama ningalikuwa Neno . . . Kunaye Mtu Mmoja tu angaliweza kuwa Neno, huyo alikuwa ni Yesu. Yeye alikuwa ni Neno la Mungu lililonenwa, kwa kuzaliwa na bikira. Mimi ni upotovu, mnaona, mimi—mimi ni matokeo ya muungano kati ya baba yangu na mama. *Huu* hauna budi kufa; *huu* ni mimi, mnaona, mwili ambao hauna budi kufa.

368 Haikuwa hivyo, kwa Yesu. Yeye alikuwa ni Neno. Alizaliwa, bikira. Ndugu, hakuna mwanamke, mwanamume, ama chochote kingine, aliyekuwa na uhusiano wowote na Yeye. Huyo mwanamke alikuwa ni kiangulio, hiyo ni kweli, na Yeye aliyanyonya maziwa yake, na kadhalika. Huenda hilo lilikuwa ni kweli huhusu hilo. Lakini, hebu nikwambie, Yeye alikuwa ni Mungu. Huyo Ndiye Yeye alikuwa. Hapakuwapo na kujuana kimwili juu yake, hata kidogo. Ilibidi awe huru na kujuana kimwili, apate kuleta Uhai kupitia kwenye ile Damu; kama tutakavyolifikia, katika dakika chache. Na basi, angalieni, Yeye alikuwa ni Neno.

369 "Lakini Neno la Bwana . . . " Manabii hawakuwa ni Neno. "Bali Neno la Bwana *liliwajia* manabii." Sio . . . Hao hawakuwa ni Neno. Neno *liliwajia*.

370 Hivyo ndivyo linavyotufanyia siku hizi. Wakati Neno lilipokuja kwa ajili ya mvulana huyo mdogo, ilikuwa ni nini? Ono. Ilikuwa ni nini kwa yule dubu? Ilikuwa nini kwa vitu hivi vingine? Vyote, ono. Ni Neno la Bwana, lilikuja kwake. Ndipo linafanya nini? Linashikilia pale.

371 Sasa, halina budi kunenwa, kwanza. "Ewe mauti, mrudishe. Katika Jina la Yesu Kristo, ninalituma hilo Neno mbele." Linashika, kama tu lilivyomshika mvulana yule akishuka kwenda hapa chini kwenye Bowling Green, akiwa na lile gari lililoibiwa. Hili hapa linaenda *huku* na kushika tena. Linafanya nini? Linaishika maskini ile—ile roho, linairudisha papa hapa, na kuikabidhi ule mwili, kama tu vile Neno lilisema lingefanya. Hiyo hapo. Inafanya nini? Imani, sio maarifa.

372 Unasema, "Sasa hebu tuone. Hewa imefanyizwa kwa *ninii na ninii*. Kuna kiasi fulani cha asidi. Kuna kiasi fulani cha gesi. Kuna kiasi fulani cha nurulimwengu. Ninaweza kuwazia hilo. Na labda kama mimi . . . " Loo, una—una . . . Unajipumbaza na wakati.

373 Sio hekima; imani! Sio hekima; itakwambia hilo haliwezi kutendeka. Imani inathibitisha limefanywa, mnaona, hiyo ni kweli, inaonyesha Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Vema.

Hebu tuharakishe sasa. Inatubidi kuharakisha.

374 "Unazaa matunda kwa jinsi Yake." Yohana 14 inasema, kwamba, "Yeye azifanye ninii Zangu . . . Yeye aniaminiye Mimi, kazi, ishara nizifanyazo . . . "

Sasa, mnasema, "Hizo ndizo ishara Yeye afanyazo?"

375 Yeye aliingia kwenye nyumba moja ambamo maskini msichana mdogo, binti wa pekee wa mhudumu mmoja, alikuwa amelala; amekufa, baridi, amekwajuka, amelazwa mle. Labda alikuwa amekufa saa kadhaa kabla Yeye hajafika pale. Walikuwa wamemlaza kwenye kitanda kidogo, wakijiandaa kumchukua, wakamtie dawa asioze. Yesu anaingia moja kwa moja chumbani mahali alimokuwa, namna hiyo. Walikuwa wakiomboleza na kulia namna hiyo. Akawatoa wote nje, kasema, "Tokeni hapa. Tokeni." Kasema, "Njoni hapa, Petro, Yakobo, na Yohana. Ninajua mnaamini." Kamwambia baba, "Unaamini, la sivyo usingenitafuta Mimi."

Naye mama akasema, "Bwana, ninaamini." Mnaona?

Kasema, "Simameni hapa."

376 Akaangalia. Huko nje alisimama msichana mdogo—mdogo. Kasema, "Talitha," hiyo ni kusema, "msichana mdogo." Haleluya! Haikumlazimu kuomba. Yeye alikuwa ni Neno. Aa-ha.

377 Hainilazimu kuomba, iwapo ninaweza kuona ono, maana Neno tayari limefanywa tayari. Inanibidi kuomba, kulipata Neno, kupata yale Mungu asemayo. Ndipo ninaweza kulinena Hilo, nikiisha kupata alilosema Yeye.

378 Lakini Yeye alikuwa ni Neno. Amina. "Msichana mdogo, nakwambia, simama." Akamwinua, kwa mkono. Jambo ndilo hilo. Mnaona? Loo, jamani!

379 Hilo ni dhihirisho. "Huzaa kwa jinsi yake." Yesu alisema, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya."

380 Kwa hiyo, haya, mnaona, mambo haya yote ya madhehebu haya na kadhalika, wanayo mambo hayo katika mkusanyiko wa vinyaa na dhambi, kama tu vile tumbo la duniani lilivyo nayo maumbile. Hiyo ni kweli. Loo, jamani! Linawezaje kutukia? Neno la kweli la Mungu linawezaje kukua kwenye hawa wa kujiunga na kanisa wenye hizi nywele zilizokatwa, wanaovaa kaptura, wanaovuta sigara, wadoezi wa uwanja wa mchezo wa tufe? Linawezaje kufanya hivyo, wakati umati kama huo unaopenda na kutafuta anasa, unadoea huko na kuyapenda mambo kama hayo, na kuupenda ulimwengu? Upendo wa Mungu unawezaje kuingia? Mbegu ya Mungu inawezaje kukua kwenye ardhi kama hiyo? Kamwe haitashika mizizi. Kamwe haitaleta Uzima wowote kwake. Itakaa hapo penye maskini mawe hayo ya kimadhehebu yaliyojaa mavumbi na kuoza kabisa, lakini kamwe haitaleta Uzima. Naam, bwana. Naam, bwana.

381 Watafuta anasa, "Wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu." Ni la kuchukiza mno! Hata hivyo, ni werevu. Hao ni werevu maradufu kama—kama tabaka hilo jingine. Hakika.

Werevu, wenye elimu, watafuta hekima, kama tu Hawa alivyokuwa, nao wana kipimo kile kile yeye alichokuwa nacho, hasa kabisa. Ni Kweli.

382 Yungiyungi ingewezaje kuishi, Mbegu ya yungiyungi iishi na kukua, wakati inapostawi majini, kukua kwenye moja ya madhehebu hayo yenye vumbi? Ingefanyaje jambo hilo, wakati yenyewe hustawi Majini. Maji ni Roho. “Wana mfano wa utauwa, lakini wanakana nguvu za Roho.” Mnaona? Ingawa Neno huwaangukia, haliwezi kukua. Haliwezi kukua. Kama tu vile Neno lilivyokuwa juu ya Hawa, bali lisingeweza kukua. Kwa nini? Yeye aliikubali hekima, hekima ya Shetani. Neno linawajia. Neno linawaangukia. Hakika, linawaangukia. Naam, bwana. Linakua . . . Hilo, Hilo litawaangukia. Wanaweza kulisikia Neno likihubiriwa.

383 Hivi uliwahi kuwaona watu wameketi kanisani, kamwe hawatapiga hatua? Ukiwahubiria wanawake juu ya kukata nywele; mwaka baada ya mwaka, inapita, wangali wamekata nywele. Ukizungumza na wanaume juu ya kuvuta sigara, wanawake kuhusu kunywa pombe; wanaendelea kunywa vile vile, vivyo hivyo tu. Ni kama tu kumwaga maji juu ya mgongo wa bata. Halina mahali pa kukulia. Mnaona? Ni maskini kule kutafuta anasa, umaarufu, “Vema, acha hao wanawake wengine wafanye hivyo kwanza, kisha nitalifanya.” Sijali wafanyalo. Ni jukumu lako kulifuata Neno la Mungu. Hiyo ni kweli. Mnaona?

384 Ingawa Neno linawaangukia, haliwezi kukua. Hekima ya shetani, mnaona, kwa hiyo linakuwa tu ni mavumbi ya kimadhehebu. Hawawezi kuamini Waebrania 13:8, wote wamejaa kiburi cha hiyo hekima, hakuna kitu kwa ajili ya Hilo kukulia. Mnaona? Wanawezaje kuamini Waebrania 13:8, “Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele”? Wasingeweza kuamini. Mnaona?

385 Loo, wao wanasema wanaliamini Hilo. Loo, ukiwaambia Hilo, wanasema, “Hakika, tunaliamini Hilo.” Basi nionyesheni matunda yake. Hebu niyaone. Hebu nione likitendwa. Hebu nione kanisa ambalo unahubiria, likifanya yale waliyofanya katika Kanisa la kwanza la kimitume basi, lililoamini Neno.

386 Mnayavuruga mabatizo yenu. Mnayavuruga mathibitisho yenu. Mnalifanya liendane na namna fulani ya kanuni za imani; badala ya kulichukua Neno, kuliacha Neno lizae tunda Lake lenyewe. Mnabuni namna fulani ya kitu mnachopaswa kufanya, kujiletea thibitisho Lake. Naye Shetani anaweza kufasiri kila thibitisho unalotaka kutoa. Hakika, anaweza, hakika anaweza. Bali hawezi kulileta Neno. Hicho ndicho kitu kimoja kinachomchoma moto. Kamwe hawezi kufanya hivyo. Naam, bwana. Loo, naam.

387 Sasa waangalieni Kaini na Habili. Wote wawili walikuwa ni waaminifu. Kaini alichukua, kwa hekima yake, iliyotokana

na kanisa la mama yake, Hawa. Huyo alikuwa mama yake. Ni wangapi wanaojua ya kwamba Hawa alikuwa ni mama wa Kaini? Hakika. Vema. Kama mama yake, alichukua kutoa hoja, mnaona, hekima, hekima yake mwenyewe. Dhabihu ya kupendeza; alikuwa na maua. Alikuwa na tunda la kondeni. Kasema, "Vema, sasa, hakika, mnaona," akasema, "Mungu . . ." Ilikuwa ni kama tu vile Shetani alivyo—alivyomwambia Hawa, "Hakika, hakika . . ." "Hakika Mungu ataipokea dhabihu yangu. Nilijenga madhabahu ya kupendeza. Nimeyafanya maridadi sana. Yamepambwa kwelikweli."

388 Kama tu vile Pasaka hii itakavyokuwa, watatumia mamilioni ya dola, kote nchini, kuweka maua ya Pasaka juu ya madhabahu fulani. Madhabahu hayakufanywa kwa ajili ya maua; ni kwa ajili ya dhabihu. Mnaona? Inaonyesha tu ile roho ya kale ya Kaini, mnaona, ibilisi yeye yule wa kale—wa kale kutoka Edeni. Mnaona?

389 I—ilikuwaje? Kaini aliwazia, "Hakika . . ." Mnajua mtu huyo alikuwa ni mwaminifu, maana ilimaanisha Uzima ama mauti, kwake.

390 Na, hao watu, msifikiri ni wanafiki. Wao ni waaminifu. Mnasema, "Basi, wangeweza kuwa waaminifu na wawe makosani?" Hakika. Mtu anaweza kunywa aseniki, kwa uaminifu akifikiri anakunywa mafuta ya mbarika ama kitu fulani, kitu kingine. Mnaona? Mwaminifu; hilo halitoshi. Ni Ukweli, sio uaminifu. Ukweli!

391 Hao wanawake huko Afrika, wanawatoa dhabihu watoto wao wachanga kwa miungu, mamba. Ninyi ni waaminifu hivyo? La. Ni wangapi wao wanasimama, hao Wachina, wanavunja mifupa yao, kwa ajili ya miungu ya jikoni! Na vipi kuhusu Waislamu na huko juu, na wanaotembea juu ya moto? Na kuweka vitu, loo, ndoana miilini, kinywani mwao, na kushona kinywa chao.

392 Na baadhi yao wanachomelea kijiti . . . Ninayo sanamu pale juu, sanamu ndogo, jinsi anavyotoa dhabihu kwa mungu wake, kuwazia angeenda Mbinguni. Kuhani hutia kijiti kinywani mwake, anakifunga kichwani mwake, kwa mnyororo; anashuka chini, anaweka mikono yake nyuma yake, anaifunga miguu yake kwa mnyororo. Hawezi kunywa, kuzungumza, kula, wala chochote kingine, hata atakapokufa.

393 Umemwona Mkristo yeyote akitoa dhabihu namna hiyo? Hata hutaiamini ile Kweli, Neno. Unaona?

394 Sasa, "Urembo," yeye alisema, "hakika Mungu ataipokea. Angalia jinsi madhabahu yangu yalivyo maridadi."

395 Mnaona roho iyo hiyo siku hizi, ya hekima? "Vema, kama tukilijenga dhehebu hili kubwa, hakika Mungu atatupokea." Yeye hatapokea chochote ila Neno Lake. La. Mnaona?

396 "Vema," wao wanasema, "sasa, angalia, Ndugu Branham, kama sisi—kama tukiwatoa wahudumu *kadhaa* kila mwaka. Mpango wetu wa kimishenari, mwaka jana, ulikuwa ni wa zaidi ya dola laki moja." Hilo linaweza likawa ni zuri sana, ndugu, bali umekufa mpaka ulikubali hilo Neno na ulijie. Hiyo ni hakika.

397 "Mbona, Ndugu Branham, kanisa letu! Unafikiri wewe ni nini, maskini akili finyu tu huko chini?"

398 Hiyo ni kweli. Sasa, hiyo ni kweli kabisa. Hiyo ni kweli. Lakini, chochote nilicho, acha nidumu na hilo Neno. Litakua liwe kitu fulani, siku moja. Mnaona? Dumuni tu na hilo Neno, haidhuru ni nini. Hatuna kitu ila maskini maskani hii hapa. Hiyo ni kadiri tunavyohitaji, kwenye wakati uu huu wa sasa, mahali tu pa kuketi, maana tunamtazamia Yesu kuja.

399 Hatutaki dhehebu lolote kubwa itubidi kutumia mamilioni kila mwaka, kwenye mijengo na vitu kama hivyo; nao watu wakijaribu kulihubiri Neno, wakiteseka huko nje, bila chakula, na mambo kama hayo. Watu wana shida gani? Hiyo si ni . . . Loo, inaonekana kana kwamba watu wangeweza kuamka.

400 Lakini, mtu yeyote angaliweza kuukubali Ukatoliki, angeweza kuwa kipofu kutosha kukubali chochote. Nitawaambieni Ukweli. Mtu yeyote angaliliacha hilo literemke shingoni mwao, angeweza—angeweza . . . "Ati watu wenye hekima," si ajabu, Biblia ilisema, "hata wafalme wa dunia walifanya uzinzi pamoja naye." Nao wenye hekima, maarifa, mnaona, nao wanafaulu, hao makasisi, watu wenye akili. Loo, jamani, unanena kuhusu walioelimika? Jamani, inawabidi kuwa na miaka, baada ya miaka, baada ya miaka, baada ya miaka.

401 Wao wanasema hawaishi na hao watawa. Basi ninataka kuwaulizeni jambo fulani. Kwa nini wasiwe tasa basi? A-ha. A-ha. A-ha. "Hao ndio Bibi-arusi, hao hapo. Watawa ndio Bibi-arusi. Nao hao ni Bwana Arusi, hakika, mnaona." Hiyo ni kweli. Mama Mkuu huwakaba roho hao watoto wachanga na kuwazamisha kwenye mashimo ya chokaa. Hamwamini hilo? Msikilize yule halisi, amekuwa mle, akishuhudia hilo. Kasema, "Sasa haya basi, hebu sheria inikamate."

402 Kisha kasema, "Tutafanya jambo lile lile walilofanya Urusi, jambo lile lile lililofanywa Meksiko. Tutakilipulia mbali kitu hicho kiwe wazi, kitakapoifikia serikali."

403 Lakini mtalifanyaje sasa wakati tuna kichwa chake mle mle ndani ya serikali? Mnaona? Mnaona? Hiyo ni kwamba hilo Neno halina budi kutimizwa, "Walifanya sanamu hapa, kwa huyo mnyama aliyewekwa pale. Nao wote wawili walizungumza pamoja na kumpa nguvu huyu mnyama, azungumze." Loo, ndugu, Neno hilo litasimama papo hapo. Sio ukomunisti utakaochukua mamlaka, bali Urumi utachukua. A-ha.

404 Sasa angalieni hapa kwenye hili. Kaini alisema, "Hakika Yeye atapokea dhabihu yangu." Lakini ya aina gani? Yeye

alisema, "Nilitoa dhabihu." Lakini ilikuwa ni dhabihu ya namna gani? Uhai wa mimea: mimea, maua, mboga. Uhai wa mimea, (kitu gani?) hakuna mateso kwake, hakuna adhabu.

405 Watu hawataki kuteseka. Hiyo ndiyo shida siku hizi. Wanakuja, watakuja sasa hivi na kuliamini hili Neno, kama haikuwabidi kutoka kanisani mwao, kama haikuwabidi kuchekwa, kudhihakiwa. La. Wanataka uhai wa mimea, namna fulani ya hekima. "Vema, maisha *haya* ni mazuri tu kama Yale." Siyo. Nitawaonyesha mahali hilo linapotoka, katika dakika moja tu, Bwana akipenda.

Lakini, "Habili, kwa imani." Utukufu!

406 Kaini, kwa hekima, alisema, "Hakika Mungu atalikubali hili. Haya hapa madhabahu. Ninalo kanisa." Hivyo ndivyo kanisa lilivyo, madhabahu, mahali pa kuabudia. Vema. "Nina madhabahu. Nitaabudu kwa uaminifu tu kama ndugu yangu. Nami nina kitu fulani cha kupendeza hapa kwa ajili yake. Hakika Mungu atakipokea." Hilo ni jambo lile lile ibilisi alilomwambia mama yake; uongo ule ule, hekima.

407 Sasa, Habili. Waebrania 11 ilisema:

> *Kwa imani Habili alimtolea Mungu dhabihu iliyo bora kuliko* ile ya *Kaini,* . . . *ijapokuwa amekufa,* bado ilinena.

408 Mnaona? "Habili . . . " Kwa nini? Hekima? Kwa thiolojia? "Kwa imani alimtolea Mungu dhabihu iliyo bora." Kwa imani katika nini? Kwa imani katika nini? Kwa . . . Yeye alikuwa na imani yake wapi?

409 Hapo, baba na mama yake tu, yeye na ndugu yake wa kambo, ingewezekanaje kwa vyovyote vile? Yeye angeweza—yeye angeweza kuipata wapi? Yeye alikuwa na imani katika nini? Imani katika mimea, imani katika *hii*? La, bwana. Yeye alikuwa na imani katika Neno. Maana, yeye alitaka kujua ni kwa nini alikuwa nje ya bustani hiyo. "Kwa nini tukatolewa nje?"

410 Mama angelazimika kusema, "Kwa sababu niliusikiliza uongo wa ibilisi. Kwa sababu mvulana *huyu* hapa alizaliwa *hivi na hivi*, hiyo ndiyo sababu Mungu alitufukuza."

411 "Vema," akasema, "hata siwezi kulikaribia lile lango. Kunaye Kerubi pale, mwenye upanga, akiulinda huo Mti wa Uzima." Kwa hiyo, kwa imani!

412 Mnaona, kwa hekima, Kaini alimtolea, mwajua, kwa kutokulijua Neno, bali wazo tu, kwa hekima. Alifanya mahali pazuri, na kupafanya pazuri na pa kupendeza.

413 Lakini, "Habili," hakuna mtu aliyemwambia, sasa, mvulana tu, "kwa imani aliona kwamba haikuwa ni uhai wa mimea; ilikuwa ni tendo la kujuana kimwili, kwa damu." Haya basi, ndugu. Pitia juu ya Hilo, wakati mmoja.

414 Kwa imani watoto Wake wangali wanaliona. Yeye kamwe hakulifundisha kwa hekima fulani sasa. Haliji kwa hekima. Linakuja kwa imani. Biblia ilisema, “Habili, kwa imani.”

Yeye alitoa nini? Damu, kutoka kwa maisha yaliyo hai, uhai wa mnyama.

415 Sisi ni mnyama, sisi wenyewe. Sisi ni mnyama mwenye damu moto. Hiyo ni kweli kabisa. Spishi ya juu, mnyama wa hadhi ya juu kuliko wote, bali akiwa na nafsi mle ndani. Hayo ndiyo maisha.

416 Sasa angalieni. Kwa imani Habili aliuona ule ufunuo, lile ono, naye akaleta damu iliyo hai, inayotiririka, kwa sababu uhai ulikuwa katika damu.

417 Uhai uko kwenye shina la—la ua. Na ni uhai wa mimea, ambao hauna hisia. Nilikuwa na tumaini hilo lingezama ndani.

418 “Habili, kwa imani,” akidumu na Neno. Kwa imani, sio kwa hekima. “Kwa imani yeye aliona kwamba ilikuwa ni kujuana kimwili, damu.” Chembe ya damu hutoka kwa mume. Mwanamume ndiye aliye na seli ya damu katika mbegu za kiume. Himoglobini ndiyo damu, huja kupitia kwa mume. Naye Adamu alijua ya kwamba haikuwa ni matofaa, na mapichi, na viazi, ama chochote kilichokuwa, yaliyosababisha watolewe katika bustani ya Edeni, yaliyosababisha dhambi. Ilikuwa ni kujuana kimwili, damu, naye akatoa damu. Kwa imani akafanya hivyo, sio kwa hekima.

419 Mtu, kupitia kwa hekima, atawezaje kulielewa hilo, wakati Biblia yote na Kanisa lote la Mungu limejengwa juu ya ufunuo wa Kiungu, kwa imani? “Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu.” Mnaona?

420 Ha! “Loo,” wao wanasema, “hakika, tunaamini Hilo.” Basi Maisha ya Kristo yako wapi katika taratibu hizi? Maisha ya Kristo yako wapi? Pili. . . Inawapasa kuandika baadhi ya Maandiko haya. Mnaona? Uko wapi Uhai? Kama . . . Wao wanasema, “Vema, tunaamini. Tunaamini. Tunaamini.” Endapo mnaamini, basi . . .

421 Yesu alisema, “Ishara hizi zitafuatana,” sio kwamba huenda zikafuatana, “zitafuatana na hao waaminio.” Yesu alisema, “Kama mtu ananiamini Mimi, kazi nizifanyazo, yeye naye atazifanya. Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo yeye naye atazifanya.”

422 Hatachezacheza tu. Atazifanya. Inaweza kutendekaje? Kwa sababu, huo hapo Uzima wenyewe ulio katika Kristo, uko ndani yako. Hautatoa hekima yoyote; hautakua ndani yake. Hauna budi kuikana hiyo hekima, upate kuichukua i—imani. Imani katika Neno, sio hekima katika Neno. Imani katika Neno!

423 Shetani anayo hekima zaidi katika Neno hilo kuliko yeyote, wahubiri wote wakiwekwa pamoja, makasisi na kila kitu.

424 Yuna hekima zaidi, bali hawezi kuwa na imani. Imani italifanya Hilo liishi. Imani ingemfanya atubu, itamfanya aondoke kwenye dhehebu lake. Hum! Yeye anayo hekima, kwa hiyo anakaa tu nayo. Vema.

425 "Lakini Habili kwa imani aliona lilikuwa ni tendo la kujuana kimwili, naye akatoa damu, uhai wa damu, naye Mungu akaipokea."

426 Sasa, katika Timotheo wa Pili 2, 3, ilisema . . . Neno linawajia sasa. Litaanguka kwenye udongo mbaya hata hivyo. Mnaona? "Wana mfano wa utauwa, bali wakikana nguvu zake," nguvu za Roho Mtakatifu. Timotheo wa Pili 3, kama mnaliandika. Vema. "Wenye mfano wa utauwa."

427 Ishara za Roho Mtakatifu za Uzima wa Milele, wanazikana Hizo. "Watu hawapaswi kunena kwa lugha. La. Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu, ubatizo wa Roho Mtakatifu. Kitu hicho kilikuwa ni kwa ajili ya mitume." Wenye mfano!

428 Paulo alisema, akilitabiri. "Katika siku za mwisho, nyakati za mwisho, mambo haya yatatukia." Sio katika siku hizo. "Naye Roho anena waziwazi: katika siku za mwisho, nyakati za mwisho, wengine watajitenga na Imani," na mambo haya yote. Mnaona? Hilo hapo, "Wenye mfano huo wa utauwa."

429 Sasa, ishara za Uzima wa Milele za Roho Mtakatifu zinawezaje kukua katika mavumbi hayo ya kikanisa, ambapo hapana Roho wa maji, hata kidogo? Mnaona? Haziwezi kukua kwenye mashamba ya anasa za kimadhehebu, na hekima, na mizaha. Ishara na maajabu ya Mungu aliye hai yanawezaje kukua katika mwa—mwanamke asiye na adabu ya kawaida kutenda kama mama wa heshima? Ninataka kuwaulizeni hilo. Hizo zinawezaje kukua ndani ya mwanamume atakayesimama mimbarani na, kwa ajili ya riziki duni ama upendeleo wa kimadhehebu, angeukwepa Ukweli wa Mungu? Ishara za kiroho zinawezaje kumfuata huyo? Haiwezekani.

430 Inawezaje—inawezaje kukua katika mhubiri atakayelishusha dhehebu lake kule chini, awavue nguo, ufukoni kule? Na hapa hivi majuzi usiku, mahali fulani ndio kwanza nipitie jana usiku, katika parokia fulani, na kufanya dansi kubwa ya shamrashamra mle ndani, wakipiga makelele, matunda ya Roho yanawezaje kukulia mahali kama hapo? Ni juu ya jiwe la kikanisa, hiyo ni kweli, wala si kwenye bonde la mateso, kuchekwa na kudhihakiwa.

431 Yungiyungi hufanya bidii sana. Mnakumbuka mahubiri yangu sio muda mrefu uliopita, miaka michache iliyopita, juu ya Bw. Yungiyungi. Anafanya kazi kwa bidii. Ambapo, Yesu alisema, "Jinsi yeye . . . anavyofanya kazi, wala hasokoti, na hata hivyo nawaambia: kwamba Sulemani, katika fahari yake yote, hakuvikwa vizuri kama moja." Jinsi ambavyo yungiyungi hilo huvuta, kujifanya la kupendeza, (kwa kusudi gani?) lipate tu

kuwa likitoa. Wapitaji, wananusa, wananusa manukato. Nyuki huruka moja kwa moja hadi moyoni mwake na kuchukua asali yenyewe kutoka kwake. Yeye huitoa tu bure. Anasumbuka, kufanya hivyo.

432 Haleluya! Huyo ni mtu halisi wa Mungu, Mchungaji Yungiyungi, Kasisi Bw. Yungiyungi, naam, bwana, anayefanya kazi ngumu kwenye Neno, anainama usoni mwake na kumlilia Mungu, "Mungu, siwezi kuona ambapo *hili* litakutana *hapa, hapa*. Halina budi kuja kwa Neno." Unapoliona, Naye Mungu anakupa wewe, basi nenda zako ukiwa huru. Sio kufanya uamsho mkubwa, "Kama mkinihakikishia dola elfu kadhaa, nitakuja." Lakini, bure, "Kama ni Timbuktu ama popote pale, Mungu, mahali unaponitaka nipande Mbegu, nitaitoa Hiyo bure." Haleluya!

433 Yesu alisema, "Sulemani, katika fahari yake yote, hajavikwa vizuri kama hilo." Kasema, "Fikirini yungiyungi."

434 Maskini jamaa mdogo, inamlazimu kuteseka kama kila kitu, apate kile anachopata, na kuchekwa na kudhihakiwa. Na makanisa yote makubwa yalimtupa nje, na kumwita kila namna ya majina machafu. Lakini yeye hudumu moja kwa moja na Neno hilo, akifanya kazi kwa bidii, mchana na usiku, amelala bondeni. Kitu gani? Yeye—yeye yupo mahali ambapo anaweza kuvuta kutoka kwenye "mito ya Maji." Kufanya kazi kwa bidii, (kwa kusudi gani?) kutoa. "Mmepokea bure, toeni bure." Naam, bwana. Loo, jamani!

Inawezaje kukua katika shamba hilo la mavumbi juu ya mwamba huo wa kikanisa?

435 Watoto wa Kaini walikuwa ni hekima, kisayansi. Waangalie watoto wa Kaini sasa wanapojitokeza. Hebu tuwaangalie kwa dakika moja. Watoto wa Kaini, walikuwa ni nini? Wajenzi, wavumbuzi, watu mashuhuri wa sayansi. Walikuwa na hekima. Mnaona? Wa—wa—walijenga hata mijengo, na kutengeneza chuma, na kuzitia matiko pamoja. Walikuwa ni wanasayansi, werevu, wenye elimu, na wa kidini.

436 Lakini zao hilo la hekima lilizaa nini? Mauti, kwa jamii yote, hapo hukumu za Mungu ziliposhuka. Hiyo ni kweli? Kundi—kundi hilo lilifanya nini? Lilisababisha mauti. Ingawaje, katika hekima yao yote na werevu, ilikuwaje? Walikufa. Kila mmoja wao aliangamia katika hukumu ya Mungu. Hiyo ni kweli? Mungu alisema hivyo. Walikuwa ni werevu, wameelimika sana, wamestaarabika, wa kidini, wazuri sana. Werevu, wenye elimu, walioitegemea hekima yao, nao wakaangamiza jamii nzima ya watu.

437 Jambo lile lile wanalofanya sasa hivi, mabomu yao ya atomiki na kadhalika, ambapo hawa wanasayansi werevu na kadhalika wata—wataiangamiza jamii yote. Wanazo cheche za mnururisho sasa hivi. Ni—ni . . . Unayaunguza tu macho yako

kabisa, zinakupa kansa, kila kitu. Waliachilia za kutosha, baharini, hata hawawezi kuzipata tena. “Zitakapoachiliwa, zitauangamiza ulimwengu wote,” wanasema. “Watu watateketea, katika miili yao.”

438 Si ajabu, Biblia ilisema, “Nao ndege wa angani wataila miili ya majemadari,” na kadhalika; kuoza, kutokana na cheche za mnururisho, kila kitu kingine.

439 Wanafanya hivyo, wenyewe, hekima yao ya kielimu. Hiyo ndiyo iliyosababisha mauti kuja: hekima ya kielimu. Iweni rahisi, liaminini Neno la Mungu, mpate kuishi. Ichukueni hekima yenu, mpate kufa. Vema. Mavuno, wakati wa mwisho, wanaangamia.

440 Vema, watoto wa Habili walikuwa wanyenyekevu, wakulima, wachunga mifugo; wachungaji, mnajua. Wachunga mifugo, wakulima, wanyenyekevu, hawakudai kuwa werevu, bali walidumu tu na Neno. Walizaa nini wakati wa mwisho? Nabii. Walimzaa. Nabii, kwa sababu gani? Ishara za wakati wa mwisho.

441 Wakati Nuhu aliposimama katika mlango ule, akiijenga ile safina, yeye alisema, “Inakuja, mvua.” Aliitwa mlokole, bali alikuwa nabii. Amina. Yeye alifanya nini? Alileta wokovu kwa wale wanaoamini, na wale waliotaka kuepuka. Huyo ndiye jamii hiyo nyenyekevu, isiyo na elimu ilizaa, iliyoamini katika imani. Wengine waliamini katika maarifa, wakaleta mauti, kwa jamii yote. Wale—wale wanyenyekevu walifanya nini kwa imani? Walileta wokovu, nabii wa Bwana, aliyewapa ishara ya kwamba wakati wa mwisho ulikuwa umewadia.

442 Mnafikiri wenye elimu wangeliamini? Waling’aka pua yao wakaondoka, kasema, “Kwani mvua inatoka wapi? Kisayansi nithibitishie palipo na maji yoyote huko juu.” Hao wanasayansi, kundi la werevu bandia, wakijaribu, kuthibitisha kisayansi hakuna Mungu. Jaribu!

443 Wakati *ile* picha ilipopigwa, hiyo iliwabwaga chini kutoka kwenye stuli yao walipokuwa wameketi. Asingeweza kuelewa. Kasema, “Kuna namna fulani ya Nuru iliyoigusa lenzi.” Hicho hapo chombo chao wenyewe cha kisayansi, kilichopiga picha Yake, ile kamera. Kama vile George Lacy alivyosema, yeye alisema, “Bwana,” kasema, “kamera hii haitapiga picha saikolojia. Nuru iliigusa lenzi. Ilikuwako.” Kasema, “Kwamba Hiyo ni nini, siwezi kukwambia, bali ipo.” Kasema, “Nitaandika jina langu kwake.” Akaandika. Nanyi mnayo, ninyi wenyewe. Naam, bwana. Hiyo ilikuwa ni FBI. Mnaona?

444 Mungu wetu, katika siku hizi za mwisho, hafanyi mambo juu juu, bali anaonyesha ulimwengu huu hauwezi kusimama. Hekima na maarifa yanakua, yakiruka hewani kasi kama nzi, na—na ndege za jeti, na kupigana chini ya maji. Na namna zote

za upotovu, huku wakiishi katika dhambi, wakijaribu kujenga kitu fulani kitakachowalinda.

445 Kipo kitu kimoja pekee: haki ya Mungu inasimama Mlangoni mwa Safina. Mlango ni nani? Kristo alisema, "Mimi ndimi Mlango wa zizi la kondoo." Nilisoma somo langu. "Kondoo Wangu wataisikia Sauti Yangu. Mgeni hawatamfuata." Kamwe hutamvuruga mmoja katika madhehebu hayo yote huko nje. Yeye atatoka ndani yake, hakika kabisa. "Nitawachukua kutoka kwenye kundi, nami nitawaongoza. Nitawatangulia." Amina. "Watajua ni Mimi. Hakuna mtu anayeweza kutembea kama Mimi, hakuna mtu anayeweza kufanya mambo nifanyayo," Yeye angesema. Amina.

446 "Rabi, sasa tunajua Wewe umetoka kwa Mungu, maana hakuna mtu anayeweza kufanya miujiza hii ufanyayo Wewe Mungu asipokuwa pamoja naye." Mnaona? Hiyo ni kweli. Maungamo ya Nikodemo. Jambo ndilo hilo.

447 Maskini jamii hiyo ndogo nyenyekevu ilitoa nabii. Naye nabii huyo, katika siku za mwisho za watoto wa Habili, alitoa nabii ambaye alionyesha ishara za siku za mwisho na kutoa onyo.

448 Ni karibu tu vivyo hivyo sasa, nafikiri. "Aliye na sikio kusikia, na asikie yale Roho anayotuambia."

449 Kwa hiyo, mnaona, Mbegu Neno la Uzima haiwezi kukua katika mazingira ya namna hiyo ya hekima. Kamwe haiwezi kukua.

450 Musa na Yoshua walikuwa na imani katika Neno. Hao wengine walitaka kucheza dansi na kuwavua wanawake nguo; Kora, (kwa nini?) kwa hekima yake ya Kimisri. Musa hakutaka hilo.

451 Waangalie hawa akina Kora siku hizi, wakifanya njia rahisi, kucheza dansi, karamu za usiku kucha; wanawake: waliokata nywele zao, nguo fupi, chochote. "Haileti tofauti yoyote. Hilo ni sawa." Si sawa. Neno linasema si sawa. Hiyo ni kweli. Kitu kile kile. Mnaona?

452 Ingawa kila mmoja wao alibatizwa, kila mmoja, Kora na hao wote walibatizwa, inaonyesha kwamba kuna aina hiyo ya kikanisa tena.

Unasema, "Ati walibatizwa?"

453 Wakorintho wa Kwanza 10:1 hadi 2. Hebu tulisome tu. Sisi...Ninajua inachelewa, lakini chakula cha jioni hakitaungua. Chakula hiki cha jioni huenda kikaendelea mbele kidogo, kama Bwana ataendelea tu kutulisha. Mnaona? Wakarintho wa Kwanza 10. Sasa angalieni hapa. Wakorintho wa Kwanza 10:1 hadi 2, nimeipata. Sasa, nimepata Wakorintho wa Pili. Wakorintho wa Kwanza 10:1 hadi 2.

Kwa maana, ndugu zangu, sipendi—sipendi ninyi *mkose kufahamu ya kuwa* zetu. . .*baba zetu walikuwa wote chini ya wingu, wote wakapita kati ya bahari;*

Wote wakabatizwa wawe wa Musa katika wingu na katika bahari;

454 Kora alikuwa na ubatizo ule ule ambao hao wengine walikuwa nao. Lakini yeye alitaka kufanya nini? Kuwaacha wanawake wacheze dansi, nao wakanywa divai kidogo wakawa na wakati mdogo, kuwavua nguo na kufanya uzinzi, na kuwa na hilo. Mnajua Biblia ilisema walifanya hivyo. Waliwachukua wanawake hao na kuwavua nguo, na kuwafanya wacheze dansi, na vitu kama hivyo. Naye Musa akawakasirikia. Mnakumbuka wakati huo? Kwa nini? Walikuwa na Dk. Kora huko, aliyekuwa na hekima. Akasema, "Nitawarudisha Misri." Huko ndiko wangalikuwa wameenda, pia.

455 Lakini, Ndugu Musa, wakati aliposhuka, ilikuwa ni tofauti. Yeye pamoja na Yoshua walidumu na Neno hilo. Mungu alitoa ahadi; wakadumu nayo. Vema.

456 Wengine walitaka kucheza dansi na kuvua nguo zao, na kutoka, kwa hekima ya Kora. Nao wote walipata ubatizo, mmoja.

457 Israeli na Moabu. Loo, ninaninii tu. . .ninyi. . .nimepitia hilo, wakati mmoja. Hatuchukui hilo. Sina budi kuharakisha. Vema. Israeli na Moabu, mnajua jinsi ilivyokuwa kule. Mmoja, mzuri vivyo hivyo, mtu mwenye hekima, madhehebu makubwa mno. Huyo mwingine, mdogo, baina ya madhehebu.

458 Ndipo, siku moja; ambapo ndipo nitapafikia sasa kabla hatujafunga. Siku moja, asili hizi mbili kuu, ama nguvu, zilikutana kwa ajili ya mashindano ya kuamua juu ya Neno la Mungu.

459 Sasa tutafikia kwenye upeo. Tungeweza kurudi nyuma. Ningeweza kuchukua dazani moja. Ningeweza kusimama hapa juma moja, hata nisiguse sehemu yake ya juu, jinsi ambavyo ninaweza kuthibitisha papo hapo, yale ninayozungumzia. Lakini natumaini mnalipata. Mnaona?

460 Siku moja, ilifikia kwenye mashindano ya kuamua. Hekima na imani zilifikia kwenye mashindano ya kuamua. Yesu na Shetani wakakutana. Hiyo ni kweli. Yesu na Shetani wakakutana. Nguvu hizi mbili kuu, hekima na maarifa, zilifika kwenye mashindano ya kuamua. Mnaona?

461 Sasa, wote wawili walilitumia Neno. Hiyo ni kweli? Loo, ndugu, hili linakuwa zuri, kwangu mimi. Mnaona? Msilikose, sasa. Loo! Semeni, "Mungu, ufungue moyo wangu." [Kusanyiko linasema, "Mungu, ufungue moyo wangu."—Mh.]

462 Wote wawili walilitumia Neno la Mungu, Biblia ile ile. Lakini halitafanya kazi katika mkondo usioongoka. Hakika

halitafanya kazi. Bila shaka halitafanya kazi. Wote wawili walitumia Neno la Mungu. Lakini Shetani alilitumia kutoka kwa maarifa ya kichwani, mnaona, maarifa ya kichwani, nalo halikufanya kazi.

463 Ninalo Andiko hapa. Mtajali kama nikilisoma? [Kusanyiko linasema, "La."—Mh.] Hebu tuchukue Waebrania, mlango wa 4, upesi sana, kwa dakika moja. Ninataka kusoma hili. Lilionekana zuri sana kwangu, papa hapa, Waebrania 4. Basi hebu tufungue Waebrania 4, na tuanzie, 1 hadi 2.

> *Basi ikiwa ikaliko ahadi ya kuingia . . .* kuingia *katika raha yake, na tuogope,* kusudi *mmoja wenu asije akaonekana ameikosa.*
>
> *Maana ni kweli sisi nasi tumehubiriwa habari njema vile vile kama hao: lakini neno lile lililohubiriwa halikuwafaa hao, kwa sababu halikuchanganyika na* (maarifa, hekima?) *imani ndani yao . . . imani ndani yao* (nini?) *waliosikia.*

464 Unaweza kuwa na Neno lote, unaweza kulijua Neno hilo kutoka A hadi Z, nalo kamwe halitafanya kazi kwako. Hivi mmewaona watu wakilichukua Neno hilo na kujaribu kulifanya Hilo litende kazi, waseme, "Ndugu, utukufu kwa Mungu"? Kamwe halitafanya kazi. Huwezi kujipumbaza na Neno. La, la. La, la. Haijalishi unakiri nini, Neno hujishuhudia Lenyewe. Haijalishi unadai nini, Neno hutoa ushuhuda. Hiyo ni kweli.

465 Sasa, Shetani alijua Neno. Alilijua Hilo kutoka A hadi Z. Vema, mwajua nini? Ningewazia, kama angekuwa na digrii, angekuwa na sifa za kutosha kuzinyosha kwenye kurasa tatu ama nne za karatasi, "Dk., Kasisi, Mzee, Ph., L.L., Q.D.," alfabeti zote kwa kila njia. Digrii yake ingekuwa katika Biblia hiyo. Anajua kila Neno Lake. Hakika anajua. Mnaona? Kwa hiyo, Shetani alisema, "Sasa, ninalijua Neno." Ninajua alilijua Neno wakati alipomjia Hawa. Kwa hiyo, alikuwa nalo kwa maarifa ya kichwani, bali lisingefanya kazi.

466 Yesu alilijua kwa imani, katika ufunuo wa Neno la Mungu katika Maisha Yake Mwenyewe yaliyokusudiwa tangu zamani. Utukufu! Natumaini hilo litakolea mpaka ndani ya moyo wako. Yesu alijua Yeye alikuwa ni Nani. Shetani alikuwa akishangaa. Yeye alijua kwamba alikuwa ni Kiumbe cha Mungu kilichokusudiwa tangu zamani, kwamba Mungu Mwenyewe alidhihirishwa ndani Yake. Haikuwa ni Yeye akizifanya zile kazi. Ilikuwa ni Baba aliyekaa ndani Yake. Amina.

467 Acha ibilisi aruke pamoja na thiolojia yake yote. Yesu; Shetani alijua Hilo. Yeye alilijua Neno. Sasa, angeweza kulinukuu Andiko hilo, jamani, kama tu Biblia inayotembea. Yeye angeweza tu kuinukuu namna *hiyo*. [Ndugu Branham alidata kidole chake mara nyingi—Mh.] Mnaona?

468 Lakini Yesu alisimama tu kimya, kwa kuwa Yeye alijua mahali alipokuwa amesimama. Alijua kwamba alikuwa amekusudiwa tangu zamani, "alikuwa ni Mwana-kondoo aliyechinjwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu." Alijua Yeye alikuwa ndiye Mtu yule. Loo! Loo, ndugu! "Aliye na sikio, na asikie." Yeye alijua ya kwamba alikuwa amekusudiwa tangu zamani kwa ajili hiyo, na hivyo ndivyo alivyolijua Neno. Mnaona? Nalo likatenda kazi. Hakika.

469 Shetani alililijua kwa hekima. Likashindwa. Alinukuu Neno lile lile Yesu alilonukuu, Biblia ile ile. Yeye alinukuu kutoka kwenye Zaburi. "Atawapa . . . Imeandikwa," Shetani akasema, "Atakuagizia Malaika zake, usije wakati wowote ukajikwaa mguu Wako katika jiwe. Watakuchukua."

Yeye akasema, "Imeandikwa pia . . . " Loo! Mnaona?

Shetani alililijua kwa maarifa.

470 Yesu alililijua kwa ujuzi. Alililijua kwa ufunuo. Yeye alijua kwamba alikuwa ni Mwana wa Mungu aliyekuwa aje ulimwenguni. Alijua msimamo Wake. Alijua alizaliwa katika ulimwengu huu kwa kusudi hilo. Na hiyo ndiyo sababu Neno la Mungu lingeweza kufanya kazi kupitia Yeye, kwa sababu Yeye alijua kile alichokuwa. Utukufu! Mmelipata kufikia hapo? Alijua alichokuwa.

471 Shetani, nyuma yake, alijua kile alichokuwa. Pia alijua hakuwa na shughuli yoyote, kwa hekima yake, juu ya Neno, kwa sababu Neno lilikuwa ni Mungu. Mnalipata?

472 Sasa, kama Yesu alijua kwamba Yeye alikuwa ni Nani . . . Yeye alikuwa ni Kiumbe cha wakati kilichokusudiwa tangu zamani. Mnaamini hilo? Yesu, yule mvulana, Yeye alijua alikuwa ni Neno lililokusudiwa tangu zamani, ule Utu wa Mungu uliokuwa usimame kwenye siku ile, upate kuwa Dhabihu kwa ajili ya dhambi. Naye alimjua adui Wake. (Kama nilivyohubiri, Jumapili kadhaa zilizopita.) Alimjua adui Wake; na Yeye alijua alikuwa ni Nani. Kwa hiyo, nguvu hizo mbili kuu zikaja pamoja, maarifa na imani. Yesu alijua Yeye alikuwa ni Nani.

473 Shetani aliijua Biblia vizuri kadiri Yesu alivyoijua, bali isingetenda kazi kwa Shetani. Mnaona?

474 Haijalishi ni kiasi gani cha maarifa uliyo nayo, halitafanya kazi. Sasa, rejesha hilo kwa baadhi ya haya madhehebu makubwa. Liwazie, kwa dakika moja. Wanasema, "Vema, tunalo Neno." Hebu nilione likifanya kazi. Ninyi Wakatoliki, mnasema ninyi ni wa asili. Hebu tulione. Nionyesheni kazi zenu, bila ya . . . Ama, nionyesheni kazi zenu, kwa, ama, pasipo na imani yenu, nami nitawaonyesha yangu, kwa imani yangu. Mnaona? Oneni yale Neno liliyosema.

475 Unaweza kupanda mbegu bila hiyo kujidhihirisha kwamba ni kitu gani, endapo inamea? Unaweza kupanda punje ya

mahindi bila kutengeneza mahindi, kama ikikua? Unaweza kupanda viazi isipokuwa viazi vikue? Unaweza kupanda ua na lisiwe ua la aina hiyo? Mnaona?

476 Basi, kama wewe umepandwa, nayo Mbegu ya Mungu imo moyoni mwako, halina budi kutoa Hilo. Yesu alisema, "Yeye atafanya kazi Zangu, kama ananiamini Mimi." Kama anasema analiamini Hilo, nazo hizi hazimfuati, yeye ni mwongo. "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya; hata nyingi zaidi ya hizi, kwa kuwa ninaenda kwa Baba Yangu." Mbona, lina nguvu! Kama hawafikii kwenye mahali pa kutelezea na kuteleza, wanatupwa penye jiwe fulani mahali fulani! Wanaanguka tu bondeni kusudi upepo usiweze kulipeperushia mbali, nao ndege hawatalifikia, litakua.

477 Lifiche ndani ya moyo wako. Daudi alisema, "Nimeificha sheria Yako moyoni mwangu," kwa hiyo hakuna dhehebu linaloweza kuichukua, ndege hawawezi kuliokota Hilo. "Nimelificha Hilo *hapa*. Ninalitafakari, usiku na mchana. Zimeandikwa kwenye nguzo za kitanda changu na kila mahali. Ninazo Hizo, nimezifunga kwa vidole vyangu. Ziko kwenye . . . "

478 Naye Yesu alisema, "Jina lako liko kwenye kiganja cha mkono Wangu." Kwa hiyo, namna gani, litasahaulika namna gani? Haiwezekani. Sasa, vema.

479 Basi, kama Yesu alimshinda Shetani juu ya imani, akijua Yeye alikuwa ni Nani, Yeye alikuwa ni Kiumbe kilichokusudiwa tangu zamani. Mko tayari? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Vipi kuhusu Bibi-arusi wa Yesu Kristo aliyekusudiwa tangu zamani sasa? Mnaamini Bibi-arusi amekusudiwa tangu zamani? Bibi-arusi wa Kristo aliyekusudiwa tangu zamani sasa, lile Kanisa, Neno Mbegu, pamoja na kila kitu alichoahidi Mungu kukiweka ndani ya Kanisa, ndani Yake sasa hivi. Liko ndani Yake sasa. Kila kitu kiko katika utaratibu. Roho Mtakatifu ametolewa. Mbegu imepandwa. Nuru za jioni zimekuwa zikimulika. Ishara ya Sodoma, ambayo Yesu aliahidi, ipo hapa, na Malaki 4. Kanisa lililokusudiwa tangu zamani!

Loo, ibilisi!

480 Kanisa la Mungu aliye hai, hapa na kwenye kanda, pia, mnajua mahali mnaposimama? Mnajua ya kwamba mliitwa na Mungu, ya kwamba Roho Mtakatifu anatawala moyoni mwenu, na kila Neno la Mungu ni halisi kwenu? Loo, ndugu! Shetani atawezaje kusimama dhidi ya hilo? Atawezaje kukomesha hilo lisikue? Atawezaje kuzizuia ishara hizo zisilifuate Hilo? Mbona, ungeweza kuwatupa gerezani. Wao, kama ungeweza, sijali kile ufanyacho, wamekwisha lijaribu. Waliozea gerezani. Walilishwa kwa simba. Walikatwa kwa misumeno. Waliraruliwa vipandevipande. Huwezi kuliua Hilo, kweli, Kanisa ambalo limekusudiwa tangu zamani. "Wale aliotangulia kuwajua," kama alivyofanya Yesu, "Yeye amewaita. Hao aliowaita,

amewahesabia haki. Na wale aliokuwa amewahesabia haki, Yeye amewatukuza, kuwakusudia tangu zamani.”

481 Na sasa, katika siku za mwisho, huku kila mbegu imepandwa; kila kitu katika utaratibu, ulimwengu katika utaratibu wake, wakati umejipanga, Kanisa liko katika utaratibu Wake, Mbegu, Nuru za jioni, ishara za kama alivyosema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma.” Malaika wa Mungu, Roho Mtakatifu, akishuka, akitenda kazi, akifanya ishara ambazo alizifanya wakati huo. Malaki 4 iliahidi Yeye atatuma, katika siku za mwisho, kile alichoahidi. Nasi tunaona hayo yote papa hapa. Wapi? Wapi?

Amina! Amina! Amina! Amina! Amina!

Mnampenda? Amina!

482 Hakika, papa hapa katika siku za mwisho, Kanisa lililokusudiwa tangu zamani, likijua mahali wanaposimama, limepandwa Mbegu, Roho Mtakatifu Kanisani. Shetani, kuwa mwangalifu.

483 Ni jambo gani lililotukia? Hebu kidogo tu sasa. Ni jambo gani lililotukia, pamoja na kila kitu kilichoahidiwa Kwake, hata ahadi za Malaki 4?

484 Shetani a—alifanya nini alipokutana na Yesu? Alimrukia, kwa nguvu zote za kikanisa alizokuwa nazo. “Ninalijua Neno, pia,” akamrukia. Hayo mavumbi ya kimadhehebu aliyokuwa nayo! Tulimrushia; bali hayakuwa na Uzima wowote. Hivi alipata kuruka! Aliondoka haraka kuliko alivyoruka. Kwa nini? Yeye aligusa huo Waya wenye volti bilioni mia moja pale. Akayaunguza manyoya yake. Akamwondokea. Akatoka Kwake, maana Waya huo ulikuwa na volti ndani Yake.

485 Kumbukeni, Shetani alikuwa na waya, pia. Lakini, haidhuru waya wa shaba nyekundu ni mzuri jinsi gani, kama hauna uhai ndani yake, umekufa. Hautafanya kazi. Waya ule ule.

486 Mmoja umetiwa nguvu kwa Dainamo, na huo mwingine haujaunganishwa, hata kidogo. Hiyo ni kweli. Hiyo ndiyo sababu itafanya kazi katika chombo kilichokusudiwa tangu zamani. Hiyo ndiyo sababu Neno litafanya kazi ambako limeunganishwa. Kuunganishwa wapi, pamoja na dhehebu? La, bwana. Hiyo ni soketi iliyokufa, “Lenye mfano wa utauwa, likikana nguvu zake.” Lakini limeunganishwa na Neno, ambalo halitapita kamwe, na linaweza kutoa nguvu zile zile ambazo Yeye alikuwa nazo. Hapo ndipo lilipo. Utukufu!

Amina. Amina.

Je, mnampenda? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Mtamtumikia? [“Amina.”] Amina. Hakika.

487 Halijashikamanishwa na dhehebu fulani, bali limeshikamanishwa katika hii—hii—hii—hii Dainamo hapa.

Ndugu, ninakwambia, linafanya kazi pale, kwa kuwa limeunganishwa, Neno lile lile.

488 Moabu alikuwa ameunganishwa mle, pia; nayo Israeli iliunganishwa, pia. Moabu hakuwa na kitu ila lundo la kanuni za imani na nabii wa uongo.

489 Lakini Israeli ilikuwa na mwamba uliopigwa, nyoka ya shaba, Nguzo ya Moto, haleluya, ishara za Mungu aliye hai. Amina. Hiyo ni hakika. Ilifanya kazi. Kwa nini? Ilikuwa ni imani. Naam, bwana. Sio juu ya maarifa, baadhi ya kanuni za wanadamu; bali juu ya imani katika Neno, Neno Lenyewe. Uzima hutokana na Neno. "Neno Langu ni Uzima." Huo umeme unakuja kupitia kwa Neno.

490 Shetani alitokea hapo, upesi sana. Mavumbi yake ya kithiolojia hayakusaidia sana papo hapo. Waya wa Shetani haukuwa na umeme ndani yake. Ulikuwa ni kanuni za imani zilizokufa. Hautafaa kitu. Hautatoa umeme.

491 Sasa, mnaona, ni waya ule ule. Yesu alitumia Neno la Baba; Shetani alitumia Neno la Baba. Shetani alikuwa ni Shetani. Yesu alikuwa ni Mungu, hiyo ndiyo tofauti, hiyo ni Kweli. Mmoja ni kanuni za imani, Huyo mwingine ni Neno. Mmoja ni wa Kweli, na huyo mwingine ni wa uongo. Mmoja atalitoa; huyo mwingine hawezi kulitoa. Mnalipata? Nyaya za namna ile ile, sasa, hiyo ni kweli kabisa, nyaya zile zile. Waebrania 2, ndio kwanza tupate, ama, Waebrania 4:2, ndio kwanza tulipate. Mnaona? Kama, kimadhehebu, kama madhehebu yanavyosema, kwa hekima. Mnaona? Madhehebu, kwa hekima, yanasema hili, "Siku za umeme zimepita."

Mnampenda? Amina!
Mtamtumikia Yeye? Amina!
Mnamwamini Yeye? Amina!
Amina! Amina!

Ninamwamini. Naam, bwana. *Amina* linamaanisha "na iwe hivyo."

492 Bwana, maombi yangu, asubuhi ya leo, mchukue kila mwaminio hapa ndani na umvute umwingize ndani ya umeme. Loo! Weka Uzima ndani yake, acha alie na kuangaza utukufu wa Mungu. Naam, bwana. Washa umeme.

493 Mnajua ninaloamini? Mbegu imepandwa (Mnaamini hilo?) kwa ajili ya Kanisa hilo kuu. Ni kama tu nyaya zimewekwa kote jengoni, kila soketi imejaribiwa kwa Neno, loo, jamani, kila mahali pa kutokea pamejaribiwa na Neno. "Msione kama ni ajabu wakati majaribu kama moto yanapokuja. Ni kuwajaribu."

494 Kuna shoti kidogo hapo, utaanguka ardhini, ulipue swichi yote. Mungu hazitaki Kanisani Mwake. Hakutakuwa na swichi yoyote itakayolipuka wala fyusi kulipuka katika siku hizi za mwisho. La, bwana.

495 Yeye anakuja na kuuchomelea mle vizuri. Naam, bwana. Vema. Kila taa inaning'inia mahali pake. Jambo pekee, tunamngojea Bwana huko nyuma aiwashe swichi. Hiyo ni kweli. Naam, bwana. Katika Neno! Hakika. Inaweza kuwa ni sasa hivi, ndugu. Kama unahitaji uponyaji, iguse tu hiyo swichi. Hivyo tu ndivyo inavyokupasa kufanya, endapo una waya halisi. Kama unganisho lako . . . "Kama waya wako umechimbiwa, na viunganisho, pia, vimepotelea ndani ya Yesu, atakwambia la kufanya." Amina. Hiyo ni kweli.

496 Sasa, hekima ya kimadhehebu inasema, "Siku za miujiza zimepita." Hakuna umeme kwenye hizo nyaya.

497 Bali imani inajua vizuri zaidi. Wanaihisi. Wanaiona ikifanya kazi. Wanajua inatoa nuru. Wanajua ifanyayo. Imani ndiyo umeme, ule umeme, Roho.

Nayo hekima ni taratibu za kimadhehebu.

498 Shetani alijaribu kumjaribu Yesu, kutoka kwa imani katika Neno la Baba. Hili hapa alilofanya. Alijaribu kumwonyesha madhehebu yake makubwa ya kikanisa, duniani. Bali asingeweza kumjaribu. "Njoo huku ukajiunge na langu. Nitakufanya askofu juu ya hayo yote."

499 "Imeandikwa . . . " kasema Yesu. Naam, bwana. Shetani asingeweza kumjaribu. La, bwana. Yeye amepita hayo. Lakini, Yesu alikuwa ni Neno. Imani Yake katika maarifa Yake Mwenyewe, kwamba Yeye alikuwa ni Neno.

500 Kama tu Musa. Mbona, Musa alijua kwamba Yeye alikuwa ni nani. Musa alijua yeye alikuwa ni mtumishi wa Mungu, alijua alikuwa ameitwa na Mungu. Alijua alilokuwa anaenda kufanya. Hiyo ndiyo sababu hakutishika yale Shetani aliyosema. Shetani alijaribu kumjaribu, kumwogopesha aliondokee. Lakini, la. Musa alijua mahali alipokuwa amesimama. Hiyo ni kweli.

Sasa sina budi kuharakisha. Ninaruka huku, ukurasa baada ya ukurasa, hapa.

501 Paulo. Jambo moja ninalotaka kupata hapa, kabla ya kufunga. Paulo aliliweka wazi kwa sehemu yake ya Bibi-arusi atakayoiwasilisha. Paulo atawasilisha sehemu ya Bibi-arusi. Mnaamini hilo? Paulo aliliweka wazi sehemu yake ya Bibi-arusi atakaowawasilisha kwa Yesu Kristo katika siku za mwisho, kuhusu hekima ama imani.

502 Hebu tusome tu kidogo. Ninawatakeni mfungue Wakorintho wa Kwanza, mlango wa 4. Wakorintho wa Kwanza, mlango wa 4, ndio kwanza tusome. Nasi tutafunga katika da—dakika chache tu, Bwana akipenda. Wakorintho wa Kwanza, mlango wa 4, nami ninataka kusoma kifungu cha 18 hadi cha 20. Vema. Haya basi.

Basi wengine wamejivuna, kana kwamba—kana kwamba siji kwenu.

> *Lakini nitakuja kwenu upesi, Bwana akipenda, nami nitafahamu, si neno la* yeyote wa *hao waliojivuna, bali nguvu zao.*

503 Mwajua, ingehitaji . . . Sasa, hilo lilikuwa ni kanisa la Kirumi lililoanza kuja, moja kwa moja mle ndani, likaanza kuja. Mnaona? Yeye alijua kile . . . Mwajua, Biblia ilisema, "Walitoka kwetu, kwa kuwa hawakuwa wa kwetu," mnaona. Hiyo ni kweli.

> *Maana ufalme wa Mungu hauji katika neno, bali katika nguvu.*

504 Unaona, "Si katika Neno." Kusema tu, "Vema, mimi, ninayo elimu, ndugu. Ninayo elimu nyingi kuliko utakayowahi kuwa nayo. Mimi—mimi ni kasisi. Mimi . . . " Hilo halina uhusiano wowote na Hilo. Halimaanishi zaidi ya wewe ni "nguruwe," ama chochote kingine; unaona, unaona, halina uhusiano wowote Nalo. Mnaona? Ibilisi alikuwa na maarifa mengi sana, pia. Mnaona? Vema. Mnaona?

> *Maana ufalme wa Mungu hauji . . . neno, bali . . . nguvu.* Mnaona?

> *Mtataka vipi* basi? *Nije kwenu na fimbo, ama katika upendo,* ama *katika . . . roho wa upole?*

505 Sasa, mlango wa 2. Ninataka kumaliza hili, kwa dakika moja tu, basi, kabla hatujafunga. Mlango wa 2; tufungue huo ukurasa. Hebu tuanzie papa hapa kwenye wa kwanza. Sasa angalieni yale, Paulo, yale anayomwambia Bibi-arusi sasa. Yeye ataiwasilisha sehemu hii ya Bibi-arusi kwa Kristo, naye anawataka wajue. Sasa, kumbukeni, Paulo angalikuwa kidogo ni mwerevu. Yeye alikuwa ni mwerevu, alikuwa, bali "ilibidi asahau hilo," alisema. Alikuwa na kila namna ya shahada na elimu, bali ilibidi asahau hizo, sasa, angalia, kumjua Kristo.

> *Basi, ndugu zangu, mimi* nilipokuja *kwenu, nilikuja,* sikuja *kwa ufasaha wa maneno, wala . . . hekima.* Mnaona? Sikuja na *hekima, nikiwahubiri siri ya Mungu.*

506 "Mimi ni Dr. *Fulani-wa-fulani,* nami nina yote. Mimi . . . Tunafundishwa katika seminari, *hivi-na-hivi*"? La, la. Paulo alisema, "Sikuja kwenu namna hiyo, kwa hekima." Sasa, na yale . . .

Somo langu ni lipi? *Hekima Dhidi Ya Imani.* Mnaona?

507 "Sikuja kwenu katika hekima," Paulo alisema, "kuwapa ushuhuda wa Mungu kwa hekima, kusema, 'Sasa angalieni hapa. Nawaambia. Tumesoma katika seminari ya kwamba siku za miujiza zimepita. Tumejifunza katika seminari ya kwamba mambo haya kweli hayakumaanisha *Hivi.*'" Yeye alisema, "Sikuja jinsi hiyo, ndugu zangu." Sasa yeye alisema nini?

> *Maana naliazimu nisijue neno lolote kwenu ila Yesu . . . naye amesulubiwa.*

Nami (kama) *nilikuwako kwenu katika hali ya udhaifu na hofu, na katika* dhiki kubwa nilikuwa pamoja nanyi.

Na ujumbe wangu na kuhubiri kwangu hakukuwa kwa maneno ya hekima ya mwanadamu yenye kushawishi akili za watu, . . .

508 Aha? Kama vile Booth Clibborn alivyosema, "Aloo?" Ni nani aliyebisha basi?

Sikuja kwenu pamoja na *hekima* fulani ya seminari, *bali kwa* yale *madhihirisho ya Roho na ya nguvu:*

Ili imani (i-m-a-n-i) *yenu isiwe katika hekima ya wanadamu, bali katika nguvu za Mungu.*

509 [Ndugu Branham anapiga mbinja—Mh.] Amina. Mnaamini hilo?

Ili imani yenu isisimame *katika hekima ya* dhehebu fulani, *bali katika nguvu za Mungu.*

510 Imani katika nguvu za Mungu! Matumaini yenu hayako . . .

511 Asili hizi mbili zimeshindana tangu Edeni; imani ya Mungu dhidi ya hekima ya Shetani. Mungu amethibitisha, katika nyakati zote, kwamba Hilo halitachanganyika. Halina budi kutenganishwa, lipate kukua.

512 Sasa, upesi, hebu nipitie neno mo—moja tu ama mawili, juu ya kila moja, nichukue tu mambo machache niliyoandika hapa.

513 Esau na Yakobo walikuwa ni mfano mkamilifu: wote wawili, wa kidini; wote wawili, mapacha.

514 Esau alikuwa ni wa namna ya kikanisa. Alikuwa ni mtu aliyekuwa mwerevu. Alikuwa na—alikuwa na msimamo mzuri wa maadili na vitu kama hivyo, bali hakuwa na haja na hiyo haki ya mzaliwa wa kwanza.

515 Yakobo hakujali kilichombidi kufanya, mradi tu alipata hiyo haki ya mzaliwa wa kwanza. Na mradi tu walikuwa pamoja, wasingeweza kuzaa. Hiyo ni kweli? Mmoja alikuwa dhidi ya mwingine.

516 Mmelishika? Amina. "Ondokeni miongoni mwao. Mkatengwe nao," asema Mungu. "Wala msiguse vitu vyao vilivyo vichafu. Nitawapokea." Mnaona?

517 Ilimbidi Yakobo kujitenga na ndugu yake wa kimadhehebu kabla Mungu kuweza kamwe kumbariki. Mungu alimwambia Ibrahimu jambo lile lile.

Israeli; na Moabu.

518 Wale manabii mia nne wa Israeli walisimama mbele ya Mikaya. Naye Mikaya akajitenga nao, naye akalipata Neno la Bwana, kisha akarudi Nalo.

519 Musa, na Kora, jambo lile lile, wasingechanganyana. Ilibidi watengane. Hiyo ni kweli?

520 Ibrahimu; na Lutu. Lutu alikuwa ni mtu wa kidini, mfano wa kanisa la kawaida. Lakini mradi tu Lutu alikuwa pamoja na Ibrahimu, yeye alisafiri kwa miaka kadhaa pamoja naye. Lakini Yeye angeninii. . .Mungu asingembariki mpaka alipomtii Yeye kikamilifu na kujitenga na Lutu, lile kanisa la kimadhehebu. Halafu, mara Ibrahimu alipojitenga na kutoka nje, kutembea peke yake, Mungu alisema, "Sasa, Ibrahimu, simama. Angalia mashariki, magharibi, kaskazini, kusini." Kasema, "Yote ni yako." Bali hakufanya hivyo mpaka alipojitenga kabisa. Hiyo ni kweli kabisa.

521 Mungu asingeweza kumbariki Sethi mpaka Yeye alipomtenga na Kaini. Alimtia alama Kaini na kumtuma kwenye nchi ya Nodi. Ndipo Kaini, kwa hekima yake ya kielimu, akawa wanasayansi na kila kitu kingine, akakuza zao la hiyo. Naye Sethi, chini ya haki yake, na upendo na imani katika Neno la Mungu, yeye alikuza zao lililomzaa nabii aliyetoa onyo kwa siku za mwisho, hiyo ni kweli, akamwokoa kila mwaminio. Nayo hekima ikamwangamiza kila mmoja wao. Wao, kila mmoja, akafa. Kila mmoja, haijalishi walikuwa na digrii ngapi na saikolojia, kila kitu kingine, waliangamia katika hukumu za Mungu.

522 Na kila kitu nje ya watu wa kweli, waliozaliwa upya kwa Roho wa Mungu, wanaoamini kila Neno la Hilo na wanalitetea, wataangamia katika hukumu za Mungu. Mnaona maskini hawa wanaojinengua wakishuka kwenda mtaani, na vurugu hizi zote, na kuendelea namna hiyo, kumbukeni, si kitu ulimwenguni ila chakula cha ile hukumu. Itaoza. Haina budi kuoza. Itaibidi tu kuoza. Enyi wanawake, amkeni.

523 Ninao ushuhuda mdogo, bali sina wakati wa kuusimulia, wa maskini mama mmoja hapa sio muda mrefu uliopita, huko California. Nilikuwa nikiendesha motokaa barabarani, nikingojea kuitwa kwenye hema. Nikaenda kule, kidogo. . . Ni—ni fedheha. Hapana shaka, maskini msichana mrembo. Naye alikuwa akitembea pale, akijinengua, amevaa kofia hii ndogo ya kaoboi, buti na mapambo yamening'inia, akijinengua barabarani. Kila mwanamume akimpigia mbinja, na kumpungia mkono, wote namna hiyo.

524 Nikawazia, "Ninapaswa tu kusimama, kama sikuwa mhubiri. Meda angalikuwa pamoja nami, ningesimama. Niseme, 'Angalia, dada, nataka kukwambia jambo fulani. Huenda ukawa ni mrembo. Unaweza kuthibitisha hilo. Unaona? Huenda ukaweza kuyafanya magari yafunge breki, huku ukijinengua hapa, nao wavulana wakipiga mbinja kama mbwa mwitu, kila kitu. Lakini moja ya siku hizi, maskini mwili huo, wadudu na mabuu yatatambaa waingie ndani yake na kuula. Na labda katika majuma sita tangu sasa itakuwa ni hivyo, umeoza, umelala pale kaburini. Bali nafsi hiyo iliyo ndani yako,

inayojilisha hiyo tamaa mbaya, itaishi kuzimuni mwa ibilisi kwa—kwa nyakati zijazo.'"

525 Musa; na Kora. Lutu; Ibrahimu. Yohana Mbatizaji; na watoza ushuru. Yesu; na makanisa ya kimadhehebu ya siku Zake. Mnaona? Imani; hekima.

Vema, hao makuhani wangeweza kusimama, waseme, "Sisi . . . "

Akasema, "Naam."

"Tunalo *hili*. Loo, baba yetu, sisi tulifanya *hili-na-hili*."

526 Kasema, "Naam. Ninyi, kwa mapokeo yenu, mmezitangua amri za Mungu, mkifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu."

527 Kasema, "Vema, Wewe ni nani, kutufundisha? Ulitoka shule gani Wewe?"

528 Akasema, "Kazi nizifanyazo, zinanishuhudia Mimi. Nisipozitenda kazi za Masihi, basi msiniamini. Na nikizitenda kazi za Masihi, basi mnajua, ziamininі hizo kazi." Kasema, "Zinanishuhudia Mimi. Nisipozitenda hizo kazi, basi msiamini."

529 Yeye alikuwa na hayo madhehebu, pia, kule nyuma, pamoja na hekima yao. Yesu alikuwa na imani. Imani katika nini? Kile Yeye alichokuwa: Mwana wa Mungu. Mnaona? Vema.

530 Mtakatifu Martin; pamoja na kanisa la Kirumi, katika siku za yale matengenezo. Lakini ninamaanisha wakati, hao, wakati kabla hawajaingia katika Rumi ya upagani, hapo lilipoanza kufanyika kanisa la Kirumi. Martin alisimama pale na kulipinga lile fundisho la sharti la kanisa hilo la Katoliki; akafanya ishara, na maajabu, na miujiza. Na—nayo makanisa yake, yote, yalinena kwa lugha, na kutabiri, na mambo makuu. Nazo nguvu za Mungu zilikuwa pamoja naye. Aliwafufua wafu na kuwaponya wagonjwa, na kila kitu kingine. Basi kulikuwako na kanisa lile la Katoliki huko, likampinga namna hiyo, na kujaribu kumchoma moto, na kila kitu kingine. Ilikuwa ni kitu gani? Hekima; imani. Vivyo hivyo sasa.

531 Hebu tusikie kilele chake chote. Zekaria 4:6 ndipo nitakapomalizia, papa hapa. Biblia ilisema, "Si kwa nguvu, si kwa uweza, bali kwa Roho Yangu, asema Bwana. Si kwa hekima, si kwa maarifa, si kwa kupendekezwa, bali kwa Roho Yangu nitaliimarisha (nini?) Neno Langu." Wale wanafunzi walipandiwa Hilo ndani yao, kisha Roho akaja kulitia nguvu hilo Neno. Mnaona? "Si kwa nguvu, si kwa uweza, si kwa hekima, si kwa ufahamu, si kwa *hili*, si kwa *lile,* bali kwa Roho Yangu nitalipa nguvu Neno Langu. Kwa Roho Yangu, asema Bwana." Ni Maji ya Neno la imani ndiyo yanayoliimarisha Neno la Mungu na kulifanya litende kazi.

532 Ni ipi itakayoshinda? Inaonekana, sasa hivi, hakika, kwamba hekima itafaulu. Lakini, haitafanya kazi. Haitafanya kazi.

533 Inaonekana hivyo, sasa hivi, ya kwamba Kanisa hilo dogo linaloliamini Neno lote la Mungu ha—hakika liko katika uchache. Lakini msiwe na wasiwasi. Biblia ilisema, "Msiogope, enyi Kundi dogo. Ni mapenzi ya Baba yenu kuwapa Ufalme." Aa-ha. Hiyo ni kweli. Mnaona? Wala msiogope. Dumuni tu katika imani. Dumuni moja kwa moja na Neno. Msiliache Neno. Dumuni na Neno.

> *Mnampenda?* Amina!
> *Mtamtumikia Yeye?* Amina!
> *Mtamwamini?* Amina!
> Amina! Amina!

Hebu na tuuimbe.

> *Mnampenda?* [Kusanyiko linaimba, "Amina!"—Mh.]
> *Mtamtumikia Yeye?* Amina!
> *Mnamwamini?* Amina!
> Amina! Amina!
>
> *Mnampenda?* Amina!
> *Mtamtumikia Yeye?* Amina!
> *Mtamwamini Yeye?* Amina!
> Amina! Amina!

534 Loo, ninampenda! Nanyi je? Ni kitu gani? Kwa imani, sio kwa hekima! "Kwa imani tumeokolewa." Hiyo ni kweli? "Sio kwa hekima, sio kwa maarifa; kwa Roho Yangu, asema Bwana."

535 Acheni Hizo zipenye ndani ya Kanisa hilo. Huo waya wa shaba nyekundu, ambao ni kipitishio. Sasa, waya wa alumini si kipitishio. Mnaona? Hapana. La. Bomba la mpira wa maji si kipitishio; ni kihami. Mbao ni kihami. Hatutaki vihami vyovyote. Tuna vingi kupita kiasi sasa, na hufanya matengano. Kwa hiyo tu—tunataka . . . Tunataka vipitishi, wanaume na wanawake waliozaliwa mara ya pili wanaoliamini Neno la Mungu.

536 Sasa, Dainamo ilisema nini? "Mwombeni Baba chochote katika Jina Langu, nitakitenda." Nawe unafanya nini? Unganisha plagi.

> Amina!

537 Hiyo ni kweli? Ingiza tu plagi, hivyo tu ndivyo unavyopaswa kufanya, nao umeme unakuja ukipitia kwenye waya moja kwa moja.

538 Nini kinachotukia? Neno linaanza kukua. "Naye atakuwa kama mti uliopandwa kandokando ya vijito vya maji; majani yake hayatanyauka; lolote afanyalo litafanikiwa. Wasio haki sivyo walivyo."

539 "Wasio haki sivyo walivyo." Sasa, usiseme, "mwenye dhambi," sasa. "Wasio haki," mnaona, hao ni wale wanaodai kuwa, nao ni wasio haki Kwake, mnaona. Hiyo ni kweli. "Sivyo walivyo wasio haki. Hawawezi kusimama hukumuni pamoja na wenye haki." La, bwana. Bila shaka hawawezi.

540 Kwa hiyo, wakati umewadia. Mbegu imepandwa, hata hivyo, hao waliokusudiwa tangu zamani. "Waliokusudiwa tangu zamani" ndiyo njia tu pale. Ningechukua Ufunuo 12, sasa hivi, na 13, na kuwathibitishia hilo, ni hao tu. Biblia ilisema, kwamba, "Huyu mpinga Kristo atakayekuja duniani atawadanganya wote," (w-o-t-e), "Wote waliokuwa juu ya uso wa dunia, pamoja na madhehebu haya na kanuni za imani. Angewadanganya wote walio juu ya uso wa dunia, kila mmoja wao, isipokuwa wale waliokusudiwa tangu zamani kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu." Kwa hiyo, ndugu, huwezi kutenda lolote kulihusu. Unapaza tu sauti, "Amina." Loo, jamani! Ninapenda hilo. Naam, bwana.

Mnampenda? Amina!
Mtamtumikia Yeye? Amina!
Mnamwamini Yeye? Amina!
Amina! Amina!

541 Ninawatakeni mjizoeze hilo kidogo huku, ninyi nyote. Ninaupenda wimbo huo, nanyi je? Huo ulikuwa ndio wimbo wetu wa mkutano, wa Phoenix. Loo! Ninaupenda. Ninaupenda. Hebu tuuimbe tena.

Mnampenda? Amina!
Mtamtumikia Yeye? Amina!
Mtamwamini? Amina!
Amina! Amina!

542 Vema, mnaweza tu kuendelea kuuimba, mwajua. "Mtamwabudu?" Na wote mwendelee tu, tena na tena. Jamani! Tuliuanzisha huko Phoenix; karibu tupararue mahali hapo kabisa. Naam, bwana. "Amina! Amina! Amina!"

Mmeingizwa plagi asubuhi ya leo? Amina!
Washa swichi. Amina!
Una umeme. Amina!
Amina! Amina!

Sasa Hilo litakua. Amina!
Lizae tunda. Amina!
Utalionyesha. Amina!
Amina! Amina!

543 Loo, huo si ni wa ajabu? Amina. Ni ajabu sana. Samahani kuwaweka nyote hapa, wakati huu wote, bali nina yubile tu, mimi mwenyewe, wakati wa ajabu sana. Vema.

Jumapili ijayo, sasa, kila mtu aliye huku . . .

544 Sasa, sasa nitapanda niende kwa Ndugu Littlefield, kueneza Neno kidogo, labda nichukue tu baadhi ya Neno hili hapa na kulieneza Hilo huko juu miongoni mwao, church of God, namna hiyo. Na labda nitazungumza tu juu ya jambo fulani nililozungumzia hapa. Hakika, mmekaribishwa kuja. Lakini wanalo kanisa dogo sana kule, linakaa watu elfu moja mia tano. Ndio kwanza niliweke wakfu, na yapata miaka kadhaa iliyopita. Litasongamana kabisa. Lakini nilimwahidi Ndugu Littlefield. Yeye ni ndugu wa thamani. Naye mtu hutimiza ahadi yake kama akiweza. Bwana akipenda, nitapanda huko juu.

545 Kutakuwako na kanisa hapa maskanini. Ninyi watu njoni papa hapa maskanini, mlio karibu na kadhalika, na mnaoweza. Njoni moja kwa moja.

546 Halafu basi, Jumapili ifuatayo, kumbukeni, Ndugu Arganbright atakuwa hapa sasa pamoja na Ndugu Rowe. Hakika mtamfurahia Ndugu Rowe. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Vema.

547 Hebu tuirejeshe ibada sasa kwa Ndugu Neville, tuone yale anayotaka kutwambia sasa. Bwana awabariki.

Hekima Dhidi Ya Imani SWA62-0401
(Wisdom Versus Faith)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumapili asubuhi, tarehe 1 Aprili, 1962, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org